

8 NOVEMBA, 2022

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Saba – Tarehe 8 Novemba, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, kwa niaba.

Na. 87

Ujenzi wa Barabara ya Moka - Mtumbikile – Matimba

MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. SALMA R. KIKWETE
aliuliza: -

8 NOVEMBA, 2022

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa barabara ya Moka-Mtumbikile - Matimba kwa kiwango cha changarawe?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete Mbunge wa Jimbo la Mchinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ilitenga Shilingi milioni 622.52 kwa ajili ya ujenzi wa *vented drift* yenye urefu wa Mita 45 na upana wa mita 7; ujenzi wa boksi kalavati kubwa katika mto Nangaru lenye urefu wa mita 26.8 na upana wa mita tisa; Kuchonga barabara yenye urefu wa kilomita 10.3, Kuweka changarawe kilomita mbili na kuchimba mifereji ya kuondoa maji barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia TARURA itajenga barabara ya Moka-Mtumbikile-Matimba kwa kiwango cha changarawe kadri ya upatikanaji wa fedha baada ya kukamilisha ujenzi wa vikwazo (*Bottlenecks*) vya barabara hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sanga.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, barabara hizi nyingi

8 NOVEMBA, 2022

za Nyanda za Juu Kusini zimekuwa na changamoto ya mvua ya muda mrefu, na barabara nyingi hazijafikiwa kiwango cha changarawe. Ni upi mkakati wa Serikali? Na ukifuatilia maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anazungumza na watu wa *TARURA* kwamba maeneo ya Kusini ambayo ni ya uzalishaji barabara hizo zijengwe kwa kiwango cha changarawe kwa wingi.

Je, ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba barabara hizi zinajengwa kwa kiwango cha changarawe, hususan kwenye Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Njombe hususani Wilaya ya Makete?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makete kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni kwamba moja tunataka kuwahakikishia tunapandisha hadhi barabara za udongo kwenye changarawe na pili, zile za changarawe kuzipeleka katika kiwango cha lami; na tunafungua barabara nyingi mpya. Kwa hiyo sehemu ya miradi mikubwa ambayo tumeielekeza katika Nyanda za Juu Kusini ikiwemo *Agri-connect* ni ujenzi wa lami ili maeneo hayo yaweze kupitika muda wote na shughuli za kiuchumi ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali ipo kazini na tutaendelea kuongeza fedha ili kuhakikisha hizi barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja zinafanyiwa kazi.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Kwa vile Waziri huyu anajibu swali namba 89, naruhusu swali namba 89 halafu tutarudi kwenye swali namba 88. Mheshimiwa Santiel Kirumba.

Na. 89

Hitaji la vyoo kwa ajili ya wanafunzi wa kike

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kujenga vyoo maalum kwa ajili ya wanafunzi wa kike katika madarasa mapya yanayojengwa ili wanafunzi hawa wasikose masomo pindi wanapokuwa kwenye siku zao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Santiel Erick Kirumba Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa matundu ya vyoo unazingatia mahitaji ya wamafunzi wote wakiwemo wavulana na wasichana pamoja na wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzingatia hili Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kuzisimamia na kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa pindi wanapojenga shule

8 NOVEMBA, 2022

mpya wazingatie kujenga matundu ya vyoo kulingana na michoro na ramani zote zinazotumwa kwao kwa kuwa ndani ya michoro hiyo imejumuisha chumba maalum cha wasichana kwa ajili ya kujisitiri wanapokuwa katika hedhi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kirumba.

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali; nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na watoto wengi wa kike kukosa masomo siku tano mpaka saba kwa hiyo kunasababisha kwa mwaka kukosa masomo kwa siku 50. Nini *commitment* ya Serikali katika madarasa haya mengi mapya ambayo hayana mfumo huu wa vyumba maalum?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Santiel Erick Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ameianisha hiyo changamoto, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi Ofisi ya Rais – TAMISEMI tunazielekeza halmashauri zote sasa kujenga vyumba ambavyo vinaweza vikawasaidia watoto wa kike kujisitiri wakati wa hedhi. Lengo ni kuhakikisha kwamba Watoto hawa hawakosi masomo wanapokuwa katika kipindi chao ili kuweza kuwasaidia kama ambavyo katika michoro yetu mipya ambayo tumeianisha.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante swali namba 88, Mheshimiwa Malecela.

Na. 88

Zahanati ya Kijiji cha Vunta kuwekewa bango la zahanati

MHE. ANNE K. MALECELA aliuliza: -

Je, Serikali inajua kwamba Zahanati ndogo ya Vunta iliyopo Kata ya Vunta kwenye Tarafa ya Mamba Vunta imewekwa bango la Kituo cha Afya cha Vunta badala ya Zahanati ya Kijiji cha Vunta?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Vunta kilichopo Tarafa ya Mamba Vunta ni miongoni mwa Vituo vya Afya sita vya Serikali vinavyotoa huduma kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Same. Kituo hicho kilipandishwa hadhi na kusajiliwa mwezi Januari, 2004 ambapo kilipewa msimbo namba 108286-6 na kinatambulika kitaifa kama Kituo cha Afya na si Zahanati.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Same ilitenga Shilingi milioni 20 kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ukarabati wa jengo la maabara ambapo ukarabati huo upo katika hatua ya ukamilishaji. Aidha, katika Mwaka 2023/2024 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Same itafanya ukarabati mkubwa wa Kituo cha Afya na kuongeza miundombinu ya huduma za upasuaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Malecela.

MHE. ANNE K MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nikiri kwamba sijaridhika na majibu ya Serikali. Kwa kuwa anavyoongea Waziri ni kama kweli Kata ya Vunta kuna kituo cha afya, lakini Kata ya Vunta kuna jengo ambalo Serikali ililirithi kutoka maendeleo ya jamii mwaka 1962 miaka 60 iliyopita. Je, Serikali katika hali ya namna hiyo, naomba uniambie Mheshimiwa Waziri, tena kiukweli, mna mpango gani wa kujenga kile Kituo cha Afya cha Kata ya Vunta?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu Ijumaa akimaliza kufunga Bunge hili mimi ninanyoosha, ninatangulia jimboni, wewe niambie unanifuata siku gani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anne

8 NOVEMBA, 2022

Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa namna ambavyo anapambana kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wanapata maendeleo lakini pia huduma za afya. Nimhakikishie ni kwamba Serikali ilishafanya tathmini ya vituo vya afya vyote vyenye miundombinu pungufu ya kutoa huduma za afya. Tuna vituo vya afya ambavyo havina wodi na havina majengo ya upasuaji. Serikali tumeandaa *database*; na nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Kituo cha Afya cha Vunta ni miongoni mwa vituo ambavyo tayari vimeingizwa kwenye *database* na vitatengewa fedha mwaka wa fedha 2023/2024 na tutapanua majengo yale ikiwemo kujenga jengo la upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita inafanya kazi hiyo na wananchi wa Same watapata huduma bora za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana la kufuatana na yeye, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge niko tayari kuongozana naye ili twende moja kwa moja Same tukapite Vunta na kuweka mpango kazi wa utekelezaji wa mpango huu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alifika Mbulu Vijijini na Mheshimiwa Waziri kwenye Kata ya Maga. Je, ni lini watatuletea fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha afya katika Kata ya Maga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumefanya ziara zaidi ya mara katika Jimbo hili la Mbulu, lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kumalizia vituo vya afya ambavyo havijakamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa vituo vya afya vipya tuangalie utaratibu baada ya kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya vya zamani lakini pia kupeleka vifaa tiba katika vituo hivyo.

NAIBU SPIKA: Ahsante ameshakuelewa. Mheshimiwa Munde, jiandae Mheshimiwa Mwakasaka.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nimeshawahi kuongea na Mheshimiwa Naibu Waziri mara kadhaa kuhusu kituo cha afya cha Une-Clinic Tabora, kwamba tunahitaji majengo ya upasuaji, *theater* na maabara ili

8 NOVEMBA, 2022

kiweze kuwa kituo cha afya, kwa sasabu akina mama wajawazito wanazaa pale, kama akina mama 200 kwa mwezi.

Je, Serikali ni lini sasa itatuletea hizo fedha ili tuweze kukamilisha Kituo cha Afya cha Kaoni Clinic?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Munde, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Munde amefuatilia suala Kituo cha Afya cha Town pale Tabora Manispaa; na alikuja pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa, tulikubaliana wafanye tathmini ya ukubwa wa eneo lililopo ili tuweze ku-*design* michoro inayoweza kukaa pale ili tujenge jengo la ghorofa ili wananchi wa Tabora Manispaa wapate huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba zoezi hilo linaendelea litafanyiwa kazi na Serikali.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Makasaka.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tabora Mjini lenye kata 29 ambalo ni kubwa sana kata nyingi za nje ambazo ni za vijijini zina upungufu mkubwa wa vituo vya afya, hasa katika Kata ya Uyui ambayo ina zahanati ambayo ingeweza Serikali ikaiboresha kuiweka kuwa kituo cha afya.

Je, Serikali inaahidi nini katika jambo hilo la kuzisaidia hizo kata za nje ya Mji wa Tabora?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Manispaa ya Tabora kama ilivyo katika halmashauri zote kote nchini kuna upungufu wa vituo vya afya kwa baadhi ya kata. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwanza tunakamilisha ukamilishaji wa vituo vya afya vilivyoanza ujenzi na kupeleka vifaa vifaa tiba na watumishi ili vianze kutoa huduma za afya. Baada ya hapo tutafanya tathmini ya maeneo ambayo ni kimkakati kwa ajili ya kujenga vituo vya afya vingine ikiwemo katika eneo hili la Uyui.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea swali namba 90, Mheshimiwa Tendega.

8 NOVEMBA, 2022

Na. 90

Mpango wa Uendeshaji wa Serikali kwa Uwazi

MHE. GRACE V. TENDEGA aliuliza: -

Je, ni kwa nini Serikali iliamua kujiondoa kwenye mpango wa uendeshaji wa Serikali kwa uwazi wakati silaha kubwa ya kupambana na rushwa ni uwazi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa Serikali kujitoa OGP haujaathiri uendeshaji wa Serikali kwa uwazi kwa kuzingatia ukweli kwamba Serikali inao utaratibu wa ndani wa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa uwazi wakati wote kwa kuwa na vyombo na taasisi zilizokasimiwa majukumu ya kusimamia na kufuatilia Sera ya Uwazi na Uwajibikaji. Mfano, TAKUKURU, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kujiunga na OGP ni hiari kwa nchi mwanachama na vilevile inaweza kujitoa kwa hiari. Kwa msingi huo Serikali iliamua kujitoa kwa hiari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ngazi za kimataifa, Serikali imeendelea kuwa moja ya nchi zilizoridhia mfumo wa kukaguana wa nchi za kiafrika *APRM (African Peer Review Mechanism)* ambao ulianzishwa mwaka 2003 na Kamati ya Wakuu wa Nchi za Kiafrika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tendega.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza swali langu halijajibiwa. Naomba niulize maswali maeili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mikataba mbalimbali ambayo tunaridhia katika nchi yetu, nini kilitokea mpaka tukajitoka katika OGP?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kama alivyosema kwamba kuna vyombo mbalimbali ambavyo tunavitumia kama alivyoainisha. Sasa ni nini kinatufanya tusiridhie katika mikataba hiyo wakati sisi nchi yetu si kisiwa?

NAIBU SPIKA: Sasa Mheshimiwa Tendega, mikataba mingine inakuwa lazima ina ushoga, utakubali nchi iwe na ushoga? Mheshimiwa Naibu Waziri.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Tendega kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, kwamba kwanini tulijitoa; tulikuwa tayari tupo na Mkataba wa Umoja wa Mataifa yaani *UPRM, (Universal Periodical Review Mechanism)* ambayo inafanyiwa review kila baada ya miaka minne, ambayo ni ya umoja wa mataifa. Wakati huo huo tulikuwa kwenye *OGP* ambayo ni *CSO private sector*. Kwa kwa hiyo kukawa hakuna sababu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri una muda wa kujibu maswali si kama unaanza kutoa mada.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo namjibu.

NAIBU SPIKA: Jibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tayari nchi yetu ipo katika mikataba ya Umoja wa Mataifa kama vile *UPRM*. Nikienda kwenye swali lake la pili, *why* tusiridhie. Kama nilivyojibu kwenye swali la kwanza lakini kwenye majibu yangu ya msingi, tayari tuna mechanism zetu za ndani ya nchi, kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, tuna taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

8 NOVEMBA, 2022

Tuna *mechanism* nyingi ambazo zinaangalia uwazi na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imeweka wazi mbele taasisi zetu na mifumo yetu yote hii itafanya kazi kwa uwazi na uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa majibu. Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Simai.

Na. 91

Ucheleweshwaji wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo - Zanzibar

MHE. HASSAN SADIKI SIMAI aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza malalamiko ya muda mrefu ya ucheleweshwaji wa fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo upande wa Tanzania Zanzibar?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Hassan Sadiki Simai Mbunge wa Nungwi kama ifuatavyo: -

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua jitihada kuhakikisha kuwa fedha za Mfumo wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo zinawasilishwa kwenye majimbo ya Zanzibar kwa wakati. Mtiririko wa uwasilishwaji wa fedha hizo umekuwa wa kuridhisha. Kwa mwaka 2022/2023 shilingi bilioni 1,400,000,000 zimepelekwa Zanzibar mwezi Septemba, 2022. Aidha, fedha za mwaka 2021/2022 zilipelekwa Zanzibar mwezi Oktoba, 2021. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Simai.

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana kwa Wabunge na baadhi ya wananchi kutokana na ucheleweshwaji na matumizi mabaya ya fedha yanayofanywa na baadhi ya Halmashauri hasa kule Zanzibar: Je, Serikali haioni haja sasa kwa kushirikiana na Serikali ya Zanzibar kubadilisha utaratibu wa fedha hizi, badala ya kupitia Halmashauri sasa kupitia moja kwa moja kwenye *account* maalumu za Majimbo husika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Kumekuwa na utaratibu usiokuwa rasmi kwa baadhi ya Halmashauri hasa kule Zanzibar, ukizingatia kwamba Jimbo la Nungwi hadi hii leo bado hivi tunavyozungumza hatujapata fedha za mwaka 2021/2022. Hii ni kutokana na hali ya sintofahamu iliyotokezea pale Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A.

8 NOVEMBA, 2022

Je, Serikali inawahakikishiaje wananchi wa Jimbo la Nungwi kuhusiana na fedha hizo juu ya upatikanaji wake?
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Sadiki Simai, Mbunge wa wananchi wa Jimbo la Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili la Mfuko wa Jimbo lipo kisheria na limeelezwa kabisa katika Sheria Na. 6 ya mwaka 2012 na katika sheria hii imeeleza wazi kwamba fedha zote za Mfuko wa Jimbo zitakuwa zinapitia kwenye Halmashauri. Sasa kwa kuwa Mheshimiwa ameshauri hilo na kwa kuwa jambo hili lipo kisheria, basi atupe muda tuone namna ya kufanya kwa sababu inabidi twende kwenye sheria ili tuhakikishe kwamba fedha hizi zinakwenda kwenye mifuko ya Wabunge wenyewe. Hata hivyo tulilifanya hili, kwani ilifika wakati tukaona kwamba fedha nyingi zilikuwa zikitumika kinyume na utaratibu. Ndiyo maana Serikali iliamua sasa zipitie kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Halmashauri hiyo ama Jimbo lake kwamba mpaka leo fedha zile hazijapatikana na kwa sababu labda zilitumika kwa mambo mengine, tuseme tu kwamba lengo la Mfuko wa Jimbo ni kusaidia kuboresha miradi ya maendeleo katika Majimbo husika na hakuna lengo lingine.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunataka tutoe wito kwa Halmashauri zote, Mabaraza ya Miji yote, kwamba fedha hizi zitumike kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya jimbo na siyo vinginevyo. La kwanza, wahakikishe wanawajulisha Wabunge kwamba fedha zimeingia; la pili, wawape fedha hizi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo lake tutalifutilia na tutahakikisha kwamba fedha zake tutazipata kwa wakati. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri hili suala siyo la leo. Sasa hivi ni takribani miaka zaidi ya 10 mpaka 15 Wabunge wa Zanzibar wanalalamika, na haya yanajirudia kila mwaka, na majibu siku zote mnatoa hayo hayo. Kwa hiyo, hivi sasa lifuatilieni kweli kweli, Wabunge wapate pesa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa. Mfuko wa Jimbo unasimamiwa na Halmashauri, Mbunge ana Kamati kwenye Halmashauri ya Madiwani kupeleka maendeleo na kuchochea maendeleo kwenye Jimbo lake. Sasa toka 2021 kuna Mbunge pale hajapata pesa za jimbo. Haya.

Sasa namwita Mheshimiwa Usonge.

MHE. JUMA USONGE HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Changamoto ya Mfuko wa Jimbo kwa upande wa Zanzibar kila siku kila tukija hapa kwenye kikao suala hili linaibuka. Mpaka muda huu nazungumza, mimi Jimbo langu la Chaani sijapokea kwa ukamilifu fedha hizi za Mfuko wa Jimbo. Tumekuwa tukilalamika kila session ya Bunge, bado Serikali hatujaona kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kutatua changamoto

8 NOVEMBA, 2022

hizi ambazo tena tunakubaliana nazo sisi Wabunge kupitia upande wa Zanzibar. Nakushukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Usonge, Mbunge wa Jimbo la Mkwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiri kwamba bado kuna changamoto kwenye Mfuko wa Jimbo pamoja na kuboreshwa kwa hizi sheria. Changamoto kubwa tuseme ipo kwenye Mabaraza ya Miji na kwenye Halmashauri. Tulichokipanga baada ya Bunge hili, twende tukakae na viongozi wote wa Mabaraza ya Miji na Wakurugenzi wa Halmashauri wote Zanzibar ili tuwaeleze umuhimu wa fedha hizi kufika kwa wakati kwa Waheshimiwa Wabunge ili waweze kutekeleza miradi yao.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tumeshakuelewa. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Hasunga.

Na. 92

**Hitaji la Soko la Mazao la Kimataifa Eneo la Mbimba
TACRI**

MHE. JAPHET N. HASUNGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga soko la mazao la Kimataifa katika eneo la *Mbimba TACRI* Vwawa ili Wananchi wapate soko la uhakika?

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa kilimo na ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi imetenga ekari 25 kwa ajili ya ujenzi wa soko ambapo eneo hilo limeshafanyiwa upembuzi yakinifu kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). Aidha, gharama za ujenzi wa soko hilo ni takribani shilingi 14,117,640,924.91. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hasunga.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Serikali. Ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka huu Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza fedha hadi kufikia takribani shilingi bilioni 954; ni kwa nini Serikali haikuweka kipaumbele cha ujenzi wa soko hili katika hizo fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Songwe ni moja ya mikoa ya kimkakati, ambayo inapakana na nchi mbalimbali jirani na ambao unaongoza katika uzalishaji wa chakula, ni mkoa wa tatu kwa uzalishaji wa chakula.

8 NOVEMBA, 2022

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko hili muhimu kwa wananchi wa mkoa huo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunampongeza Mbunge kwa kazi kubwa aliyoifanya kuhakikisha kwamba eneo lile linapatikana kutokea TACRI. Pili, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua umuhimu wa Mkoa wa Songwe katika kilimo cha nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili tutalipa kipaumbele katika bajeti inayokuja ili basi wananchi wa Mkoa wa Songwe na hasa wakulima wa mazao mbalimbali waweze kupata fursa hii ya kuwa na kituo cha mazao; na kwa sababu pia Songwe inaungana na nchi nyingine, itakuwa ni fursa ya kipekee kwa wananchi wetu kupata masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalipa kipaumbele na ataona katika bajeti inayokuja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakoso.

8 NOVEMBA, 2022

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Serikali iliahidi kujenga Soko la Kimataifa katika Kijiji cha Itetemya, Kata ya Karema ambacho kingewasaidia kuunganisha kati ya nchi ya DRC Congo na wananchi hao: Je, ni lini huu mradi ambao iliahidi takribani miaka mitano iliyopita utatekelezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mbunge, kama ifuatanyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilishatoa ahadi juu ya ujenzi wa soko katika eneo hilo. Nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa kati ya maeneo ambayo tunayapa kipaumbele ni ujenzi huu wa masoko. Nimwondoe hofu kwamba katika mikakati yetu inayokuja tutaunganisha masuala ya miundombinu ya masoko tunayoyafanya na ujenzi wa masoko hayo, pamoja na kumkumbuka katika eneo lake. Hivyo Mheshimiwa Mbunge atupe nafasi katika bajeti inayokuja pia tutaikumbuka katika eneo lake hilo.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Oliver.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kuna Soko la Kimataifa lililoanza kujengwa katika Kitongoji cha Nzaza Kata ya Kabanga Wilayani Ngara 2014 na ujenzi huo ukasimama ghafla: Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi huo wa soko hilo kwa

8 NOVEMBA, 2022

manufaa makubwa ya wananchi wa Ngara na wakulima kwa ujumla? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mbunge Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, soko lilopo pale Kabanga katika Wilaya ya Ngara ni kati ya masoko sita ambayo Wizara imepanga kuyamalizia katika mwaka huu wa fedha. Hivyo soko hili lipo katika mpango na litatekelezwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Maganga.

Na. 93

Kuanzisha Skimu ya Umwagiliaji ya Mbongwe

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Skimu za Umwagiliaji katika Jimbo la Mbogwe?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na zoezi la utambuzi na uhakiki wa maeneo zaidi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe. Hadi sasa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na wananchi wa Mbogwe wameweza kuibua Skimu ya Mugelele yenye eneo la ukubwa wa hekta 300. Aidha, baada ya zoezi hilo kukamilika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itatenga fedha katika bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa ajili ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maganga.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili. Kwa kuwa mwaka 2021 tulipitisha bajeti kubwa na tukasema kwamba sasa mbegu zitatolewa na ruzuku, lakini mpaka sasa hivi mbogwe hatujaona kitu chochote. Majibu yake yakoje?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; nina imani hujawahi kufika katika Wilaya ile: Je, uko tayari kuongozana nami baada ya Bunge ili ukaangalie maeneo ya Mbogwe, maana ni maeneo yanayofaa sana kwa kilimo? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, swali la kwanza sijalisikia vizuri.

NAIBU SPIKA: Swali la kwanza rudia.

8 NOVEMBA, 2022

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Swali la kwanza nimesema hivi, tulipitisha bajeti mwaka 2021, Mheshimiwa Rais ametoa ruzuku kwa wakulima wa pamba pamoja na alizeti, lakini mpaka sasa hivi wakulima wale wanalalamika hawajapata ruzuku kwenye pamba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ruzuku la mazao hasa ya kimkakati yanaendelea kuratibiwa na bodi husika. Natoa maelekezo kwa bodi husika kuhakikisha kwamba wakulima wa pamba katika mikoa ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge waweze pia kufikiwa na ruzuku hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu mimi kwenda Mbogwe, baada ya kikao hiki cha Bunge, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kuangalia suala la kilimo katika eneo lake la Mbogwe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Chaya.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Serikali iliahidi kufanya ukarabati wa Skimu za Chikuyu na Udimaa: Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi hii? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu za Chikuyu na Udimaa ni skimu ambazo kama Naibu Waziri nimeshakwenda kuzitembelea, nimeziona na tumebaini changamoto yake. Ninavyozungumza hivi sasa, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Umwagiliaji na timu yake wanaelekea katika maeneo hayo kwa ajili ya kukamilisha kazi ya kupitia upya michoro na kuanza utekelezaji wa miradi ambayo itawafanya wananchi waendeleo na kilimo cha umwagiliaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asia nimeona umesimama.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza; je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Skimu ya Kata ya Endagaw ilhali tayari ilishatoa zaidi ya shilingi milioni 800 na bado haijaanza kufanya kazi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalumu, Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ipo katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka huu, zoezi la utekelezaji linaendelea.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Ngassa, Mbunge wa Igunga.

Na. 94

Skimu ya Umwagiliaji ya Igurubi

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Skimu ya Umwagiliaji ya Igurubi katika Jimbo la Igunga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nicholas George Ngassa Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya umwagiliaji imepanga kufanya mapitio, upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji katika Skimu ya Igurubi. Aidha, mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu na gharama ya ujenzi kujulikana, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itatenga fedha katika bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ngassa.

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naishukuru Serikali. Pale

8 NOVEMBA, 2022

Igunga tuna skimu nyingine inaitwa Mwanzugi Mwamapuli walitupatia fedha; na kwa majibu haya ya Mheshimiwa Naibu Waziri, basi nimeridhika tunasubiri kwa ajili ya usanifu. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Dkt. Florence.

MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa skimu zilizojengwa katika Jimbo la Mhambwe, ikiwemo Nyendara, Lumpungu, Kigina, Mgondogondo, Kahambwe, lili ziweze kuwasaidia wakulima wa jimbo hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika moja ya mikakati tuliyonayo katika mwaka huu wa fedha ni kuhakikisha tunakarabati na kukamilisha skimu ambazo tulizipitia na kuona zinahitaji marekebisho madogo ili wananchi waendeleo kutumia kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika baadhi ya skimu katika Jimbo lake zitatekelezwa mwaka huu na nyingine katika mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu. Mheshimiwa Kuchauka.

8 NOVEMBA, 2022

Na. 95

Maandalizi ya vyuo kupokea wanafunzi wa sayansi

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA aliuliza:-

Je, ni kwa kiasi gani Vyuo vya Serikali vimejiandaa kupokea wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-_

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatanyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mradi wa *Higher Education for Economic Transformation (HEET)* inatarajia kuongeza fursa za wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu kwa kujenga na kukaratabati miundombinu kama ifuatavyo: ujenzi wa maabara na karakana za kufundishia 108; vyumba vya mihadhara na madarasa 130; kumbi za mikutano ya kisayansi 23; mabweni 34; miundombinu ya shambani na vituo atamizi 10 kwa ajili ya kuendeleza ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho hayo yanatarajiwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma programu za Sayansi kutoka wanafunzi 40,000 kwa

8 NOVEMBA, 2022

mwaka 2020 hadi kufikia 106,000 mwaka 2026. Aidha, mradi huu pamoja na kuboresha mitaala zaidi ya 290 pia utasomesha wahadhiri 831 katika programu za kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, kwa mwaka wa masomo 2022/2023, Serikali kupitia *Samia Scholarship* imetoa ufadhili wa asilimia 100 kwa wanafunzi 640 wenye ufaulu wa juu waliodahiliwa katika Vyuu Vikuu kusoma Programu za Sayansi, Teknolojia, Hisabati na Tiba.

Mheshimiwa Saibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri yanayotia moyo. Hata hivyo majibu haya hajatoka takwimu; yaani hizi takwimu hazijaja na *percent* ili tuone ukubwa wa tatizo sisi kama wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi hapa nina takwimu ya chuo kimoja tu hiki cha *MUHAS* hapo Muhimbili. Mwaka 2022/2023 udahili, wanafunzi walioomba pale walikuwa 27,540; waliokidhi vigezo 19,287, lakini chuo kile kina uwezo wa kudahili wanafunzi 866 tu, ambayo ni 4% tu ya mahitaji: Je, hatuoni kwa *trend* hii kwamba tunakatisha tamaa vijana wetu kuendelea kusoma masomo ya Sayansi? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyowaelezakwenye majibu yangu ya msingi, tumeona ukubwa wa tatizo, ndiyo maana Serikali imeingia mkataba wa kuchukua mkopo huu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari fedha hizi tumeshazipata na zinakwenda kutanua sasa wigo wa vijana wetu kuingia katika Masomo ya Sayansi. Amezungumzia suala la Muhimbili ambayo sana sana ni masomo ya tiba, lakini hapa tunazungumzia sayansi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa takwimu zilizopo mwaka 2020 waliofanya mtihani wa kidato cha sita walikuwa ni 84,212; mwaka 2021 waliofanya mtihani wa *form six* walikuwa ni 88,273; na mwaka 2022 waliofanya mtihani wa *form six* walikuwa ni 94,456.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi kama zaidi ya 40,000 wanakwenda kwenye masomo ya sayansi, yaani karibu asilimia 50 wanadahiliwa katika nyanja hiyo ya sayansi, bado tumesimama pazuri. Hata hivyo mradi huu unakwenda kutusogeza zaidi ya asilimia 70.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Issaay

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Hivi sasa wanafunzi wa vyuo vya afya nchini kwa ngazi ya cheti na diploma wanasoma kwa

8 NOVEMBA, 2022

ghrama kubwa. Je, ni kwa nini sasa Serikali isione namna ya kuwapunguzia wanafunzi hawa gharama katika masomo yao ya fani ya afya kwa ngazi ya cheti na diploma ili wazazi waweze kumudu gharama zilizobaki?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issaay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tukiri kwamba ni kweli kwamba upande wa elimu ya tiba ada zimekuwa ni kubwa, lakini wakati tunatoa bajeti yetu hapa, wenzetu au benki yetu ya *NMB* ilitoa ufadhili wa zaidi ya shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kada hizi za kati. Kwa hiyo, eneo la kwanza naomba wazazi na walezi wa wanafunzi hawa waweze kuifikia benki hii ili waweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tuko katika mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba tunafikia kada hii ya kati pindi tutakapoongeza bajeti kwa ajili ya wanafunzi hawa kupata mikopo vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amandus.

MHE. AMANDUS J. CHINGUILE Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika Jimbo langu la Nachingwea kuna Chuo cha Ualimu lakini hakitoi kozi ya sayansi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kozi ya sayansi katika chuo hiki cha Nachingwea?

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna Chuo cha Ualimu pale Nachingwea kwa vile Mheshimiwa Mbunge ametoa ushauri, naomba tuuchukue ushauri huu twende tukaufanyie tathmini ili tuweze kuangalia kama kuna uhitaji wa kuanzisha kozi hiyo ya sayansi katika chuo hicho.

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa majibu mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Dkt. Paulina.

Na. 96

**Malipo ya Malimbikizo ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu
Nchini**

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa Wahadhiri wote nchini malimbikizo yao ya miaka ya nyuma?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu: -

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali hulipa malimbikizo ya watumishi wote wa Serikali wakiwemo Wahadhiri baada ya kujaza fomu za malimbikizo (*arrears clearance forms*). Mara baada ya mtumishi kukamilisha kujaza fomu hizo na kuwasilishwa, madai yao hupelekwa Ofisi ya Rais, Management ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na baadaye Hazina kwa ajili ya malipo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Septemba, 2022, Serikali imelipa jumla ya Sh.1,172,429,710 kwa ajili ya malimbikizo ya Wahadhiri. Serikali itaendelea kulipa malimbikizo ya Wahadhiri kulingana na bajeti ya fedha kwa mwezi na mwaka husika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Paulina.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuhakikisha malimbikizo hayaendelei tena kutokea katika kipindi kijacho?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali ipo tayari kulipa riba katika malimbikizo ya malipo yaliyochelewa kulipwa kwa Wahadhiri kama inavyofanya kwa wakandarasi wanaochelewa kulipwa malipo yao? (*Makofi*)

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu ya msingi, kwamba Serikali hulipa malimbikizo pamoja na stahiki nyingine za watumishi kulingana na bajeti. Kwa hiyo, mkakati wetu kama Serikali jambo la kwanza ni kuhakikisha kwamba tunaweka bajeti stahiki na toshelezi ili malimbikizo kwanza yasitokee na pili watumishi wanapokuwa na madai yao yaweze kulipwa kwa wakati. Huo ndiyo mkakati wetu kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la pili la riba, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba malipo haya hulipwa kwa mujibu wa kanuni, sheria taratibu na miongozo na kwa kanuni tulizonazo hivi sasa, hazina eneo ambalo linaonesha kwamba malipo yatakapochelewa yalipwe na riba. Kwa hiyo, halipo na badala yake tunasimamia utaratibu wa kawaida ambao ni bila riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi.

8 NOVEMBA, 2022

Na. 97

Kuwapatia Wakausha Dagua Vifaa vya Kisasa

MHE. MARYAM AZAN MWINYI aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuwapatia vifaa vya kisasa wananchi wanaofanya shughuli za kukausha dagaa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) inatarajia kujenga vichanja 80 vya kukaushia dagaa (*drying racks*), kununua mitambo minne ya umeme ya kukaushia dagaa (*electric drier*) na *Solar Tents* 15 katika Halmashauri za Kilwa, Mafia, Pangani na Bagamoyo katika mwaka wa fedha 2023/2024. Pia Wizara itaendelea kuwahamasisha na kuwaunganisha Wajasiriamali wa Sekta ya Uvuvi ili waweze kupata mikopo nafuu kupitia TADB itakayowawezesha kununua zana bora na za kisasa za kuendesha uvuvi endelevu, biashara yenye tija ya mazao ya uvuvi na matumizi ya vifaa vya kisasa vya kukaushia dagaa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maryam.

8 NOVEMBA, 2022

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wanawake wengi ndiyo wanajishughulisha na ukaushaji wa dagaa, je, Serikali ina mpango gani maalum wa kuwasaidia kwa haraka wanawake hawa ili kupata tija zaidi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango maalum tulionao, la kwanza Serikali imejikita katika kulitangaza zao la dagaa kuwa ni zao la kimkakati na lengo na dhamira ya Serikali ni kulipa thamani zao hili kulifungulia masoko na kuweza kuwahakikisha hata mabenki yaweze kuwa na utayari wa kuwakopesha akinamama wanaojishughulisha na shughuli hizi za ukaushaji wa dakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kufungua masoko ya duniani na hivi tunavyozungumza zao la dagaa limekuwa na thamani kubwa sana katika soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo pia kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kuwawezesha kupata mikopo kupitia Benki yetu ya kilimo na kuhimiza halmashauri zetu kupitia ile asilimia nne ya akinamama, kuwasaidia na kuwakopesha zaidi akinamama wazalishaji

8 NOVEMBA, 2022

hasa kundi hili la wavuvi linalokausha dagaa na kufanya biashara hii ya dagaa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mama Kikwete, jiandae Mheshimiwa Zodo na Mheshimiwa Dkt. Kaijage.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa dagaa ni shughuli ambayo wanawake wanajishughulisha nayo sana na shughuli hii inaendana sambamba na suala zima la mwani. Je, Serikali ina mpango gani kuhusiana na suala la mwani kuwasaidia wanamwani hawa kutupatia vifaa? Sambamba na vifaa kutupatia au kututafutia soko la mwani kwa ajili ya ustawi wa wanawake?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wetu katika mwani, kwenye bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha 2022/2023, tumetenga takribani Shilingi Bilioni 3.4 kwa ajili ya kununua vifaa kwa maana ya kamba, taitai na mbegu kwa ajili ya kuzitawanya katika vikundi vya akinamama mwambao wote wa pwani kuanzia Mkinga mpaka kule Mwa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile mkakati wetu ni kujenga maghala, nia ni madhumuni ni kuongeza uzalishaji. Hivi sasa tunazalisha tani 3,500 tunataka tufike tani 10,000 hadi 15,000 ili sasa tuwe na kauli katika soko.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimwia Salma Kikwete lakini na Wabunge wote kwamba, Serikali tumejipanga vema, tunalo lengo hata la kuingiza mwani katika mtindo wa stakabadhi ghalani ili tuweze ku-control bei ambayo kwa muda mrefu sana imeonekana ni yenye kuyumba. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zodo.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali katika bajeti yake ya mwaka 2021/2022 ilituahidi vichanja kwa wavuvi wa dagaa; na kwa kuwa hata kwenye bajeti yake ya 2022/2023, bado ametuahidi vichanja na Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna vichanja 80 watapeleka. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka vichanja hivyo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kabisa mwaka huu niliousema wa fedha wa 2023/2024, baada ya kuwa tumekamilisha taratibu zote za kitaalam, ambazo ndiyo zilizokuwa zikitukwamisha tutakwenda kutekeleza ahadi hii ya Serikali kwa hakika kabisa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kaijage.

8 NOVEMBA, 2022

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami naipongeza Serikali kwa kuja na mradi mzuri huu wa kuinua wavuvi na kwa kuwa Wilaya za Mkuranga na Kibiti ni wilaya ambazo zinajihusisha na uvuvi sana na kundi kubwa la wanawake wanafanya shughuli hii. Je, ni lini mradi huu wa kuinua wavuvi utawafiki wananchi wa wilaya hizi mbili? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mkuranga na Kibiti ni miongoni mwa wilaya zitakazofaidika na program hii, lakini vilevile zitafaidika na program kubwa inayokwenda kwa jina la Tanzania *Scaling up Blue Economy* ambapo tutajenga maghala ya kuhifadhia samaki, masoko vikiwemo na hivi vichanja. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Alice na Wabunge wengine wa Mkoa wa Pwani, Tanga, Lindi na Mtwara pamoja na wengine wote kwamba tumejipanga vema na hili tunakwenda kutekeleza.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Monni.

8 NOVEMBA, 2022

Na. 98

Ahadi ya ujenzi wa Bwawa Mji wa Itolwa – Chemba

MHE. MOHAMED L. MONNI aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya ujenzi wa Bwawa katika Mji wa Itolwa, Kata ya Jangalo itatekelezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikamilisha utafiti wa ujenzi wa bwawa la mita za ujazo 106,100 katika Kijiji cha Itolwa Wilayani Chemba. Gharama za ujenzi wa bwawa hilo ni shilingi bilioni 1.7 na katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bwawa hilo. Maji yatakayohifadhiwa katika Bwawa la Itolwa yatatosheleza mahitaji ya wakazi wa Kijiji cha Itolwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Monni.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante./ Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuishukuru sana Wizara ya Maji wamefanya kazi kubwa, lakini nina swali moja la nyongeza. Kijiji cha Ombiri kilikuwa na bwawa la asili ambalo sababu ya mvua kubwa kingo

8 NOVEMBA, 2022

zake zimekatika. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wanarudisha bwawa lile kwa ajili ya watu wa kijiji kile? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunafahamu bwawa la Ombiri katika Kijiji cha Ombiri, limepata matatizo, sisi kama Wizara kwa umuhimu wa bwawa namna ambavyo tunaendelea kuyajenga, kwa hiyo, bwawa hili ambalo limepata hitalafu sisi kama Wizara tumelipa kipaumbele, tutakuja kulitekeleza kwa kulikarabati vizuri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mradi wa Maji wa Nyantukuza, Jimbo la Nyangh'wale umeenda kukamilika na kwa sababu kuna ukame mkubwa wa maji, je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza maji kutoka chanzo hicho kwenye kata zifuatazo: Nyidundu, Nyalubele, Shabaka, Kaboha na Mwingilo, je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza maji hayo kwa haraka ili kupunguza adha hii ya ukame wa maji? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Nyangh'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mradi ule ni mradi ambao tunatarajia uondoe matatizo ya maji katika kata hizo hizo ulizozitaja. Naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo sasa Wizara tunapambana kuona tunakabili na hili tatizo la ukame, tutafika na kuona uwezekano wa kuweza kusambaza maji katika kata alizozitaja Mbunge. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tundaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, Mheshimiwa Sima.

Na. 99

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Singida Mjini

MHE. MUSSA R. SIMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Kiwanja cha Ndege Singida Mjini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Singida kilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ufadhili wa Benki ya Dunia mwaka 2017 kupitia mradi wa *Transport Sector Support Project (TSSP)* kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa Kiwanja hiki cha Ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo vya Ndani na Washirika wa Maendeleo ili kuanza ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Singida.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sima.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali lakini tangu 2017 mpaka sasa ni miaka mitano hakuna kinachoendelea. Swali la kwanza, nataka *commitment* ya Serikali lini ujenzi wa uwanja huo ama ukarabati utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nataka kujua mkakati wa Serikali ambao utahakikisha ujenzi huu unafanyika kwa wakati? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu la msingi, ujenzi huu utaanza pale ambapo Serikali

8 NOVEMBA, 2022

itakuwa imepata fedha na kuupangia uwanja huu kuanza ujenzi. Kwa hiyo, *commitment* ya Serikali ni kwamba tayari tumeshaanza hatua za awali kwa maana ya kufanya usanifu na kama nilivyoieleza kwenye jibu la msingi, tunaendelea kutafuta fedha pamoja na Washirika wa Maendeleo ili fedha ikipatikana tuanze kuujenga huu uwanja wa Singida.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sillo.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Manyara ambao eneo lilishatengwa eneo la Mwada?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sillo, Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu zinaendelea za kutwaa eneo ambalo uwanja huu utajengwa na baada ya taratibu hizo kukamilika uwanja huu utanza kujengwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mbunge wa Chwaka.

8 NOVEMBA, 2022

Na. 100

Wafanyabiashara wanaoweka bustani kando ya barabara

MHE. HAJI MAKAME MLENGE aliuliza:-

Je, ni kwa nini wafanyabiashara wanaoweka bustani kando ya barabara hulipishwa fedha nyingi na *TANROADS* na *TARURA*?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haji.

MHE. HAJI MAKAME MLENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali hata hivyo na maswali mawili ya nyongeza.

Je, Wizara yako inayo mpango wowote wa kutengeneza bustani kando kando ya barabara hasa maeneo ya Mjini?

Swali la Pili, kwa kuwa mazingira ni muhimu. Je, Wizara yako inashirikiana vipi na Wizara ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira katika kuratibu mazingira,

8 NOVEMBA, 2022

hasa bustani katika maeneo ya pembeni ya barabara?
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Makame Mlenge Haji, Mbungwe wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria na Kanuni zimetoa maelekezo kwa watu wote ambao wanataka kutumia hifadhi ya barabara bila kuathiri matumizi wafike kwenye mamlaka husika ili waweze kuendeleza na kupendzesha Miji. Suala hili linafanyika kwa barabara za *TANROADS*, vilevile barabara za *TARURA* kwa maana ya *TAMISEMI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusu kushirikiana na hifadhi ya mazingira ni kwamba taratibu na sheria inayoongoza iko chini ya Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, tunahakikisha kwamba tukishampa mtu kazi, kwa maana ya kumpa kibali, basi anafanya kazi kulingana na miongozo na taratibu ambazo zimewekwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ambayo inalinda kutumia hifadhi ya barabara. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chaurembo niliona umesimama au umeghairi? Tunaendelea Waheshimiwa, Wizara ya Afya, Mheshimiwa Shekilindi.

8 NOVEMBA, 2022

Na. 101

Kuboresha Huduma za Afya kwa Wazee

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma za afya kwa Wazee badala ya kutumia Dirisha la Wazee ambalo linawatesa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimuwa Shekilindi, MBunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuimarisha huduma za afya kwa wazee. Kwa miaka mingi wazee wamekuwa wakipatiwa huduma mahsusi kwa kupitia madirisha maalum ya huduma za afya kwa wazee yaliyotengwa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika kuimarisha huduma za afya kwa wazee, Wizara katika Mwaka huu wa fedha 2022/2023 imepitishiwa muundo mpya ambao umewezesha Wizara kuanzisha seksheni ndani ya Kurugenzi ya Tiba inayoshughulika na Huduma za Afya ya Wazee, Huduma za Utengamao na Huduma za Tiba Shufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Seksheni hii mpya, Utaratibu wa huduma mbalimbali za afya ya wazee utafanyika na maboresho ya huduma za afya kwa wazee yatapokelewa na kuchakatwa na kupatiwa

8 NOVEMBA, 2022

majawabu kwa wakati. Rasimu ya mwongozo wa utekelezaji wa mkakati wa huduma za afya kwa wazee ipo katika ngazi ya maboresho hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzee na kuzeeka havikwepeki, Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuwaenzi wazee wetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shekilindi.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pia nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, mfumo huu wa kutumia dirisha la wazee unaonyesha una mapungufu makubwa. Je, Serikali haioni kuwa ipo haja sasa kubadilisha mfumo huu na ikiwezekana wazee wapewe kadi kabisa za bima ya afya, kuliko kupewa vitambulisho kama ilivyokuwa sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wazee wengi wanaoishi vijijini hawajui kabisa kwamba kuna dirisha lile la afya, kutumia huduma za afya; je, Serikali ina mpango gani wa kuwafikia wazee hawa ili nao waweze kupata huduma hii muhimu kwao kama wazee wenzao wanaoishi mijini? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, samahani swali la pili sikulisikia vizuri.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Swali la pili mtaalam wa madawa asili?
(Kicheko)

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wazee wengi wanaoishi vijijini hawajui kabisa kwamba kuna dirisha hili la afya. Je, Serikali ina mpango gani kuwafikia wazee hawa ili nao waweze kupata huduma hii? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi kwa maswali yake mawili ya nyongeza hususani katika kuhakikisha kwamba wazee wetu wanapata huduma bora za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tubadilisha mfumo wa kutumia dirisha la wazee lakini tutumie mfumo wa bima ya afya kwa wote. Nitumie Bunge lako Tukufu kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge wote, Ijumaa kupitisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote, kwa sababu moja ya jambo ambalo linakwenda kutatua ni kuhakikisha kwamba wazee pia wanapata huduma za matibabu bila ya kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Wizara ya Afya tunaamini kwamba, kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote kutaboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee ikiwa ni pamoja na dawa. Kwa sababu wazee wengi sasa hivi wanakwenda kwenye dirisha la wazee, dawa hakuna, wakiwa na bima tunaamini watapata dawa.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Wazee wa Vijijini hawapati hii huduma, tumekinyanyua kile kitengo kilichokuwa kina shughulikia huduma za wazee, kimekuwa sasa ni *section*, kwa hiyo, kina Mkurugenzi Msaidizi, kazi yake kila siku ni kuangalia huduma za matibabu kwa wazee, huduma za *rehabilitation* pamoja na huduma za *palliative* za shupaa. Kwa hiyo, tunaamini kabisa pia hii itaongeza muamko katika kutatua changamoto za wazee. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Waheshimiwa tuanendelea. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Ngonyani, kwa niaba yake Mheshimiwa Manyanya.

Na. 102

Serikali kutoa ruzuku kwenye majiko madogo ya gesi

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA K.n.y MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka ruzuku kwenye majiko madogo ya gesi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha nchi inafikia zaidi ya asilimia 80 ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2032. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kufanyika kwa mjadala wa Kitaifa wa nishati safi ya kupikia, kuunda kikundi kazi kwa ajili ya uratibu, kutenga fedha katika bajeti ya 2023/2024 kwa ajili ya shughuli za nishati safi ya kupikia, kuanzisha mfuko wa nishati safi ya kupikia pamoja na kuzitaka taasisi zote zenye watu zaidi ya 300 kama vile shule, vyombo vya ulinzi na usalama, Magereza na kadhalika, kutumia nishati mbadala kupikia ikiwemo gesi na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini inatarajia kutekeleza mradi wa majaribio kwa kutoa ruzuku ya asilimia 50 ya gharama zote (jiko, gesi, mtungi pamoja na vifaa vinavyohusiana). Katika Awamu hii vifaa vipatavyo 100,000 vitasambazwa katika Mikoa 25 ya Tanzania Bara. Naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Manyanya.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza napongeze jitihada zinazoendelea kwa upande wa Serikali, lakini changamoto mojawapo inayofanya matumizi ya gesi kuwa yapo chini zaidi ni kukosekana kwa vituo vya kuuzia gesi, hasa katika maeneo ya vijijini ambayo yapo mbali na yanasabababisha kuongeza gharama kubwa kwenye mitungi pamoja na gesi kwa ujumla.

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali hiyo?

8 NOVEMBA, 2022

Jambo la pili, sambamba na gesi umezungumzia kuhusu kuwezesha nishati safi katika maeneo ya vijijini, bado maeneo ya vitongoji ambavyo ni vikubwa sana havijapata nishati safi ya umeme, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha kufikisha nishati hiyo, sambamba na hii ya gesi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Manyanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la kwanza, wakati wa utekelezaji wa huu mradi wa kutoa ruzuku, tunaamini wigo wa wafanyaji biashara kwenye eneo hili wataongeza na hivyo watafika katika maeneo yote kwa sababu Serikali itajitahidi kuhakikisha shughuli hii inapata ruzuku na hivyo wawekezaji mbalimbali wanaweza kushiriki. Pia, mwongozo tunaoutengeneza utaangalia namna ya kufanya, kama wanavofanya wenzetu wanaosambaza mbolea na maeneo kama hayo, ili tuweze kufika katika maeneo yote husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, kwenye swali la pili la umeme wa vitongoji, Serikali inaendelea katika mzunguko wa tatu awamu ya pili ya REA, viitongoji baadhi vinapatiwa umeme, lakini pia kuna miradi ya jazilizi inaendelea katika maeneo yetu na Serikali inaendelea kutafuta fedha kuhakikisha kwamba vitongoji vyote vinapatiwa umeme ili wananchi waweze kutumia nishati hiyo safi.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Reuben Kwagilwa.

Na. 103

**Ujenzi wa Kituo cha Kupozea Umeme Kwambwembwele
Vibaoni – Handeni Mjini**

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kituo kikubwa cha kupozea umeme Kwambwembwele Vibaoni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mbunge wa Handeni, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza mpango wa kuimarisha Gridi ya Taifa uliopewa jina 'Gridi Imara' kwa kujenga miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme pamoja na vituo vya kupoza na kudhibiti umeme. Mpango huu una miradi zaidi ya 40 inayotekelezwa ndani ya miaka mitano kuanzia mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2022/2023 Serikali itajenga njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 132 kutoka Mkata kwenda Kilindi kupitia eneo la Kwambwembwele Vibaoni, Handeni Mjini. Katika mwaka

8 NOVEMBA, 2022

wa fedha 2024/2025 kituo cha kupoza umeme kitajengwa na kupokea umeme kutoka katika njia ya Mkata/Kilindi itakayojengwa mwaka huu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Reuben.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni hatua zipi zimefikiwa katika ujenzi wa njia ya msongo wa Kilovoti 132 inayotokea Mkata kupita Handeni Mjini kwenda Kilindi?

Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa kukatikakatika kwa umeme na kutokuwa na umeme unaokidhi ndani ya Wilaya ya Handeni kumesababisha shughuli za uzalishaji kusimama na hasa kwenye migodi mikubwa iliyopo ndani ya Wilaya.

Je, uko tayari kuambatana na mimi baada ya Bunge hili ukaione hali halisi ya jinsi ambavyo uzalishaji umesimama kwenye viwanda vyetu? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa sasa katika utaratibu wa kujenga njia ya Mkata kwenda Kilindi kupitia

8 NOVEMBA, 2022

Kwambwembwele, Handeni Mjini ipo katika utaratibu wa zabuni. Tunatarajia mwishoni mwa mwaka huu mkandarasi wa eneo hili na maeneo mengine ambapo tutajenga vituo vya kupooza umeme na *line* za kusafirisha umeme watakuwa wamepatikana. kwa hiyo saa hivi hatua ni ya zabuni na tayari maombi yameshafanyika inaendelea *evaluation* kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili, nipo tayari kabisa kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda Handeni Mjini lakini pia na maeneo mengine yenye matatizo ya namna hii ili tujionee na tuweze kuweka msukumo katika utekelezaji wa maelekezo na ahadi za Serikali kwa wananchi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Waziri, watu wanapenda kula mihogo wekeni umeme wa uhakika ili wapike mihogo. Waheshimiwa Wabunge tuanendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mgalu. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 104

Serikali kugawa mashine za EFD kwa wafanyabiashara

MHE. SUBIRA K. MGALU aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kugawa mashine za kutolea risiti EFD kwa Wafanyabiashara ili kuongeza wigo wa walipa kodi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu: -

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa kila mfanyabiashara anapata mashine za *EFD* kwa njia rahisi na isiyo na gharama, Serikali kupitia *TRA* ilianzisha mfumo rahisi wa utoaji wa risiti ujulikanao kama *Visual Fiscal Devices (VFD)*. Mfumo huu wa kisasa wa utoaji wa risiti pasipo kuhitaji kutumia mashine kama ilivyo sasa badala yake mtumiaji anaweza kutumia vifaa vingine vya kieletroniki kama vile simu janja, kompyuta na vishikwambi kutoa risiti zilizounganishwa na mfumo wa *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo unaendelea kutumika na kusambaa nchi nzima na hauna gharama badala yake mtumiaji ataingia gharama ndogo ya bando ili kupata mtandao wakati wa matumizi. Aidha, wafanyabiashara wanaruhusiwa kisheria kujirejeshea gharama ya ununuzi wa mashine za *EFD* wakati wa uandaaji wa hesabu zao za kodi wanazopaswa kulipa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mgalu.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri na naipongeza *TRA* na wadau mbalimbali kwa ubunifu huo wa mashine ambayo inarahisisha, sasa maswali yangu mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo: -

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado yapo matukio ambayo baadhi ya wafanya biashara ya kutotoa risiti hasa katika maeneo yenye biashara mfano Kariakoo. Je, Serikali kupitia *TRA* kwa kuwa imepewa kibali kwa mara ya kwanza kaujiri watumishi wengi kwa wakati mmoja, inawatumiaje watumishi wale katika mapambano dhidi ya vitendo hivi vya kutotoa risiti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa katika jibu lake la msingi ameeleza kwamba, wafanyabiashara wanaruhusiwa kusheria kurejesha gharama za mashine za *EFD* wanazozinunua wakati wanakokotoa mapato ya kutoza kodi. Je, Serikali inajipangaje kutoa elimu hii kwa wafanyabiashara wengi ili kuondoa dhana ya kwamba mashine za *EFD* ni gharama zaidi? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kabla ya kujibu maswali haya, kwa idhini yako, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofuatilia na pia ni Balozi wa *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, Serikali iliwapatia mafunzo yale ambayo ni muhimu kabisa, awali kabla ya kuanza kufanya kazi, lakini kama hilo halitoshi, Serikali imeandaa Mkakati wa kutoa

8 NOVEMBA, 2022

mafunzo ya watumishi hawa, mafunzo maalum kwa watumishi hawa wapya kila baada ya miezi minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Serikali kupitia *TRA* ina program ya kutoa elimu kupitia vyombo vya habari, tv pamoja na redio. Nichukue fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, kuwaelekeza *TRA* kuendelea kutoa mafunzo hayo kimkakati. Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kuna kipindi kumekuwa kukitokea tatizo la upatikanaji mfumo hasa kwa watu wanaohitaji zile mashine za *EFD*, hivyo kuchelesha kupata zile mashine za *EFD* nini mkakati wa Serikali wa kuimarisha mfumo ili wafanyabiashara waweze kupata hizi mashine za *EFD* kwa wakati? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizo zilikuwepo za mfumo huo wa mashine ya *EFD* na ndiyo maana tukaamua sasa kuleta mfumo mpya na kifaa kipya ambacho kinajulikana kwa *VFD*. Ahsante. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Kaiza, kwa niaba

Na. 105

Hitaji la Magari Mapya ya Jeshi la Polisi

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA K.n.y. MHE. AGNESTA L. KAIZA aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kulipatia Jeshi la Polisi magari mapya kama moja ya vitendea kazi ili litekeleze majukumu yake ipasavyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kulipatia Jeshi la Polisi magari kama nyenzo ya kutendea kazi. Mkakati wa Serikali ni kutenga fedha kwenye Bajeti yake kila mwaka ili kununulia vitendea kazi muhimu yakiwemo magari na pikipiki. Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Jeshi la Polisi limetengewa kiasi cha Shilingi Bilioni 15 kwa ajili ya ununuzi wa magari 101 na pikipiki 336. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa.

8 NOVEMBA, 2022

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, naomba nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora ni moja kati ya mikoa mikubwa na yenye watu wengi lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana ya usafiri kwa askari wetu katika vituo mbalimbali. Serikali inampango gani wa kupeleka magari ili kuweza kurahisisha kazi za askari wetu wanapokutana na matukio?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Jimbo la Tabora mjini lina kituo cha *Central Police*, lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana, na nimekuwa nikiliuliza sana swali hili la usafiri, hata gari lililopo ni tia maji tia maji. Serikali ina mpango gani basi angalau katika bajeti hii kupeleka magari machache katika Mkoa wa Tabora, hususani Jimbo la Tabora Mjini ili kurahisisha kazi za askari wetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba kweli Mkoa wa Tabora ni mkubwa na uhitaji wake wa magari hauhitaji kupingwa, iko wazi. Kwa kulitambua hilo, Mkoa wa Tabora umepata mgao wa magari. Katika magari 78 tuliyoyapokea mwezi uliopita Tabora wamepata magari mawili. Moja limepelekwa kwa *RPC* Tabora na jingine limekwenda *FFU* Tabora. Kuhusu manispaa ya Tabora Mjini niahidi, kadri tutakapokuwa tunapata fedha, kama

8 NOVEMBA, 2022

ambavyo mwaka huu tumetengewa Shilingi bilioni 15. Fedha zitakazopatikana tutanunua magari na Tabora kwa uhitaji wake pia watafikiriwa kupewa gari. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cherehani.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwenye Bunge la Bajeti lililopita Mheshimiwa Naibu Waziri aliniahidi kupeleka fedha kwenye ujenzi wa Kituo cha Polisi kilichopo katika Halmashauri ya Ushetu; na wananchi wale walishajichanga pamoja na wadau mbalimbali wakajenga msingi. Sasa nataka nijue, ni lini Serikali inapeleka fedha hizi ili kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Halmashauri ya Ushetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cherehani kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu maeneo ya Wilaya mpya kama ilivyo ya Ushetu wanahitaji kuwa na vituo vya polisi ili kusogeza huduma za usalama wa raia karibu zaidi na wananchi. Ni ahadi yetu kwamba kwa vyovyote vile kwa sababu wananchi wameshajitokeza, wamechangia nguvu zao na jitihada wakafikia mpaka kiwango cha msingi, nimtie moyo Mheshimiwa Mbunge, kwamba pale ambapo tutapata fedha kwa ajili ya ujenzi, Wilaya ya Ushetu itazingatiwa pia. Nashukuru.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu unakwenda, tunaendelea na swali letu sasa la mwisho, Mheshimiwa Haji Amour Haji.

Na. 106

Uhitaji wa Sera na Sheria ya Makampuni ya Ulinzi Binafsi

MHE. HAJI AMOUR HAJI aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutunga Sera na Sheria ya Kampuni Binafsi za Ulinzi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mbunge wa Pangawe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa Sheria na Sera inayosimamia kampuni binafsi za ulinzi. Kwa sasa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kutunga Sheria ya Huduma za sekta binafsi za ulinzi umekamilika na utawasilishwa katika Baraza la Mawaziri kwa ajili ya maamuzi baada ya kupata maoni ya kina ya wadau wa pande zote mbili za Muungano juu ya Rasimu ya Sheria hiyo. Baada ya kukamilika kwa hatua hizo, muswada wa sheria utawasilishwa Bungeni.

8 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa muda wa maswali umekwisha na muda wetu umekwisha, wageni wa Bunge.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika ni; *Hon. Lentheng Ntombi Mekkgwe- Speaker of the Gauteng Legislative and CPA Africa Region Treasurer, welcome to the Parliament Madam Speaker. (Makofi)*

Wengine, *Ms. Sthandiwe Ngubane-Director Inter Legislative Relations, Ms. Thembi Mabuza-Personal Assistant to the Speaker, welcome to the Parliament. (Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni saba wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya ambao ni wadau wa maendeleo kutoka Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa UKIMWI (PEPFAR) wakiongozwa na Mkurugenzi Mkazi Ndugu Jessica Green, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Fredy Mwakibete, Naibu Waziri wa Uchukuzi ambao ni Kwaya ya Usharika kutoka Kanisa la KKKT-Kisasa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Maimuna Pathan ambao ni Mheshimiwa Diwani na Katibu wa wananchi kutoka Nachingwea Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Wageni 71 wa Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka ambao ni Waheshimiwa Madiwani na Watumishi kutoka Halmashauri ya Tabora Mjini wakiongozwa na Mstahiki Meya Ramadhani Kapela, karibuni na msisahau mwenyeji wenu awapeleke kwenye chai sasa hivi. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

Wageni watatu wa Mheshimiwa Fatuma Toufiq kutoka *Sports link Academy* inayosimamia kukuza vipaji vya mpira ambao ni washirika wa timu ya *Wolverhampton Wonderers Fc* ya nchini Uingereza, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq wanafunzi na walimu wanaotekeleza mradi wa *Girl Education Champions Project* kutoka Shule za Sekondari za Wilaya ya Chemba, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani ambao ni wapigakura wake kutoka Singida Kaskazini, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Mariam Ditopile ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa na Sekretarieti ya Wilaya ya Kondo, karibuni sana. Mambo ya Kondo hayo, yameshaanza. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Mohamed Monni ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum kutoka Chemba Mkoa wa Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 33 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Mkoa wa Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Fletei Massay ambao ni Walimu kutoka Jimbo la Mbulu Vijijini Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni Viongozi wa Kata za Mlowo na

8 NOVEMBA, 2022

Nambizo CCM kutoka Mbozi Mkoa wa Songwe, karibuni.
(Makofi)

Wageni 23 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni Wanakwaya wa Kanisa la Moravian Arusha Road kutoka Jijini Dodoma, karibuni. (Makofi)

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi 30 kutoka *Dodoma Institute of Development and Entrepreneurship*, karibuni Dodoma. (Makofi)

Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO-KATIBU MEZANI: Kamati ya Mipango.

SPIKA: Kamati ya Mipango.

KAMATI YA MIPANGO

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaorodha ya wachangiaji leo. Tunaanza na Mheshimiwa Profesa Muhongo. Profesa Muhongo upo?

8 NOVEMBA, 2022

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni dakika 15, si ndiyo? Haya, kwanza kabisa kwa niaba ya...

MWENYEKITI: Ni dakika 10 Mheshimiwa Profesa.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Ooh, waliniambia ni dakika 15, wengine watanipa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe na mimi rambirambi za kutoka Musoma Vijijini kwa maafa na majonzi yaliyotupata, tunaomba wapumzike kwa amani. Vile vile katika mjadala wetu tunaoufanya sasa, nadhani tutakuwa tumejifunza na bajeti tunayoitayarisha, mambo yaliyotokea *MV Bukoba* na yaliyotokea juzi tutayaona kwenye mipango na bajeti ya mwaka ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wetu ni lazima kwanza tujue malengo yetu. Mipango tunayoifanya iko ndani ya mipango ya miaka mitano ambayo inaisha 2025, ambayo malengo yake ni ukuaji wa uchumi, upatikanaji wa ajira mpya na huduma bora kwa wananchi. Ndiyo maana kwa vyote hivi hatuwezi kukwepa pendekezo ambalo tumerudia mara kwa mara kulitoa, kwamba lazima tuwe na *Planning Commission* ambayo iko ndani ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa malengo yetu ambayo yako kwenye hiyo *document* inasema kwamba, ikifika mwaka 2025 tunataka *GDP per capita* yetu iwe dola 3000. Hiyo inamaanisha kwamba ikiwa sasahivi tuko watu takribani milioni 62, kufika 2025 huenda tutakuwa milioni 68 lakini tunaweza tukafika milioni 70. Maana yake ni kwamba ukichukua *GDP per capita* ya dola 3000 kwa

8 NOVEMBA, 2022

kila mtu kwa mwaka, tukifika 2025, tunapaswa kuwa na *GDP* isiyopungua bilioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi *GDP* yetu ni dola bilioni 62. Kwa hiyo huu mpango na bajeti yake ni lazima ituweke kwenye barabara ya kutoka bilioni 62 sasa kwenda kwenye bilioni 200; ni kazi kubwa kweli kweli. Na hapa lazima mipango yetu tuelezane ukweli, tuone kama hilo lengo la *GDP per capita* ya dola 3000 lilikuwa sahihi au tuliandika tu kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi sisi tukiwa na bilioni 62, *GDP per capita* yetu inakadiriwa mwishoni mwa mwaka kuwa dola 990. Kwa maneno mengine tumerudi chini, na hivyo tutaenda kwenye *group* la nchi masikini kufuatana na viwango vilivyowekwa na Benki ya Dunia tarehe moja Julai mwaka jana. Kwa hiyo tumeshuka, tusiongelee uchumi wa kati, hatuko huko tena, tumeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huohuo sisi tukiwa hivyo, wenzetu wa Kenya ikifika mwisho wa mwaka huu sisi tukiwa na *GDP* ya dola bilioni 62, wao watakuwa na *GDP* ya dola bilioni 107. *GDP per capita* ya Kenya, mwisho wa mwaka huu itakuwa ni dola 1,550, sisi tutakuwa ni dola 990. Kwa hiyo ukichukua yale ma-*group* yaliyotengenezwa na *World Bank*, Jirani yetu Kenya ambaye tunataka kumpatia na gesi yetu, yeye yuko kwenye *Lower Middle-Income Country* ambayo inaanzia dola 1046 mpaka dola 4095. Sisi tuko chini tuko dola 990, Kenya wapo dola 1,550. Kwa hiyo haya tunayoanza kuyajadili leo, mapendekezo yangu ni haya: -

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo yetu ni lazima tupunguze mfumuko wa bei (*low inflation*), mipango na bajeti yetu. *Inflation August* mwaka huu ilikuwa 4.6%, Septemba imepanda imekuwa 4.8%. Hii lazima tuiunguze, ndiyo tuyajadili, tushawishi Wizara ipunguze. Lengo la pili muhimu kwenye mambo tunayoyapanga na bajeti yake na inafanyika duniani kote, wanapunguza *low inflation* halafu wanapunguza na *interest rates*. Ikiwa *inflation* itapanda inamaanisha benki nazo zitapandisha riba zao za mikopo. Kwa hiyo huu mpango na bajeti yake lazima tulenge huko kwamba *interest rates* zisipande, zikipanda hata waliokopa nyumba, baiskeli na magari lazima zipande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho tunapaswa kukiongelea kwenye hii bajeti ni kuzuia *Government Bonds* (hatifungani) kutumika pasipokuwa na malengo sahihi. Maana yake ukiitumia, *inflation* ikiongezeka, utalazimika kutumia hii hatifungani. Ukishaitumia ujue sasa umeleta matatizo kwa uchumi wa nchi. Kwa hiyo hili nalo, hii bajeti ije itueleze namna ya kuzuia kukimbia kutumia *Government Bonds*, kututoa kwenye matatizo ambayo tungeweza kuyatatua kwa njia nyingine kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mipango tunayoijadili na uchumi wake, lazima ituelekeze ambapo wachumi wanatueleza. Unajua kuna wachumi wa aina mbili na inabidi uchague unapenda kumsikiliza nani. Kuna wale waliochukua *econometrics* kama akina marehemu Prof. Rweyemamu na kitabu chake cha miaka ya 1970; halafu kuna wale ambao ni *political economist*, hao maneno ni mengi na hesabu zao za kujumlisha na kutoa tu. Sasa inabidi sijui unataka kumsikiliza yupi?

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukichukua wataalamu wa uchumi kabisa wanasema duniani ukitaka kupunguza uchumi ni lazima uchumi wako ukue kwa zaidi ya 8%. Kwa hiyo hii mipango lazima itueleze, kwa sababu mwaka 2020 uchumi ulikua kwa 2%, mwaka jana kwa 4.5% na mwaka huu tunategemea kwenda kati ya 4% na 5%; na mimi takwimu zangu nazitoa kwenye vyanzo ambavyo dunia inaviamini. Unaweza kuwa na chanzo chako kama huko duniani hawakijui, sipendi kukitumia hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa China, ukisikia China kufanikiwa kiuchumi, kwa zaidi ya miaka 20 uchumi wao ulikuwa kwa kadiri ya asilimia 15 mpaka asilimia 20; kwa miaka 20 ndipo China ikafika hapo ilipo. Sasa sisi tunataka tu tufike 8% *growth*. Kwa hiyo mapendekezo yangu ni kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji ili uende kasi, ndugu zangu lazima tuwe na bidhaa nyingi na mpya kwenye soko, siyo kuongeza tozo. Tozo na kodi hazikuzi uchumi. Kinachokuza uchumi ni bidhaa kwenda kwenye soko la ndani na soko la nje. Kwa hiyo hii bajeti, mipango yetu na bajeti, tueleze hivyo, halafu lazima itueleze ajira mpya. Hili neno mpya, siyo zilezile. Ajira mpya ni zipi na kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, itueleze mzunguko mkubwa na mpana wa fedha kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, tufanye yafuatayo: mimi nina mapendekezo yangu kwa wataalamu kwamba twende kwenye kilimo, kwani kina asilimia 30 ya *GDP* yetu. Hebu tupigane tufikishe asilimia 40. Sasa sitaki kurudia, haya nilishayaongea. Mazao ambayo ni lazima tuyawekee mkazo ni yale ambayo tunatumia ndani ya nchi na nje ya nchi yana soko,

8 NOVEMBA, 2022

ambayo ni mahindi, mchele, ngano, mihogo, matunda na mbogamboga. Haya yote matumizi yake duniani kila siku ni kati ya asilimia 40 na 60 ya watu waishio duniani, twende huko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uvuvi na ufugaji. Samaki watoke ziwani, watoke baharini, tuongeze nyama na maziwa. Hapa uvuvi na ufugaji tukazane tuchangie angalau 5% ya GDP yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, madini. Tuendeleo na *Tanzanite, Gold* na *Diamond*. Pia kama nilivyowahi kuwaeleza hapa, kuna madini ambayo ni muhimu na yana thamani kubwa kuliko haya. Haya ni lazima mipango na bajeti hii itueleze inavyoiwezesha *geological survey*. Haya madini yatapatikana kwa kutumia *geological survey*, siyo Tume ya Madini. Tume ya Madini inasimamia, sasa utasimamiaje huna kitu kipa? Tuwapatie *geological survey* waendeleo kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna madini ya *electronics industry*, yanayotumika kwenye *electronics* kama *Palladium, Lithium, Copper, Tin, Nickel, Gold* na *Aluminum*. *Computer* zozote tulizonazo zina *Lithium, Cerium, Europium, Samarium, Neodymium* na madini mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ugomvi mkubwa sasa hivi unaendelea wa *microchips* kati ya Marekani na China kama mnafuatilia. Kwa sababu hizi hata simu zenu zote zina *microchips*. *Computers* zote na *electronics* zote madini yanayotakiwa humo ni *Silicon* na *rare earth element* 17, niliwahi kuyataja humu, sina haja ya kutaja.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya madini, atakayetusaia kuyapata ni *geological Survey*, wawekeze wafanye utafiti, watafute madini mapya yanayohitajika duniani, yanaitwa *technology metals*. Sasa hapa madini tujipige mpaka tufikishe asilimia 15 ya GDP; wanakaribia 10, lakini uchumi wetu uwasukume twende kwenye 15% of our GDP.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ni muhimu na ukiona katika mapendekezo yangu nimeanza ajira ya watu wengi naenda napungua kilimo, uvuvi, ufugaji, *mining* na sasa uchumi wa gesi. Yote hayo yalitushinda tukadhani uchumi wa gesi, ndiyo utatutoa, lakini tukaamua kuweka kapuni. Sijui kama tutasalimika tusipotoa huko kapuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba uchumi wa gesi una vitu vitatu muhimu; tutazalisha umeme mwingi wa bei nafuu na ujenzi wa mitambo yake ni wa haraka. Halafu umeme wa gesi hauna jua, hauna ukame, tuta-export LNG tunayotaka kuijenga pale Lindi, ni biashara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu muhimu kabisa, ni *petrochemical industrials*. Hapa kabla hatujamuuzia mtu yeyote jirani yetu tunayeshindana naye gesi, lazima tujiulize: Je, tukimpa gesi yetu, atakuja na viwanda haraka atuuzie bidhaa zinazotokana na gesi yetu? Hilo ni suala la muhimu sana. *Petrochemical industries* mfano wake ni mbolea, *plastics* zote, viti vyote mnavyokalia, vyote ni gesi; sabuni, *detergents* nyingine, *drugs*, madawa ya wadudu, rangi na *insulating materials*. Viwanda ni vingi sana vya gesi. Kwa hiyo, napendekeza hapa hii *gas economy* ituchangie kati ya 15 na 20% ya GDP. Huu mpango...

8 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Profesa, hiyo ni kengele yako ya mwisho, nakuongeza dakika tatu.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wewe Mwenyekiti ni mwema bwana. Nyingine ya tano ni *tourism*. Kufika Aprili mwaka huu 2022, *tourism* imeingiza dola bilioni 1.5. Sasa jamani, tujitahidi *tourism* tujitahidi ituletee 12% ya GDP yetu, hapo uchumi utakuwa mzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, nimeandika, *sports, games, music na culture* vitupatie GDP mbili. Mwisho ni *climate change*. Tunataka kuiona hii bajeti inaongelea hili, maana yake matatizo yamekuwa mengi. Sasa hivi *Carbon dioxide emission* za Tanzania *per Capita*; tunavyochafua mazingira kwa kila mtu kwa mwaka. Kwa mwaka 2020 ilikuwa *0.18 metrics tons a person per annum*. Mwaka 2019 ilikuwa *0.21 metric tons per person per annum*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutengeneze mpango na tuje na bajeti. Ndiyo maana kwa kumalizia ni kwamba haya yote niliyoyataja hatuwezi kuruhusu Wizara moja inayapanga yote, mengine hayapo kwao ndiyo maana tunahitaji *Planning Commission*. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Profesa Muhongo.

Waheshimiwa Wabunge, uchangiaji wa mpango ndiyo huo aliousema Profesa Muhongo. Sasa ukisimama hapa halafu unaulizia kituo cha afya ambacho hakijakamilika; Kituo cha afya kitakamilika kwa Mpango,

8 NOVEMBA, 2022

siyo kwa kuomba. Mheshimiwa Waziri wa Fedha anajitahidi sana na anaupiga kwa kuandaa mipango. Kwa hiyo, tuunge mkono na hili alilolisema Profesa tuyachukue na sisi tuyaboreshe na kuyachangia. Kama huna, wewe simama sema kama alivyosema Profesa, inatosha. Tutakwenda na wewe hivyo hivyo.

Sasa baada ya Profesa, atakuja Mheshimiwa Dkt. Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Amar na Mheshimiwa Silanga.

Kabla ya hapo, kuna tangazo. Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Wabunge wote kwamba leo kutakuwa na Semina ya Wizara ya Kilimo kuhusu mfumo wa utoaji wa mbolea ya ruzuku ya usajili wa wakulima, saa 7.00 mchana kwenye ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria.

Mheshimiwa Dkt. Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru sana kwa fursa hii. Natumaini nami utanipa dakika 15. Kwanza nianze kwa kusema kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tunaona jinsi ambavyo wanakimbizana kutafuta wawekezaji kutoka nje, na zaidi kutafuta *resources*, fedha kutoka kwenye Mataifa rafiki na kutoka kwenye mashirika ya Kimataifa ili waweze kuongezea kile tulichonacho na kuweza kusukuma na kutekeleza mipango ambayo tulikuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba wote tunaelewa kwamba lengo kuu la mipango tunayotunga hapa na bajeti ni ukuaji wa pato la Taifa ili wananchi

8 NOVEMBA, 2022

waweze kuinua maisha yao kwa kujipatia kipato cha juu na kuweza kuboresha huduma wanazopata. Kwa hiyo, ndiyo lengo kuu. Kama tukishindwa kufikia hilo, basi hatujakamilisha kazi yetu kama tunavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naamini kwamba tumefeli kidogo. Kwa sababu gani? Katika lengo la mwaka huu kubwa kwenye bajeti ya mwaka uliopita na mpango wa mwaka huu ambao tunautekeleza pia, ni kwamba tuweze kufufua uchumi wetu. Sasa kufufua uchumi wetu siyo kupata 4.8% ambayo ilijitokeza baada ya madhara ya Uviko. Kufufua uchumi wetu maana yake ni kurudisha kasi ya ongezeko la pato letu kwenye 7% au zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Muhongo amesema sawa kwamba hatuwezi; na miaka hiyo ya nyuma kabla, tulipokuwa kwenye 7%, nia ilikuwa kwamba lazima tuongeze ile kasi ifike asilimia 8, 9 hata 10 ambayo ndiyo inaweza kupelekea kusema kwamba sasa tumejiondoa kwenye umasikini na kufika katika vurugu ya nchi ambazo zipo kwenye kipato cha kati na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hatujaweza kufufua, tumebakia na asilimia 4.9; na ninashangaa kwenye huu mpango tulionao sasa hivi, tunasema kwamba hata mwaka unaokuja 2023 pato letu litakuwa kwa asilimia 5.3. Hata maoteo yanayofanyika kwenye mpango wetu huu hatujaweza kuwa *courageous* tukasema turudi kule tulipokuwa ndani ya kipindi cha miaka mingine miwili. Bado tuko chini ya 7% pengine mpaka mwaka 2025, ndiyo maoteo yaliyopo.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nafikiria kuna tatizo moja hapa, kama siyo kwenye takwimu, ni kwenye maandishi mengine. Ukweli ni kwamba haiwezekani nchi nyingine kama Botswana, Kenya na Rwanda; Rwanda imeongeza uchumi wake na kasi ya ukuaji wa pato lake ni asilimia 9.5 na Kenya ni asilimia 7.2. Sasa tunapoanza kusema kwamba aah, ni mvurugano wa *logistic industry* kwenye dunia, ni vita vya Ukraine, tusing'ang'anie huko. Tujaribu kuangalia ni kitu gani tunaweza tukafanya, tukarudisha uchumi wetu kwenye ukuaji wa 7% au zaidi ya 7%. La sivyo, hatutafika popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mkubwa ambao nashauri utumike kuweza kufufua uchumi wetu kwa haraka ni ule wa kushirikisha sekta binafsi. Inavyooneka sekta binafsi yetu haichangamkii fursa. Haioni fursa. Tunatengeneza miundombinu mizuri, kila kitu kinafanyika sawa sawa kwenye upande wa Serikali na utaona kwamba sekta zilizokuwa kwa kasi zaidi ya 8% ni zile ambazo zinapata uwekezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maji imekua kwa asilimia 11.9, huduma za jamii, ni asilimia 8.5, habari 8%, fedha na bima asilimia 10, madini na kadhalika. Ukienda hizi sekta nyingine ambazo tunashirikisha sekta binafsi, uchukuzi na uhifadhi imekua kwa asilimia 1.7 tu na ndiyo huko wenzetu tuko tunakimbizana. Ukienda kwenye kilimo 4%, pesa yote inaenda huko kwenye bajeti ya kilimo lakini ina-grow kwa 4% licha ya kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Bashe. Viwanda imekua kwa asilimia 6.3, biashara asilimia 4.4, ujenzi asilimia 5.3, upangishaji na majengo asilimia nne na nukta. Sasa hizo ndiyo sekta hasa za wajasiriamali, lakini hazikui. Hawajaweza kuchangamkia fursa.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri njia ya kuweza kulazimisha watu wajiingize kwenye uchumi huu pengine, badala ya kutupa fedha za kupeleka kwenye barabara za *TARURA* kwa sababu tumeshapeleka kiasi kidogo na barabara zimeanza kuwa nzuri, tupe hiyo Shilingi milioni 500 kila Mbunge achangamkie mradi wake kwenye jimbo lake, aajiri watu, ahakikishe wajasiriamali 500 mpaka 1,000 wanaingia kwenye mradi huo, waanze kuzalisha, na hiyo iwe ni mbegu itakayozalishwa mwaka hadi mwaka. Pia tutakuwa tunashirikisha wajasiriamali wetu kwa nguvu zaidi kuliko kusubiri ile mikopo ya 4,4,2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini tukiweza kufanya vile itatusaidia. Lazima ile miradi inayoletwa ionekane kwamba itatekelezeka na Wabunge wasimamie na wajitolee katika kusimamia kweli.

Mhshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana, sekta hii haiwezi kupata fedha kutoka kwenye vyombo vya fedha. Kwa nini? Kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Muhongo, riba ziko asilimia 16. Bbado asilimia 16, haijapungua! Toka mimi niingie huku Bungeni miaka ya nyuma riba ni asilimia 16. Sasa hii *issue* ni kwamba mtu mwingine anaogopa kuchukua mkopo wa riba asilimia 16. Watu wengi wanaogopa kwa sababu hakuna faida ya haraka namna hiyo, lakini tukitumia huu mpango wa sasa hivi wa *fiscal stimulus*, tuache hii *monthly stimulus* ambayo imeshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *monthly stimulus* imeshindwa kwa sababu ukweli ni kwamba *inflation* iliyopo na kadhalika, siyo *a man management type* ni *supply oriented*. Kwa hiyo, ni lazima tutumie mbinu nyingine ya kufanya *fiscal stimulus*; tutapeleka fedha

8 NOVEMBA, 2022

namna gani kwenye uchumi wetu vijana waweze kuchakarika tuanze kuona mabadiliko yanatokea kwenye zile sekta ambazo naamini Mheshimiwa Prof. Muhongo amezitaja vizuri. Kama hilo likifanyika naamini tutakuwa na kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa *issue* ya *inflation*, mimi naamini bado tuko vizuri. Asilimia 4.6 ni nzuri, lakini naamini pia kuna *suppressed inflation* hapa. Watu wanaona bei zinakua sana, lakini tukienda kwenye karatasi tunaambiwa ni asilimia 4.6. Haiwezekani iwe 4.6 wakati Ulaya ambako *inflation* yao kwa kawaida ni 2% mpaka 3% iko asilimia 10. Ukienda UK ni asilimia 10, EU huko kwa wastani ni asilimia 10, na ni *plus!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *East Africa*, nchi za wenzetu hawa, wao *inflation* ni 9%. Wastani wa *block* yetu ni asilimia 9.5. Ukisema sisi ni asilimia 4.6, nasema na sisi tuko kwenye kisiwa fulani ambacho Mungu ametubariki. Kwa hiyo, naamini pengine siyo rahisi sana kufikia lengo hilo ambalo tumejiwekea sasa hivi ni 3% mpaka 5%, tutajiminya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana lazima tuache ile *monthly accommodation* kwamba mikopo itolewe kwa sababu kinacho-*drive inflation* ni mikopo ambayo inaongeza ujazo wa fedha, kufukuzana na *supply* ndogo. Kwa hiyo, lazima mikopo itolewe ili tufungue mwanya huo ili tuweze kusaidia sekta zile ambazo zinahitaji mikopo ili ziweze kuongeza uzalishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kubana kiasi hicho, lazima tufuate *monthly accommodation* kukubali kwamba tuongeze kidogo *inflation* lakini kwa sababu ni

8 NOVEMBA, 2022

muda mfupi, pengine ugavi (*supply*) itajifungua, halafu *inflation* itaanza kushuka tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa kilimo naona matatizo. Ukweli ni kwamba tumejitahidi, lakini gharama za kilimo zimeongezeka sana. Kwenye korosho kwa mfano, wametumia gharama kubwa, wanasema kwamba bei za chakula duniani zinapanda kila mahali, lakini yule mtu aliyetumia gharama kubwa sana za kuvuna korosho yake *this time* anaambiwa bei zimeshuka. Hii dunia inatuonea namna gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani jitihada tunazoona Mheshimiwa Rais wetu anafanya kutafuta masoko, *specific* masoko kwa Marekani, ndiyo jitihada tunazohitaji kwa mazao mengine ili tuwe na *a captive market* ambayo tunajua kabisa kwamba kwa bei za kule tutapata kiasi hiki, lakini sasa hatuwezi kumwambia mtu aliyetumia gharama sijui mara ngapi, halafu unamwambia eti bei ya kuuzia korosho sasa imeshuka. Wanalia! Mimi nimesikia wanalia, lakini siyo kwa korosho tu, ni kila zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ilivyo kwenye kilimo, wale wenzetu wanatusubiri, wanatupiga. Wewe unatumia gharama kubwa, unaenda *step* mbili *forward* unarudi nne nyuma kwa sababu bei inashuka unakuta *income* yako ni ile ile, gharama hujai-recover. Ni ngumu sana. Kwa hiyo, naona tuangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kuna tatizo lingine kwa upande wa mabwawa, ni mojawapo ya kufanya *decision*. Ni kwamba pale unapoona kwamba kuna mwanya wa mfanya maamuzi ili kupendelea, *the only*

8 NOVEMBA, 2022

way ni kumfanya afanye kitu kwa haki. Kila mtu apate kwa usawa, basi unaamua kuweka *rules* au vigezo ambazo zita-*guide* ile *decision*. Ukiwa na *rule*, ni lazima kama yule mtu anagawa kwa mfano *cake* ya Taifa wanagawa hapa, ile bajeti ya kilimo inagawanywa, kungekuwa na *rooms* zinazosema kwamba ili upeleke bwawa mahali fulani, ni lazima kigezo hiki na hiki kifikiwe. Siyo unaenda kufikiria tu mwenyewe, unaamua peke yako, unaweka bwawa kubwa hakuna hata mtu, yaani mwaka mzima upepo ni mkubwa hata kitu hakioti, wewe unaenda kuweka mabwawa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuweke vigezo ili kuhakikisha kwamba *decisions* zinafanyika kwa uhakika na kwa njia ambayo ni *objective* na sahihi. Kwa sababu fedha hizi za kwetu kwenye bajeti na kwenye mpango zinapotea wapi? Kwenye matumizi. Wewe utatafuta hela nyingi utapata, lakini kwenye matumizi ukitumia ovyo ovyo tu, ukatupatupa hutapata tija. *It is not efficiently invested and you don't get anything.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani naomba, hata tusipoongeza ile bajeti, lakini tukatumia kwa namna ambayo itatumika na itasimamiwa vizuri na miongozo ikatolewa sahihi na watu tuone; tutaiona hapa Bungeni, lakini miongozo itolewe, watu watumie kwa haki na wawe waadilifu na hatua zichukuliwe. Niliona Wabunge walikuwa wakali sana kwenye *CAG report*. Kwa hiyo itumike, naamini tutafika mahali penyewe na hakuna haja ya kuongeza kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunasema uchumi ukue lakini kwenye mazingira tulivu, *natural economic stability*. Sasa *issue* inajitokeza ni hivi, niliangalia bajeti kwa

8 NOVEMBA, 2022

mfano ya wenzetu, majirani zetu, mwaka jana wao hawakutangaza *new measures* za *revenue*, walisema *revenue measures* za mwaka jana zitaendelea ku-*hold*, unaona lakini tutaongeza ufanisi kwenye ukusanyaji na kuziba mapengo kwenye ukusanyaji wa kodi. Kwa hiyo sasa maana yake nini? Ie kalenda ya kodi ikawa izingatiwe kwa hiyo tunamuomba pia Waziri, anapoenda kufikiria hili aione kama...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Dkt. Kimei. Kwa maana hiyo Waheshimiwa Wabunge lazima tuwe na *inclusive growth* kwenye kilimo, *tourism*, madini, uchumi wa bluu. Kila eneo la uchumi tuwe na *inclusive growth*, bila hiyo hatutafika haya malengo na Waziri wa Fedha nafikiri anayajua haya vizuri na yeye atatusaidia tufike kwenye malengo hayo.

Mheshimiwa Amar, wajiandae Mheshimiwa Njalu na Mheshimiwa Kamoga.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kidogo kwenye huu mpango. Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ameniwezesha kunipa afya njema na kuweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyotoa mwongozo kwamba unaweza ukasema ametangulia kusema

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Muhongo profesa, Mheshimiwa Kimei na mimi hapa darasa la saba naomba nitoe mchango wangu, pamoja na kwamba wamenitangulia hawa vigogo. Mpango huu kwanza nianze kumpongeza Waziri wa Fedha kwa Mpango mzuri ambao ameuweka hapa mbele tuweze kuujadili. Nitakuwa na yangu machache sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kama atakumbuka huwa nalalamika kila mara, kila Bunge linapofikia kipindi kama hiki kwa kumwambia kwamba upotevu wa fedha kwenye maeneo mbalimbali ni upotevu mkubwa sana ikiwa kwenye maeneo hususani kwa wafanyabiashara. Hili pato ambalo tunalizungumzia limekua, lingeweza kukua zaidi iwapo tutaendelea kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo yetu ya watu wanaofanya biashara. TRA ina upungufu kidogo pamoja na kwamba inafanya kazi vizuri, lakini kuna wafanyakazi au watumishi wa (TRA) ambao siyo waaminifu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano kwenye Jiji la Dar-es-Salaam kwa sababu naishi hapo, ukweli ukizunguka kwenye maeneo mbalimbali ya wafanyabiashara, hususani kwenye maduka unakuta watu wengi wananunua bidhaa na hawapewi risiti. Hili lipo kwa asilimia mia moja linafanyika, kama wanatoa risiti basi ni kwa asilimia kumi ama kumi na tano na hao wanaotoa risiti, umenunua mali ya shilingi milioni moja, unapewa risiti ya shilingi laki moja. Hawa wafanyabiashara wanapata wapi hicho kiburi? Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba hili ulichukue ukae na hicho kitengo cha (TRA) wajaribu kuangalia huu upungufu watazuia vipi, kwa sababu leo hii tuna mambo mengi ambayo tunahitaji yakafanywe kwenye maeneo yetu. Kama fedha haitakusanywa vizuri, haya maeneo yatafanyiwa vipi kazi? (Makofi)

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna maeneo mengine ambayo inabidi tuyaangalie. Kuna watu wanahitaji kulipa fedha za Serikali kupitia *control number*, unakuta mtu anafuatilia siku tatu nne mpaka wiki hajapewa *control number*, je, hiyo fedha aliyonayo mfukoni haitapata kazi nyingine? Suala hili nalo wajaribu kuliangalia sana kwa sababu watu wanaenda kuomba kulipa fedha ya Serikali, kuna tatizo gani kumpa siku hiyo hiyo *control number*? Inachukua mpaka wiki nzima, *control number* haijatolewa. Huu nao ni upungufu na unasababisha kupunguza mapato ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia mpango wa Serikali, namna gani tuboreshe tuweze kukusanya pato la Taifa. Nizungumzie upande wa madini, wachimbaji wetu wa madini hivi sasa wanaongeza ama wanachangia pato la Taifa kutoka asilimia nne mpaka asilimia nane. Hata hivyo, watu hawa wachimbaji wetu ama sekta hii ya madini ikiwaboresha vizuri wachimbaji kwa kweli Wizara hii ya Madini inaweza ikachangia pato la Taifa hata zaidi ya asilimia ishirini. Nitatoa mfano kidogo, wakiwezesha hawa wachimbaji wetu, mfano, STAMICO anafanya utafiti wa kufanya *explorations* ili kujua huyu mchimbaji anapata wapi madini na kwa kiasi gani ili aweze kupata mapato makubwa. STAMICO ama hawa GST wanafanya gharama zao kuwa ni kubwa sana, kiasi kwamba, hawa wachimbaji wadogo ama wachimbaji wa kati wanashindwa kumudu gharama za kufanyia *explorations*, matokeo yake wanakwenda kufanya uchimbaji ambao ni *local*. Kwa hiyo mapato hayapatikani kwa wingi, lakini wakiwezesha kwa kupunguziwa gharama za kufanyia *explorations* na pia kuwezesha vyombo vya kiuchimbaji vya kisasa, naamini kabisa Wizara ya Madini inaweza ikaongeza pato lake

8 NOVEMBA, 2022

katika Mfuko wa Taifa kwa kiwango kikubwa sana.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukusanya mapato hayo, tunahitaji tufanyiwe mambo mengi. Hata hivyo tuangalie kwenye upande wa sekta ya kilimo, leo hii mvua zetu zimekuwa ni za rasharasha, lakini kilimo kinachangia kipato kikubwa sana. Leo hii katika maeneo mbalimbali tumekuwa na ukame, lakini mvua zinaponyesha kuna maji mengi yanapotea, kwa nini Serikali ama Wizara ya Kilimo isiweke mkakati mzuri wa kuweza kujenga mabwawa makubwa ili sasa kipindi chote cha mwaka kiwe ni kipindi cha kulima. Wakulima watakapopata mazao ina maana tunanyanyua pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano kidogo, kwenye maeneo kama vile Jimbo la Nyang'hwale. Jimbo la Nyang'hwale tuna maeneo mengi sana ya mabonde ambayo maji yanatiririka yanakwenda Ziwa Victoria. Yale maji yangeweza kutegwa na kuweza kumwagilia na kupata mazao, tungeweza kuchangia pato. Hilo ni eneo moja, je, ikiwa kwa nchi nzima? Kwa hiyo naomba hili nalo lichukuliwe liwe katika vyanzo vyetu vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vyetu vya mapato tukivipata, basi Serikali isisahau basi kuweka mpango wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Busisi - Nyang'hwale kwenda Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Ahsante sana.
(Makofi)

8 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silanga, wajiandae Mheshimiwa Kamonga na Mheshimiwa Salimu Mussa Omar.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Mpango wa Taifa. Nitaanza kuipongeza Wizara kwanza jinsi inavyofanya kazi yake na jinsi inavyorejesha mrejesho kwa wananchi na tunaona matunda yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo Serikali ikiyachukua na kuyafanyia kazi, naamini tutakuwa na pato kubwa la Taifa kwenye nchi yetu. Tunayo Bandari ya Dar-es-Salaam, Bandari ya Dar-es-Salaam imezidiwa na mizigo, lakini tunayo Bandari Kavu ya Kwala, wakichukua Mpango Mahususi wa haraka kwenda kuipunguzia Bandari ya Dar-es-Salaam tukaiboreshe ile Bandari Kavu ya Kwala, naamini pato letu litaongezeka kwa kasi sana kulingana na mizigo mingi inayopita hivi sasa. Nasema hivi kwa sababu mizigo inayopita pale ya *transit* kwa maana ya *DRC-Congo, Zambia, Malawi, Uganda* pamoja na Rwanda. Kwa hiyo utaona kwamba Bandari ya Dar es Salaam ime-*stuck* na meli nyingi ukitazama zimesimama zile ni fedha na ndiyo mipango tunayoijadili hapa. Kwa maana hiyo tukitumia ile Bandari Kavu kwa muda mfupi na kwa haraka zaidi naamini pato letu litaongezeka na mahitaji tutakuwa tunayapata kwa haraka zaidi kulingana na vyanzo tulivyonavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Serikali basi iangalie umuhimu wa kuangalia uwekezaji katika maeneo mbalimbali. Tunayo *port* ya Kigoma lakini na Ziwa Tanganyika, naamini maeneo haya Serikali ikiyachukua na kuanza kuyafanyia kazi, tutapata mapato

8 NOVEMBA, 2022

ya kutosha. Vilevile uwekezaji wetu na mipango yetu tunayoipanga inategemea na mali tunayoingiza kutoka katika maeneo mbalimbali, lakini tofauti za kibiashara ukiangalia kwa Ruvuma tunayo makaa ya mawe, tukiiboresha Bandari ya Mtwara, ina maana katika uchumi, kibiashara zaidi tutavutia wawekezaji wengi wa kutosha na vilevile Bandari ya Mtwara itabeba mzigo wa kutosha kwa maana makaa ya mawe ukiangalia na changamoto iliyopo sasa hivi tutajikuta pato letu linaongezeka kwa kasi kubwa sana. Pamoja na hayo na mipango tunayoendelea kuifanya, tunayo mipango sasa hivi tunakuja na Bima ya Afya, maana yake nini? Mipango na fedha zote tunazozitafuta hizi, tukiboresha mazingira haya yote tunayoyapanga, Watanzania watatibiwa bure kwa sababu tayari watakuwa na mchango ndani ya Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile juzi Jumamosi wakati tunapitisha hoja za CAG, tulikuwa tunaangalia mapato na matumizi yasiyo rasmi na vitu vingine. Ushauri tu kwenye Mpango wa Taifa kupitia Waziri wa Fedha, basi angeenda kuangalia namna gani ataelekeza fedha zingine, mfano, kwenye halmashauri zetu tunatoza asilimia moja ya mapato ya ndani ambayo wakulima ndiyo wanayazalisha wao na tunatoa asilimia mia moja. Asilimia arobaini inaenda kwenye maendeleo na asilimia sitini inabaki kwa matumizi ya ndani. Kwa nini asilimia ishirini isitolewe ikaelekezwa kwenye sehemu ya Bima ya Afya kwa wananchi ambao wako kwenye mazingira magumu huko vijijini ambayo ukiitengenezea mpango itasaidia kwa Taifa letu kwa sababu wananchi ndiyo hao hao wanaozalisha na ndiyo hao hao tunaowatoza kodi, kwa nini wasibaki na asilimia arobaini ya matumizi na asilimia ishirini ikaenda kwa wananchi na asilimia ishirini

8 NOVEMBA, 2022

ikaenda kwenye maendeleo ambayo tunayatarajia kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, mipango tunayoiweka hii basi tuweke na mipango ya kudhibiti wizi unaoendelea kwenye nchi yetu hii, kwa sababu bila ya kuwa na mpango wa kudhibiti nako ni sehemu ya tatizo. Ukisikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge, lakini na hali iliyopo kule vijijini kwa wananchi na mabilioni tunayoyataja hapa utaona bado hatujafanya kazi ya kudhibiti fedha. Bado tunafanya kazi ya kukusanya mapato mengi lakini matumizi yake yanaenda nje ya utaratibu. Hii ni hatari na wananchi hawawezi kutuelewa, lakini kwa vile Serikali ipo na inasikia ni vyema sana kila ngazi inayohusika ikahakikisha inadhibiti kile ambacho tunakipata ili kiende kufanya kazi inayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo naamini kabisa Taifa letu ni tajiri na lina mipango mizuri na kazi zinazoendelea vizuri kwa sababu tunaendelea kupata fedha kutoka nje lakini na sisi humu ndani tuna fedha, ni vyema sana tukatumia tulichonacho pamoja na za nje zikasaidia Taifa letu lakini kwa mipango tunayoiweka halafu fedha hizo zinaenda nje ya utaratibu, kwa kweli hii ni hatari na wananchi hawawezi kutuelewa. Hivyo, ni vyema sana tukajikita kwenye sehemu ambayo tunaweza tukafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tukienda sehemu ya uzalishashaji. Wenzangu wamechangia vizuri kwamba tunayo maeneo muhimu sana ambayo nchi kama nchi inaweza ikayagawanya. Watawala wa mwanzo Hayati Mwalimu aligawanya majukumu Mtwara akaweka korosho, Lindi akaweka mbao, Rukwa akaweka kilimo

8 NOVEMBA, 2022

yaani kila maeneo aliweka utaratibu. Sasa ni vizuri mipango tunayoipanga tukaangalia nini kwenye nchi yetu ambacho kinahitajika kwa uharaka zaidi? Eneo fulani tukaliwekea utaratibu, tukaanza kutengeneza uzalishaji. Tukiweka katika mazingira hayo, naamini kabisa tutafanya mambo makubwa na kelele zitakuwa zimepungua, lakini vilevile wananchi wataelewa tunafanya nini kwenye Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Kamonga, Mheshimiwa Omar amepata dharura, Mheshimiwa Neema atakuwa jioni, wajiandae Mheshimiwa Chege na Mheshimiwa Michael Costantino.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wataalam wake ambao wameshirikiana katika kuainisha vipaumbele mbalimbali. Katika kipaumbele ambacho kimenivutia zaidi ni kuona kwamba sasa Mchuchuma na Liganga inapaswa ianze kufanya kazi. Hili sio kwamba limeandikwa huku, niwe shuhuda hapa, hata kule jimboni kwangu wananchi wanaendelewa kuhakikiwa kwa ajili ya kulipwa fidia na maeneo yaliyosalia nayo yanaendelea kufanyiwa uthamini kwa ajili ya ulipaji fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumashukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha hizo bilioni 11 kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi wa Nkomang'ombe, Iwela,

8 NOVEMBA, 2022

Kipangala, Mundindi, Amani na wengine ambao walikuwa na mashamba yao kwenye ile miradi. Kwa hiyo niishukuru sana Serikali na niombe sasa baada ya uhakiki tu, wananchi wale waweze kulipwa fedha zao na miradi ianze kama ambavyo Serikali imeweka kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napiga hesabu ndogo hapa, ule Mradi uliokwama wa makaa ya mawe, sasa hivi makaa ya mawe yamepanda sana bei duniani. Tani moja inafika mpaka *USD* 350 kwenye Soko la Dunia, lakini kwa ndani ni *USD* 50. Sasa ule mradi ulikuwa una mpango wa kuzalisha tani milioni tatu za makaa ya mawe ambazo ukizidisha tu kwa hizi *USD* 50 unaona kwa mwaka Serikali ingekuwa inapata karibu trilioni mbili kutokana na makaa ya mawe. Hizi ni fedha nyingi sana ambazo zingetusaidia sana kuepukana na zile kodi ambazo ni kero ambazo tunazianzisha na wananchi wanatulalamikia. Nadhani wazo sasa la kuona hii miradi ianze ni la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile upande wa Liganga, ule mradi ulikuwa umekusudia kuzalisha tani milioni 2.9 na kwenye Soko la Dunia kile chuma ghafi kwa tani moja ni *USD* 81.5. Kwa hiyo ukichukua hiyo, ukizidisha mara tani milioni 2.9 utaona kuna trilioni tatu na *point* ambazo Serikali ingelikuwa inazipata kutokana na uzalishaji wa chuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechelewa sana kuanza hii miradi, uchumi wetu umechelewa, lakini kwa kitendo cha kuingiza kwenye Mpango sasa, naomba Bunge hili liweze kuunga mkono Mpango huu na tuisimamie Serikali kuhakikisha kwamba miradi hii inaanza ili tuweze kuingiza mapato mengi kwenye nchi yetu.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hizo fedha pia kuna fursa nyingine nyingi, sasa hivi kuna changamoto kubwa sana ya ajira, sasa miradi hii ina uwezo wa kuajiri Watanzania hata milioni kumi ajira zile za moja kwa moja na bado kuna wale watakaokuwa wanapata ajira za udereva, wale watakuwa wanajijajiri kwenye kuanzisha *garage*, watakaoanzisha vituo vya mafuta na nyumba za kulala wageni, kwa hiyo tutatengeneza ajira nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia takwimu za sensa ya watu na makazi ambazo Mheshimiwa Rais wetu amezisoma hivi karibuni, utaona Mkoa wa Njombe una idadi ndogo ya watu. Idadi ile siyo kwamba ndiyo watu wote walioko Njombe. Hii ni ishara kwamba Njombe watu wanazaliwa na kuhamia maeneo mengine. Kwa hiyo tunavyofanya *decentralizations* ya hizi *projects*, tunavyotawanya hii miradi tunasaidia vilevile *ku-control* ule mtawanyiko wa watu nchini, watu wasisongamane uelekeo mmoja. Kwa hiyo hawa watu milioni kumi wakipelekwa kule kwenye hizi ajira kwa kweli tutakuwa tumeinua sana uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na miradi hii, lazima ionekane pia kwenye miundombinu ya barabara, kuna ile barabara inayoanzia Itoni – Ludewa - Manda, nashukuru sana Serikali wameidhinisha bilioni 95 upande wa Itoni mpaka Lusitu na bilioni 179 kutoka Lusitu mpaka Mawendi, lakini barabara hii haijafika Makao Makuu ya Wilaya na haijafika kwenye Mgodini wa Makaa ya Mawe ambapo ni kilometa 68 na haijafika Manda ambako kuna bandari ambayo nayo ingeweza kuunganisha usafiri wa mizigo kwa sababu tuna meli ya mizigo ambayo haina mzigo pale Ziwa Nyasa. Kwa hiyo barabara hii ikikamilika

8 NOVEMBA, 2022

hata meli hii itaweza kufanya kazi vizuri na itapata mzigo wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara pia inayounganisha Liganga na Mchuchuma, kwenye uwekezaji huu dhamira na Mheshimiwa Rais, ionekane pia katika kuandaa mazingira ya miundombinu ya barabara na Kiwanja cha Ndege cha pale Njombe. Vilevile kutoka Mkiu – Liganga - Madaba na ile Liganga na Mchuchuma ni kilometa 70. Kuunganishwa kwa barabara hizi ni ishara tosha kwamba miradi sasa itakuwa inaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pale Mlima Kimelembe sasa hivi kuna wachimbaji wengine wadogo ambao wanashindwa kusafirisha makaa ya mawe, tulikuwa tunahangaika bilioni sita ili ule mlima uweze kukatwa, lakini kwa mapato haya kama iwapo tutakata mlima, tani milioni tatu za makaa ya mawe zitasafiri, mapato yake ni triloni mbili kwa nini tujiulize mara tatu kutoa bilioni sita kwa ajili ya kukata mlima? Kwa nini tujiulize kupata hiyo bilioni mia moja kwa ajili ya kukamilisha barabara? Kwa hiyo hoja ya msingi hapa ni dhamira, hivyo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili sasa niende kwenye kilimo. Ninaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa kipaumbele kwenye mipango yake kwenye sekta ya kilimo ni jambo zuri, vilevile kilimo kinakwenda sambamba na kuongeza thamani kwa mazao, viwanda mbalimbali ili kuongeza ajira kutokana na *crisis* ya ajira. Kwa hiyo, tuone pia namna ya kuongeza thamani ya mazao vile viwanda ili kuongeza thamani ya mazao kwa ajili ya kuongeza ajira.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imetoa fedha nyingi kwenye sekta ya kilimo lakini bado nako kuna upungufu wa watumishi. Nitatoa mfano, kule Jimboni kwangu ninavyo Vijiji 77 lakini ninao watumishi wapatao 48 tu, kwa hiyo ilikuwa ni muhimu sana hizi fedha tunazopeleka na hii miradi ambayo imepokelewa vizuri kule na wananchi tuongeze pia wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaipongeza Serikali kwa kutoa ruzuku kwenye mbolea. Najua mwanzo ni mgumu na niwashukuru wataalam, Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na wataalam wake kuna mtu anaitwa Ngairo, yule bwana anapokea simu saa 24, nampongeza sana, ila sasa ule udongo kule kwetu Ludewa unahitaji mifuko mitatu ya mbolea. Hivi asubuhi nimepata taarifa, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kuna ghala la pale Ludewa Kijijini kuna mbolea wananchi wanagawiwa, lakini foleni ni kubwa siyo tatizo, ila ombi lao ni kwamba, ekari moja inahitaji mifuko mitatu, mfuko mmoja wa *dap* wanapandia na mifuko miwili ya *urea* kwa ajili ya kukuzia. Kwa udongo ule ukiweka mbolea mifuko miwili huwezi kupata mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu kutokana na wao kusomea *field* wamekuwa wataalam saa nyingine kuliko hata wataalam wa kilimo, wanaweza kukabiliana na mazingira yao. Kwa hiyo, niionbe sana Serikali tuweze kuwasikiliza hawa wananchi badala ya kuwapa mifuko miwili tuweze kuwapa mifuko mitatu ya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, tumeanza sasa na changamoto na nimekiri kwamba Wizara inajitahidi, lakini tuongeze kasi ya kuwasimamia hawa mawakala ili

8 NOVEMBA, 2022

waweke vituo maeneo yale ambayo ni *catchment areas* zenye wakulima wengi waweze kupata mbolea kwa wakati bila usumbufu ili tuweze kufidia hii changamoto ya mazao ya chakula ambayo imejitokeza kutokana na bei ya mbolea kupanda sana mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi na tukaendelea kuboresha barabara za vijijini hakika tutakuwa tumemkomboa mkulima. Kwa sababu, ataweza kutoa

mazao yake shambani kuyapeleka kwenye soko kwa ajili ya kujipatia kipato. Na hii itaendelea kuwapa hamasa wakulima kuweza kulima zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mifugo na lenyewe pia kwa kuwa Wilaya yangu kwa mfano, nitatoa mfano Jimbo langu la Ludewa tunakwenda sasa kupata miradi mikubwa kutakuwa na uhitaji mkubwa sana wa maziwa, nyama, mayai na vitu kama hivyo. Sasa niombe Wizara ya Mifugo itusaidie kule kuna vyama vya ushirika vya wafugaji, lakini hawana madume bora kwa ajili ya kuboresha ile mbegu ya ng'ombe wa mawziwa waliyonayo. Kwa sababu Ludewa mpaka sasa kwa takwimu ambazo nilizipata inaonesha kuna ng'ombe wa nyama 33,000 kwa hiyo, hawawezi kutosheleza. Kwa hiyo, tungeweza kuanzisha *ranches* kule Ibumi na wataalam wa kilimo walishaomba maeneo ya mashamba zile *block farming* na hizi *ranch* kule eneo la Ibumi, Masimavalafu tunahitaji sana usaidizi wa Serikali ili kuweza kufikia malengo yetu ya kuongeza idadi ya mifugo.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele imegonga na mambo yangu sikumaliza. Niunge mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jafari Chege, jiandae Mheshimiwa Nusrat Hanje. Sorry, baada ya Mheshimiwa Michael Constantine atakuja Mheshimiwa Nusrat.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa maoni yangu kwenye mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali na hatimae mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya Taifa wa mwaka 2023/2024. Kwa sababu ya muda tu na kwa sababu ninayo mengi ambayo ningetamani na mimi nishauri ili yaweze kuingizwa kwenye utekelezaji wa mpango na hatimaye yaingizwe kwenye bajeti ili tutakapokuwa tunajadili mwakani basi mengi ambayo yanawagusa wananchi kwa ujumla wake Waziri wa Fedha pamoja na Serikali kwa ujumla wake, wawe wameyaweka kwenye bajeti ili angalao yalete ahueni kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu nichukue nafasi hii kwanza kupitia kidogo taarifa ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na mtikisiko wa uchumi wa kidunia. Pamoja na mambo mengine ametaja sababu mbili ambazo ndiyo zinasababisha sasa mtikisiko wa kiuchumi kidunia, moja ni vita inayoendelea Ukraine, lakini la pili amezungumzia mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka tu nishauri kwenye hili la mabadiliko ya tabianchi ukisoma vizuri taarifa ya

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Waziri, niombe tu alipe mkazo kwa sababu, mabadiliko ya tabianchi sit u kwamba, yanakwenda kuathiri uchumi wa nchi, lakini pia yana madhara katika afya ya kibinadamu kwa ujumla wake. Kwa hiyo, nilikuwa natamani sana lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanadamu tunaishi kutokana na ikolojia inayotuzunguka, lakini sote tunakubaliana kwamba, ikolojia ile imeanza kuathirika kutokana na shughili nyingi za kibinadamu, miti imeanza kukatwa na maeneo mengi sana yameanza kuathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, hivi ninavyozungumza nchi wanachama wa Jumuiya ya Dunia wako Misri wanajadili juu ya mabadiliko ya tabianchi. Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri uone namna ya kulijazilisha vizuri, namna ambavyo Serikali tumejipanga kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kabla ya mwaka 2030 na kuendelea ili angalao isije ikafika huko tukakutana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema ya kwangu yatakuwa yale ambayo yanawagusa wananchi ambayo ningetamani yaingizwe kwenye bajeti. Kwanza, Mheshimiwa Waziri ningetamani sana bajeti ya mwakani pamoja na mpango wa bajeti hiyo ambao unakuja mwakani ili angalau tuweze kuujadili na kuupitisha, ni vema Wizara yako ingejipanga namna ya kuboresha na kuongeza mapato ya Halmashauri, hasa Halmashauri ambazo ziko pembezoni mwa mipaka ya nchi, lakini Halmashauri ambazo mapato yake yako chini ya bilioni moja.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani mpango wako na bajeti ujikite sana tutakapokuja kujadili uone namna ambavyo unakwenda kuzisaidia hizi Halmashauri ili angalao zisiendeleo kutegemea vyanzo vilevile kila mwaka. Mfano nitatoa, zipo Halmashauri ambazo zinategemea vyanzo viwili tu vya mapato. Ningeshauri sana kwenye Wizara yako kwa sababu huwa mnatenga fedha za miradi ya kimkakati na nimekuwa nilisema sana hili kwa Mheshimiwa Waziri. Muone hizi fedha za miradi ya kimkakati mpeleke kwenye Halmashauri ambazo mapato yake yako chini ya bilioni moja, lakini mapato yake hayako *stable*. Tungetamani kwenye bajeti ya mwakani inayokuja tupate angalao kujua fedha za miradi ya kimkakati zinazokwenda kwenye Halmashauri ambazo mapato yake hayako *stable* mnakwenda kuzisaidiaje? Kwa sababu, huko mbele haya mapato mwisho wake utafika yatakwishwa, maana yake hizi Halmashauri hazitaweza kujiendesha. Kwa hiyo, ningetamani kwenye mpango na bajeti yako Mheshimiwa Waziri uone namna ya kulifanya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye mpango na bajeti tutakayokuja kujadili mwakani, Mheshimiwa Waziri kwa sababu tunaishi na watu, ipo fedha ambayo inatolewa na Halmashauri ya asilimia 10 kwa ajili ya akinamama, vijana na watoto. Fedha hizi zinatolewa kulingana na kiasi ambacho Halmashauri zinakusanya. Zipo Halmashauri ambazo kiwango cha fedha wanachokusanya ni kidogo sana kiasi kwamba, kinachokwenda kwa vijana kwa ajili ya mikopo na akinamama hakitoshelezi. Ningetamani kupitia mpango wako uje utuambie nini mnajiandaa, hasa Halmashauri ambazo zinakusanya fedha kidogo kwa ujumla kwa vijana wa watu 10 unakuta mfano fedha wanayopewa ni

8 NOVEMBA, 2022

Milioni Moja au Milioni Mbili ambayo haitoshi hata kujiendesha kwenye kikundi hicho ambacho kipo. Mnao mpango gani kama Wizara na Serikali kusaidia hizi Halmashauri ili fedha inayokwenda angalao kikundi kimoja kikipata fedha kiweze ku-*sustain*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika hilo ningetamani kwenye mpango na bajeti yako Mheshimiwa Waziri, ni vyema ukaona namna ya kupitia utaratibu na sheria za mfumo huu wote ambao unatoa fedha zinazokwenda kwenye miradi kwenye hivi vikundi vya vijana, akinamama na walemavu. Ningetamani mpango wako na bajeti hiyo ije iseme namna mlivyojipanga kama Serikali kupitia upya namna ya utoaji wa fedha, namna ya kupata vile vikundi, namna ya pesa zinavyopata kwa sababu, hawa ndiyo wananchi ambao wametuzunguka huko, hawa ndiyo wangetamani kwenye bajeti ya mwakani waone namna ambavyo inakwenda kushughulika na changamoto zao kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika hilo ningetamani kwenye mpango na bajeti yako Mheshimiwa Waziri utuambie ni namna gani mnakwenda kujenga kama Serikali, barabara za lami kwenye maeneo ambayo yanaunganisha kati ya nchi na nchi, kwenye maeneo ya miradi ya kimkakati ambayo kimsingi yanaweza yakainua uchumi wa nchi, pia kwenye Mkoa na Mkoa? Ningetamani kwenye bajeti yako pamoja na mapendekezo utakayokujanayo mwakani ili mtuambie kwenye Halmashuri ambazo kimsingi zinagusana nchi na nchi angalao wapate kidogo barabara za lami ili ku-*sustain* na kuibua uchumi wa nchi ile pamoja na zile Halmashauri na hatimaye ninyi kama Serikali naamini

8 NOVEMBA, 2022

mtakuwa mmepata mapato mengi sana, ningetamani hilo pia Mheshimiwa Waziri uje utwambie ni namna gani ambavyo mmejipanga? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri katika hilo, uone namna ambavyo unaweza ukapitia Sheria za Manunuzi na utekelezaji wa maeneo mbalimbali. Sheria za Manunuzi ambazo ziko TARURA, RUWASA na maeneo mengine kwa sababu, naweza nikakutolea mfano Mheshimiwa Waziri; tumepitisha bajeti mwezi wa Saba, leo tunazungumza ni mwezi wa Novemba tunakwenda mwezi wa Disemba, bajeti ya fedha, fedha za mipango tulizopitisha kutekelezwa kuanzia mwezi wa Saba mpaka leo hakuna Mkandarasi site, hakuna kazi, maana yake ni nini? Hizi Taasisi zote bado zipo kwenye utaratibu wa kimanunuzi. Ningetamani kupitia ofisi yako upande wa *fiscal policy* au upande ambao wanahusika na mambo nya sera na sheria uone ni wapi ambapo tunakwama? Ni kwa nini tunapitisha bajeti mwezi Julai, lakini utekelezaji wake unakwenda zaidi ya miezi Minne katika utekelezaji wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kwamba, hata unaposema umeona kwenye bajeti yako wanasema angalao mwakani kuanzia Januari mpaka Juni, tunategemea uchumi wetu ukue kwa asilimia 5.3. Unaweza usikue kwa sababu, inawezekana mvua hizi zinazokuja barabara nyingi zitakuwa hazijatengenezwa. Hivi ninavyozungumza na wewe maeneo mengi umeme bado haujafika sawasawa, ninavyozungumza na wewe maeneo mengi bado miradi ya maji tuliyopitisha bajeti haijaanza kutekelezwa, hawa wote ukiwauliza ni utaratibu wa kimanunuzi ambao kimsingi ndiyo unasababisha hizi shughuli ziweze kuendelea.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani kwenye mpango na bajeti ili mje muone namna gani ambavyo mnaweza mkapitia, ili fedha inapotoka ya Serikali inakwenda moja kwa moja kwa mwananchi na isichukue muda mrefu na ikaleta maswali mengi sana kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningetamani nilizungumze na tulilisema hapa Mheshimiwa Waziri na umelisema kwenye hotuba yako ni pamoja na usimamizi wa fedha mnazopeleka. Umesema kwenye hotuba yako kwamba, utaimarisha na kupeleka fedha kuimarisha simamizi hizi, ofisi ndogondogo za Ukaguzi za CAG ambazo ziko kwenye Halmashauri. Mimi nikuongezee lingine, pamoja na mipango yako na bajeti tafuta namna ambavyo utaongeza usimamizi kwa kuwalipa fedha Wasimamizi Wakuu wa fedha za miradi huko ni Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye mpango na bajeti inayokuja mwakani ningetamani na penyewe uone namna hawa wasimamizi wa kwanza ambao leo unapeleka zaidi ya Bilioni Mbili kwenye Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, msimamizi wa kwanza wa kuhakikisha fedha inatumika ni Diwani. Sasa lazima angalao kwa kuwa unaandaa fedha za kwenda kulipa namna ya usimamizi - CAG, angalia namna ambavyo unaweza ukaweka mpango mkakati mzuri wa kuwalipa wale Madiwani ili kazi zao ziweze kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri ni kuhusiana na ulinzi na usalama. Mimi niko kule Rorya na maeneo mengine, ningetamani sana kwenye mpango

8 NOVEMBA, 2022

wa Serikali pamoja na bajeti muone namna ambavyo mnaweza mkapeleka fedha kwenye maeneo ya Maziwa na Bahari Kuu kuimarisha ulinzi na usalama wa maeneo yale. Niliwahi kutoa mfano hapa tunalinda sana maeneo ya maliasili na ndiyo maana tumeweka Jeshi Usu, ukienda kwenye madini kule wanalinda, lakini ukienda maeneo ya Maziwa na Baharini huku hakuna ulinzi wa rasilimali samaki na hakuna ulinzi wa wavuvi wanaovua maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano na niliwahi kusema hapa, ukienda Rorya leo wavuvi kila siku wanalia kupigwa na kunyang'anywa nyavu zao, kupigwa na kunyang'anywa samaki, hakuna ulinzi. Kinachohitajika kule ni *feasibility* ya ulinzi angalao Askari waweze kuonekana, lakini hawapo. Nini ambacho ningeshauri katika hili kwenye maeneo ya Maziwa na Bahari, kwenye mpango wako na kwenye bajeti Mheshimiwa Waziri, uone namna unaweza kupeleka fedha kwa mfano maeneo ya Kanda ya Ziwa yote na Mkoa wa Mara ambao wanaathirika na hii shughuli ya kupigwa na kunyang'anywa samaki. Peleka fedha watu hawa waweze kununua mashine, ipo mashine pale Rorya ambayo ukubwa wake na utumiaji wa mafuta ni mkubwa sana kwa siku wanatumia zaidi ya lita 600 hawawezi Askari wale kuimarisha ulinzi maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa wakiiomba Serikali iweze kuwasaidia kupata mashine ndogo za *watt power* 40 mpaka 50 ili waweze kuratibu ulinzi wa maeneo yale ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, wavuvi wanapigwa sana, watu wanafilisika kule. Ningetamani kwenye ulinzi na usalama

8 NOVEMBA, 2022

wa maeneo ya bahari Mheshimiwa Waziri nione namna mlivyojipanga kuimarisha rasilimali samaki kwenye maeneo ya maziwa ili angalao kuondokana na hili ambalo limekuwa likienda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningelisema hapa ni kuhusiana na kilimo. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa namna anavyokwenda, lakini ningetamani pia hii *block farming* ambayo inaendelea ingeenda na kasi kwenye maeneo mengi ya nchi, pia iende sambamba na hili suala linalokwenda la utambuzi wa udongo ambao unafaa kwa aina fulani ya zao, hasa kwa Mikoa ambayo haina mazao ya kimkakati na mazao ya kibiashara, ikiwemo na Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili likienda haraka litatusaidia sisi kulingana na yale mabadiliko ya tabianchi ambayo kimsingi yanatuathiri maeneo mengi na ndiyo yanatusababishia baadae ukame na njaa, kutakuwa hakuna chakula. *Block farming* inaweza ikatusaidia hasa tukiendana na kilimo cha *irrigation* kwenye maeneo mengi kwa kutambua mazao ya kibiashara kwenye Mikoa ambayo haina, ili kukingana na kuepukana na hili linalokwenda. Ningetamani sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha mtakapokuja kutenga fedha muendane kwanza na haya yote mliyoyapanga, lakini mwakani muende mtenge fedha kwenye Mikoa ambayo haina mazao ya miradi ya kimkakati ili kuweza kuimarisha na kuwapa fedha ili waweze kubuni, hasa Mkoa wa Mara ambao kimsingi umekuwa ukiathirika kwa kiwango kikubwa sana.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie moja kama muda utakuwa unaniruhusu. Lipo suala la utekelezaji wa umeme wa REA na hapa tumekuwa tukijibiwa sana, mimi ningetamani sana kwa baadae kuna umuhimu wa kuja kupitia kanuni ya majibu ambayo kimsingi huwa yanatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa umeme wa REA leo ninavyozungumza ambao kimsingi unakwamisha shughuli na bajeti tuliyopitisha, tusipolisema leo maana yake hata mwakani litakwamisha shughuli na bajeti tunayopitisha. Wakandarasi maeneo mengi hawako site au hawatekelezi, lakini Serikali imekuwa ikisema kufikia mwezi wa 12 tutamalizana na hili zoezi, haliwezekani Mheshimiwa Waziri. Mimi ningetamani kama linawezekana adhabu yoyote itolewe kwangu mimi itakapofika mwezi wa 12 kama Wakandarasi watakuwa wamemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano, Vijiji 13 Mkandarasi ametekeleza Kijiji kimoja tu ndiyo umeme unawaka, ana mwaka mmoja na nusu. Leo tumebakiza mwezi mmoja ukisimama ndani ya Bunge ukasema ndani ya mwezi mmoja utamaliza Vijiji 11 haileti maana. Mimi ninaomba sana fedha hizi za miradi, hizi ambazo zinachochea ukuaji wa uchumi kwenye umeme na maji zitoke kwa wakati, lakini usimamizi wake uweze kuwa imara sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Michael Constantine, ajiandae Mheshimiwa Nusrat na ajiandae Mheshimiwa Reuben.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipatia nafasi na mimi ya kuchangia mpango huu. Niombe kwanza kuipongeza Wizara kwa kutuletea mipango mara zote ambayo huwa inapokelewa vizuri kwa Wabunge, pia inapokelewa vizuri kwa wananchi na wanakuwa na matumaini makubwa ya kuona yanayopangwa yanakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia mpango, nimeusoma, nimesikiliza pia mapendekezo ya Wizara, nimesikiliza mapendekezo ya Kamati yetu muhimu kabisa inayochambua mpango kwa kina, nimeona vipaumbele vya Serikali, lakini kwa kweli nimevutiwa sana na kipaumbele hiki cha kusukuma na kuimarisha sekta ya uzalishaji. Katika maeneo haya, nami nimeona nitoe mchango wangu kidogo kwa kutazama maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwamba, Serikali imeweka mpango kwenye suala zima la sekta ya kilimo na wamezungumzia kwenye sekta ya kilimo eneo la kilimo cha pamoja. Ni jambo jema na niseme hili jambo si geni sana, kwa wale wakongwe wa miaka mingi, enzi za Mwalimu walikuwa na kilimo cha pamoja. Maeneo mengi ya vijiji yalikuwa na kilimo cha bega kwa bega na yaliwasaidia wananchi kwenye kuhakikisha kwamba, wanalinda kwa pamoja, wanavuna kwa pamoja na wanafanya mambo yao vizuri. Ni wazo jema leo Serikali imeona irudi kule na ifikirie kilimo cha pamoja kwa ajili ya kukuza uchumi wa wananchi. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo hapa liendeleo kutazamwa. Tumefikiria kuanzisha kilimo cha pamoja, lakini tumeenda kuanza kwenye maeneo ambayo upatikanaji wa maji ni wa kutegemea mvua. Yapo mabonde ambayo kwa hakika kabisa kama Serikali itatupia jicho huko, yana mabonde ya asili ambayo maji yanatiririka kwa muwa mrefu; tuna mabonde ya Mto Ruvu, tuna mabonde ya Mto Rufiji, tuna mabonde makubwa ambayo maji yake yapo miaka yote miaka nenda miaka rudi. Ni mpango tu wa Serikali kuwekeza nguvu kule na kuwasaidia wananchi waliopo maeneo yale kulima kulingana na maji yale yanavyopatikana kwa maana ya kuwapelekea pembejeo za kutosha, kuwapelekea mitambo inayoweza kufanya uzalishaji wa kisasa zaidi ili kuwaondoa kwenye kilimo cha jembe la mkono na uzalishaji ukawa mkubwa sana. Tukifanya hivi uzalishaji utakuwa mkubwa na Taifa hili linaweza kwenda kujiongezea kipato na linaweza kwenda kufanya mambo makubwa sana kwa sababu, wananchi wake watakuwa wamejitosheleza kwa chakula na wanaweza sasa kufanya utaratibu mwingine wa matumizi ya fedha inayobaki kama bakaa kwenye shughuli nyingine za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwamba, kuna suala zima limezungumzwa kwenye mipango kule la miradi ya kimkakati. Miradi hii ya kimkakati mingi inatekelezwa kwenye maeneo ya Halmashauri, lakini tangu tuanzishe hii *program*, sera hii ya miradi ya kimkakati ni miradi michache ya kimkakati imetekelezwa kwenye Halmashauri hizi. Kwa nini inatekelezwa michache?

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, vile vigezo vinavyowekwa kufikia kutekeleza hii miradi ya kimkakati, Halmashauri nyingine zinashindwa. Ukiangalia kwamba, Halmashauri nyingi nchini zina kipato kidogo, wako chini ya mapato yao ya ndani ya Bilioni 1.5 au Bilioni Mbili. Ukiangalia moja ya sharti ambalo wanalo wanatakiwa watengeneze mpango wao, wapitishie kila kitu kwenye ngazi yao, kwa gharama zao ndiyo waweze kupewa pesa hizi za Serikali kuendesha hii miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeishauri Serikali kupitia hili eneo, ingewezekana Serikali pale Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wangukuwa na timu maalum ya kutengeneza miradi, kwa sababu Halmashauri nyingi hazina wataalam wa kutosha, badala ya kutumia mapato machache ya Halmashauri kuwatafuta wataalam wa kuwatengenezea maandiko kungekuwa na timu maalum ipo pale Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo inakwenda kwenye zile Halmashauri zinazofahamika zina kipato kidogo kabisa, kwenda kuwasaidia kutengeneza mipango yao, ili ile mipango yao iweze kuwezesha na Serikali na iweze kuwasababishia kuwaongezea kipato kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kutumia mapato kidogo ya Halmashauri kuwatafuta wataalam wa kuwatengenezea maandiko, kungekuwa na timu maalum tu pale TAMISEMI ambayo inakwenda kwenye zile halmashauri zinazofahamika zina kipato kidogo kabisa kuwasaidia kutengeneza mipango yao ile iweze kuwezesha na Serikali na iweze kuwasababishia kuwaongezea kipato kwenye maeneo yao.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukibaki na hii sera, kwamba halmashauri ambayo haina kipato yenyewe ndiyo ijiandalie andiko ilhali hawana wataalam, wanachukua kilekile kidogo ambacho wamezalisha wanakwenda kumlipa mtaalam wa nje ili awatengenezee andiko. Sasa kwa kitendo kile, badala ya kutumia kipato kidogo kwa ajili ya kuendeleza shughuli za halmashauri wanakitoa tena kufanya shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali, hasa pale TAMISEMI, kuwe na timu. Inawezekana kabisa kukawa na timu moja pale iliyoandaliwa ya watu wachache, wataalam wazuri wa kuandika maandiko, wakawa wanakwenda katika halmashauri moja moja wanadaa maandiko na wanayafanyia kazi, hizo halmashauri zinaendelea kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kitendo hicho cha kuzalisha maana yake sasa uchumi wa eneo hilo utakuwa, kwa maana ya kwamba halmashauri itakuwa na mapato ya kutosha, lakini vilevile wananchi watakuwa na mapato ya kutosha. Na kwa kufanya hivyo basi Serikali itakuwa inakusanya kodi vizuri na Pato la Taifa litaweza kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninaomba nilizungumzie ni suala zima la utekelezaji wa miradi. Nishukuru nimesoma kwenye maoni ya Kamati, nimegundua wamezungumzia ufinyu wa eneo la Bandari ya Dar es Salaam; na wameona ufumbuzi pekee wa kuondoa tatizo la Bandari ya Dar es Salaam ni kutanuka kwenda kufanya shughuli kwenye Bandari inayofikiwa ya Bagamoyo.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Kamati na Serikali. Ushauri na rai yangu pale; niwaombe sana hili wazo si la kuliachia jamani. Wote tunaona sasa hivi nchi yetu tunaitumia Bandari ya Dar es Salaam kutoa mizigo kwenda nchi za jirani na ndilo eneo pekee linalotuingizia pato la kutosha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kwa kweli tukatengeneza ile Bandari ya Bagamoyo ikafanyiwa utaratibu ianze mchakato wake kwa sababu itaisaidia Bandari ya Dar es Salaam. Na kwa sababu Bagamoyo na Dar es Salaam ni jirani, meli zile zitakuwa zinafanya kazi vizuri na wakati huo zitakuwa zinatoa mzigo pale na kwenda kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali, kwenye bajeti inayokuja, kwenye mpango unaokuja, ni vizuri wakaiweka hii katika hatua ya kwenda kuitekeleza. Yale masharti ambayo yanaonekana yana changamoto ndio wakati Serikali kuyaondoa, na tutakapokuwa tumeyaondoa yale basi shughuli hiyo itakwenda kuanza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba ukiangalia suala la Bandari ya Dar es Salaam kwa maana ya kwamba na kuitazama hiyo Bandari ya Bagamoyo kuifikiria kwenda kuanza, ukiangalia Dar es Salaam kote ndiyo kunakoanza njia kuu zinazoweza kutoa mizigo. Tuna Reli ya Kati, tuna Reli ya TAZARA, tuna Barabara ya Dar es Salaam – Morogoro – Mwanza, na sasa tuna mwendokasi (SGR); zote hizi ni njia kuu za kusafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunategemea kule kwenye chanzo cha njia kuu za kusafirisha ndiko ambako

8 NOVEMBA, 2022

mizigo itashuka, sasa kwa sababu tayari nako tumeongeza Bandari ya Kwala ambayo nayo inawekwa pale kwa ajili ya kusaidia kupunguza mzigo wa Dar es Salaam, sasa itakuwa imekaa mwelekeo mzuri tu. Bagamoyo itakuwa inafanya kazi, Dar es Salaam inafanya kazi, Bandari ya Kwala inapokea mizigo; hizi reli nilizozitaja zinatoa mizigo kupeleka kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kufanya hivi niishauri Serikali, ni vizuri kwenye bajeti inayokuja ikawekeza nguvu hii miradi mikubwa kama huu wa Bagamoyo na barabara yake ya kutoka Bagamoyo kwenda maeneo mengine ili iweze kuungana na Kwala, mizigo iwe inasafirishwa kwa urahisi. Kwa kufanya hivi Pato la Taifa na pato la mtu mmoja mmoja litaongezeka. Tukifanya hivyo vilevile tunasababisha wawekezaji ambao wanakwenda kukaa kwenye maeneo yale ambayo miundombinu hiyo ipo watakuwa wanafanya kazi kwa njia rahisi zaidi, na kwa kufanya hivyo basi tutakuwa tunakamilisha malengo ya kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mimi nishauri na nitoe maoni machache. Kwanza niombe Serikali kwamba ifanye mapitio ya mabonde yote makubwa. Badala ya kukaa kuanza kufikiria ni maeneo gani tupeleke pesa za kilimo zikafanye kazi yenyewe ifanye kazi ya kupitia mabonde yote makubwa kama vile Bonde la Mto Ruvu, Wami, Mto Rufiji, kule Ifakara, kuna mabonde makubwa, waende kwenye maeneo hayo wakafanye utafiti wa kutosha kwa kupima udongo ule, waone unaweza kutumika kwa namna gani na maeneo hayo yanafaa kilimo cha namna gani, tupeleke hii bajeti

8 NOVEMBA, 2022

kubwa ya Serikali ya kilimo kwenye maeneo hayo ili tuweze kuondoa changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye maeneo hayo kuna suala limezungumzwa la kutengeneza programu maalum ya uwezeshaji wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sote humu ndani Wabunge tunafahamu, kila Mbunge amepiga kelele ni namna gani fedha zinavyotumika vibaya kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia tatizo la matumizi mabaya ya fedha kwenye halmashauri inawezekana likawa linasababishwa na usimamizi mdogo unaotokea katika sekretarieti za mikoa. Kwa hiyo hili wazo la kwenda kuwapatia hawa uwezeshaji mkubwa wa kuweza kusimamia unaweza ukasaidia kutupunguzia hizi changamoto za upotevu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye TAMISEMI nina jambo la kushauri kutokana na jinsi nilivyoona mpango; itoe maelekezo ya kutosha kwenye halmashauri juu ya namna bora ya kukusanya mapato, lakini pia namna bora wanayoweza kufanya *reallocation* ya matumizi ya pesa za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna namna ambavyo wanapanga kwenye bajeti. Bajeti zinapitishwa na halmashauri, zinakuja zinapitishwa hapa Bungeni lakini ikifika wakati halmashauri hizohizo ambazo zimeomba kupitishiwa bajeti hizo, wanaomba kufanya *reallocation* ya miradi yao, wanapunguza mapato yao waliyowekewa kukusanya.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii sera ingeangaliwa vizuri ili hii fursa isitolewe, kwa sababu unapotoa kibali cha kubadilisha bajeti uliyoiomba mwenyewe kwamba utakusanya maana yake unapunguza nguvu ya kukusanya mapato; na unapopunguza nguvu ya kukusanya mapato maana yake unasababisha mapato ya nchi yasiongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya machache hayo, naomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nusrat, wajiandae Mheshimiwa Reuben na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Miaka Mitano, mpango wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya uchumi, ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, maendeleo ya watu na vitu vingine. Hakuna Serikali ambayo inataka kuona watu wake wanateseka, haipo, kwa jinsi ninavyofahamu. Hakuna Serikali ambayo imejidhatiti kusimamia wananchi wake na kuhakikisha kwamba wanaishi katika mazingira mazuri na wanajikwamua kwenye umaskini ambayo inafurahia wananchi wake kupitia katika mfumuko wa bei uliokithiri, uchumi unaokua kwa kasi ya kinyonga na maendeleo ya watu yasiyo maendeleo ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi umekua kwa asilimia 0.4 kwa mujibu wa mpango huu na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini mfumuko wa bei bado

8 NOVEMBA, 2022

umeendelea kuishi nje ya malengo ya Serikali ambayo ni kwamba mfumuko wa bei ulikuwa ubaki *stable* kwenye asilimia 3.0 mpaka 5.0. Tumeshuhudia malengo ya Serikali yakiwa mbali kabisa na hali ilivyo kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia maendeleo ya watu maana yake tunategemea kuona watu wakijikwamua kwenye lindi la umaskini. Nimesema mwanzo kwamba haipo Serikali ambayo inatamani watu wake wateseke, kwa hiyo mimi naamini, pamoja na jitihada zote zinazofanywa na Serikali, lengo lao ni kuhakikisha kwamba wanawatengenezea Watanzania mazingira mazuri ya kuishi ili uchumi wa Mtanzania mmoja mmoja ukiwa mzuri Serikali kazi yake ni kukusanya kodi. Kwa hiyo ninaamini nia njema ipo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunajikwamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zipo sababu nyingi sana zimetajwa kwamba kwa nini tuna changamoto hizi, kwa nini bado mfumuko wa bei hauko *stable* kwa sababu kuna athari za vitu vingine ambavyo vimetajwa, masuala ya kupanda kwa bei ya mafuta, mbolea na nini. Kuna sababu nyingi ambazo sidhani kama tuna haja ya kujielekeza huko kwa sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri na Kamati wamefafanua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Deni la Taifa; kwa hali isiyo ya kawaida Deni la Taifa kutoka mwezi Aprili mwaka huu mpaka mwezi Juni mwaka huu, 2022, limeongezeka kwa kiasi cha shilingi trilioni 2.119 kutoka shilingi trilioni 69.44 Aprili mpaka shilingi trilioni 71.559.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajua kwamba ongezeko hili limetokana na kukopa kwa ajili ya

8 NOVEMBA, 2022

kuhakikisha kwamba tuna-*fund* miradi ya maendeleo ili tu-move, *it's well and good*. Na kwamba Deni la Taifa linahimilika, kwa sababu siku zote tumekuwa tunasema kwamba Deni la Taifa bado linahimilika, Deni la Serikali bado ni himilivu na nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa hapa tulipofika na tunapokwenda, kwenye shilingi trilioni 71.559 ninaomba Bunge hili liweke ukomo wa uhimilivu wa Deni la Taifa. Kwa sababu ni kweli tunakopa kwa ajili ya ku-*fund* kwa sababu hakuna mtu anakopa akafanye starehe, ndiyo maana nilisema kwamba hakuna Serikali inayotaka wananchi wake wateseke.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa binti yangu, Mheshimiwa Nusrat, kwamba Serikali inakopa kwa *factors* za kiuchumi, siyo *factors* za kuwekewa *limit*. *Factors* za kiuchumi za nchi ndizo zinazotoa *direction* ya Serikali kuwa na uwezo wa kukopa ama la. Tukisema Bunge liweke *ceiling* ya Serikali kukopa tutakuwa tunakwenda kinyume na *principles* za kiuchumi katika masuala mazima yanayoweza mambo ya ukopaji katika masuala ya kuendesha Serikali duniani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nusrat.

8 NOVEMBA, 2022

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma kwenye Taifa letu; tumesema nia yetu ni njema, hatutaki wananchi wetu wateseke na tunataka pato la ndani wananchi walifaidi wenyewe. Lakini kwa sasa hivi hali ilivyo tunaendelea kulipa madeni, *it's well and good* kwa sababu tunaona *flagship projects* na nini, lakini *aim* si ni kujenga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sikilizeni tushauri; kwanza kuhusu mwenendo wa biashara na huduma ndani na nje. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri na Mpango inatueleza kwamba tumekuwa tuna-*import* zaidi kuliko ku-*export*. *It's well and good* kwa sababu kwenye taarifa kunaonekana kuna ongezeko la kutoa bidhaa nje (ku-*export*) kwa asilimia 25, na kwamba tumetoka dola za Kimarekani milioni 8,811 mwezi Juni mwaka jana mpaka dola za Kimarekani milioni 11,116.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *progress*, lakini ukweli ni kwamba sekta ya utalii – na niwapongeze sana kwa jitihaa zilizofanyika – sekta ya utalii ndiyo imekuza hii; lakini ongezeko la ku-*import* ni kubwa kwa asilimia 39, limeongezeka kwa asilimia 39 zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana mwezi Juni kwenye ku-*import* tulikuwa tume-*import* kwa takribani dola za Kimarekani milioni 9,841 mpaka dola za Kimarekani milioni 13,715, sawasawa na ongezeko la asilimia 39. Tuki-*export* kidogo tuka-*import* zaidi tunajikosesha fedha za kigeni, maana na sisi Tanzania mazingira yetu pia ya biashara yanakuwa siyo mazuri.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe kwenye mpango huu Serikali ijielekeze zaidi katika kutengeneza mazingira yetu ya bidhaa za ndani ili tupunguze ku-*import*. Lakini pia kutengeneza mazingira ya kwetu ili tu-*export* zaidi; na hii ni *principle* ya kawaida tu ya biashara, wala haihitaji *Ph.D*, ni suala tu la kawaida, uki-*export* zaidi unapata mapato ndani zaidi, uki-*import* zaidi unatumia mapato yako ya ndani zaidi kupeleka kwa watu wengine, kwa hiyo ni biashara tu ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, kwa sababu tunatafuta ubunifu na mbinu zaidi kwa ajili ya kupata mapato kwenye nchi kwa sababu lengo si ni kuhakikisha kwamba Watanzania hawateseki? Sijaona. Nimeangalia mpango mzima, na nimeangalia kwenye hotuba nzima ya Mheshimiwa Waziri, sijaona kitu kinaitwa *carbon marketing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kutokana na mabadiliko makubwa ya tabianchi, nchi zenye misitu ikiwemo Tanzania sasa hivi zinafanya biashara ya *carbon*. Kwa hiyo nilitegemea kiwe ni chanzo kipya cha ubunifu cha kibiashara kwa ajili ya kuongeza pato kwenye nchi. Kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri atusaidie kuelewa mpango wa Serikali kwenye masuala ya kufanya biashara ya *carbon*. Najua anajua *carbon marketing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sehemu ya tatu na ya mwisho; sekta ya madini. Taarifa za Taasisi ya Jiolojia na Utafiti Tanzania (*GST*) inatuambia kwamba Tanzania tuna takribani *critical minerals* 24, kwenye utafiti ambao umefanywa na Taasisi ya Jiolojia na Madini Tanzania.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa amezungumza, lakini nafikiri tusaidiane kuelewa; ukisoma hotuba nzima ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 14 ambao amezungumza yeye kwenye hotuba masuala ya madini, ukurasa wa 68 ambao amezungumza masuala ya madini kwenye mpango, ukurasa wa 24 amezungumza masuala ya madini kwenye mpango, hakuna kitu kinaitwa *critical minerals*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tofauti kati ya *critical minerals* na *strategic minerals*. *Critical minerals* ni madini muhimu, *strategic minerals* ni madini ya kimkakati. Madini ya kimkakati maana yake ni madini ya kusaidia kukuza uchumi. Madini ya kimkakati ndiyo tumeyazoea tangu mimi nasoma; kuna *gold*, *tanzanite*, *aluminum* na madini mengine ya kawaida ambayo yanatusaidia kukuza uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia inazungumza mabadiliko ya tabianchi. Wakati tunatoka kwenye mhamo wa nishati (*energy transition*) kutoka kwenye nishati ambazo ni chafu kwenda kwenye nishati safi tunategemea kuna soko kubwa la madini muhimu. Madini muhimu ni pamoja na *graphite*, *lithium*, *helium*, *nickel*, *cobalt* na mengine, yako 24. Waheshimiwa Wabunge waende kwenye websites za masuala ya *energy*, kuna *International Energy Agency*, wana website yao, ukiangalia tu kwenye *tablet* yako unapata *information* nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa masikitiko makubwa sana, kwanza Sheria ya Madini ya mwaka 2009 haizungumzi chochote kuhusiana na *mhamo wa nishati (energy transition)* kuelekea kwenye *critical minerals*. Na

8 NOVEMBA, 2022

ni *well and good* kwa sababu tunataka tupate pato la nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *Geological Survey of Tanzania*, Tanzania ni ya tano kwa kuzalisha *graphite* lakini ina *reserve* ya tani milioni 18 ya *graphite* kweye ardhi. Na naomba niwaambie kwamba GST haina teknolojia ambayo ingetusaidia kujua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nina uhakika kabisa kuna uwezekano mkubwa sana hiki tunachokisema inawezekana Tanzania ni ya kwanza duniani kwa sababu hatuna teknolojia. Kwa hii teknolojia yetu ya kawaida tu imesababisha tujue kwamba kuna tani milioni 18 kwenye ardhi. Sasa hapo hatujazungumza *nickel*, hatujazungumza *rare earth minerals*, kwa sababu hizi *iPhones*, Waheshimiwa wana *iPhones* hapa, *iPhones* zinatengenezwa na aina ya madini ambayo ni *critical*, yanaitwa *rare earth elements*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mhamo (*transition*) wa nishati unatusababisha twende kwenye nishati ya jua, twende kwenye nishati ya upepo. Hizo *critical minerals* 24 nilizosema Tanzania zipo kwa mujibu wa GST, zinatusaidia kutengeneza *solar panels*, *wind turbines* – Kiingereza hapo kidogo, lakini sasa hatuna Kiswahili chake – mitambo ya kuzalisha umeme wa jua, mitambo ya kuzalisha umeme wa upepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia inazungumza *electric cars*, kuna madini ambayo yanatengeneza *electric car batteries*. Kwa hiyo tuache kuzungumza kuhusu *gold*...

8 NOVEMBA, 2022

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako, ni kengele ya pili.

Mheshimiwa Reuben, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Kapufi.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 08 Aprili, 2021 Waziri wa Fedha aliwasilisha hapa Mpango mkubwa wa nchi wa Miaka Mitano. Mpango huu wa miaka mitano ndio ambao umesababisha leo tunajadili mpango wa mwaka mmoja mmoja; na mpaka sasa tumekwisha jadili mipango miwili na sasa tuko kwenye mapendekezo ya mpango huu wa tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mpango ule mkubwa wa miaka mitano ambao ulikuwa wa 2021/2022-2025/2026 uliandaliwa kwa kutumia rejea ya vitabu kadhaa, nitavitaja harakaharaka; Dira ya Taifa ya Maendeleo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, hii niliyoishika na watu waione, kitabu makini kabisa; Mpango Elekezi wa Muda Mrefu, matokeo ya tathmini, sera na mikakati mbalimbali ya kisekta, Dira ya Afrika Mashariki 2050, Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hivi vitabu vyote nilivyovitaja hiki kimoja ndicho ambacho tulikwenda nacho kwa wananchi, ndicho ambacho tulikinadi, ndicho ambacho wananchi waliamua kwamba watakichagua hiki na wakaichagua Serikali ya CCM ili iweze kuleta maendeleo. Kwa hiyo mipango yote tunayoipanga lazima ilete tafsiri ya hiki kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huu mpango mkubwa kulikuwa na shabaha za mpango ambazo ziko tano. Na mimi leo nataka tuzipitie vizuri tukirejea mapendekezo haya ya mpango yaliyopo mbele yetu tuone kama yanaleta tafsiri ya hiki ambacho kipo kwenye mpango wetu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha ya kwanza ya mpango ule mkubwa wa miaka mitano inasema, “ukuaji wa uchumi kuongezeka kutoka asilimia sita mwaka 2021 hadi kufikia 58% mwaka 2026.” Ilani yetu ya Uchaguzi ukurasa wa 13 (b)(1) inasema, “kuweka sera madhubuti za uchumi jumla ili kukuza uchumi kwa wastani usiopungua asilimia nane kwa mwaka.” Hiki ndicho ambacho tumewaahidi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyongea kwa Januari mpaka Machi, 2022, uchumi wetu umeripotiwa kukua kwa asilimia 5.4. Hii ndiyo kusema tuko chini na nje ya mpango wetu ambao tumeuweka sisi wenyewe. Kwa hiyo, Serikali wanayo kazi ya kwenda kufanya kuhakikisha kwamba kitabu hiki wanakitafsiri na wanakitekeleza kwa namna ambavyo kinaelekeza. Kinataka ukuaji wa uchumi kwa asilimia nane, lakini Serikali imeripoti ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.4.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shabaha ya pili ilikuwa ni mapato ya ndani ukijumuisha mapato ya halmashauri kuongezeka kutoka asilimia 15 ya pato la Taifa hadi kufikia asilimia 16. Hivi tunavyozungumza ukisoma haya mapendekezo ya mpango yaliyoletwa mbele yetu, sura ya 3 (3), (2)(i) inasema, mapato ya kodi; kwenye mpango wanatarajia yafikie asilimia 12 ya pato la Taifa. Yaani mpango huu wa mwaka mmoja uko nje kabisa ya mpango mkubwa ambao ndiyo tumekubaliana kuufanya. Wao wanaongelea mapato ya kodi kufikia asilimia 12 ya pato la Taifa ilhali mpango mkubwa unataka tufikie kuanzia asilima 15.9 mpaka 16.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na mipango ya hivi. Mipango hii midogo ya mwaka mmoja mmoja inatakiwa itafsiri mpango ule mkubwa tuliojiwekea na ambao tumeupeleka kwa wananchi kuunadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha ya tatu ya ule mpango mkubwa inasema, “mfumuko wa bei kuendelea kuwa wa tarakimu moja, wastani wa 3% mpaka 5%.” Naipongeza Serikali kidogo hapa kwa sababu wamejitahidi sana kuweka mfumuko wa bei kwenye *single digit*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikilizeni niwaambie jambo muhimu unapoongelea mfumuko wa bei na hasa kwa Watanzania. Jambo la muhimu kabisa tunapoongelea mfumuko wa bei kwa Watanzania wa kawaida na wananchi walio wengi tunaongelea mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi. Hicho ndicho kinachogusa Watanzania. Taarifa hii ya mpango mpaka kufikia Agosti, 2022, mfumuko wa bei za vyakula na vinywaji baridi uko asilimia 7.8; *it is above 3% to 5%*.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya mfumuko wa bei ya chakula, nitumie hii nafasi niombe sana Serikali, kama kuna vyakula kwenye maghala sasa hivi, waruhusu viende kwa wananchi. Hali ni mbaya sana. Hivi sasa Handeni Mjini... *(Makofi)*

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimefurahishwa sana na mchango wa kaka yangu, Mheshimiwa Mbunge ninayemheshimu sana, lakini napenda kumpa taarifa kwamba analolizungumza, tayari Serikali ya CCM wameshaliona. Leo ninavyozungumza, Ikungi tumepokea Tani 100 za mahindi kuwauzia wananchi kwa bei ambayo itapunguza *tension*. Kwa hiyo, kwa kweli Serikali na Wizara ya Kilimo tunalshukuru sana. Naomba nimpe taarifa hiyo. Sasa itakuwa ni vyema na kule kwake wapeleke. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Reuben.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawazungumzia wananchi wa Handeni ambao mpaka leo asubuhi wamenunua kilo ya sembe kwa shilingi 2000. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge, mahindi yamefika kwake Ikungi, hilo ni jambo la kuishukuru Serikali ya CCM. Ninachosema hapa ni kwamba Mpango huu uwe wa Kitaifa na siyo wa Ikungi

8 NOVEMBA, 2022

peke yake. Kwa hiyo, ni muhimu sana tukazingatia kilichopo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, hili la chakula narudia tena, naomba Serikali kama ina chakula kwenye maghala, *i-offload* ili mahindi yawafikie wananchi kwa bei ambayo itakuwa ni elekezi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha namba nne ambayo mpango mkubwa umeuweka inasema, akiba ya fedha za kigeni kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa. Hili nalo naipongeza Serikali. Mpaka sasa wamejitahidi sana ku-*maintain* akiba ya fedha za Kigeni *around 5.1 billion US Dollars* ambazo zina uwezo wa kuagiza vitu kutoka nje *monthly* kwa asilimia 4.6. Kwa hiyo, hili nawapongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwenye ule mpango mkubwa, ni sekta binafsi kuzalisha ajira zipatazo 8,000,000, ndicho tulichokubaliana na ndicho ambacho tumekipeleka kwa wananchi. Ukifungua Ilani ya Uchaguzi ukurasa wa nane kipengele cha f(1) hadi (4) inasema, “kutengeneza ajira zisizopungua 8,000,000 katika sekta rasmi na isiyo rasmi kwa ajili ya vijana.” Wamesema, hayo yanaweza yakafikiwa endapo tutawekeza kwenye kilimo, mifugo, uvuvi, madini, maliasili, sekta za huduma na utalii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ajira 8,000,000, mwaka wa kwanza wa mpango umepita, na mwaka wa pili wa mpango umepita. Tafsiri yake ni nini? Ni kwamba mpaka sasa Serikali ilitakiwa iwe imezalisha ajira milioni 3,200,000. Namtaka Waziri mwenye dhamana ya huu mpango atakaposimama hapa atuambie wamezalisha ajira ngapi? Kwa sababu kama ni 8,000,000, maana yake kila

8 NOVEMBA, 2022

mwaka ni 1,600,000. Kwa hiyo, kwa miaka miwili ambayo tayari tumeshaimaliza, ilitakiwa tuwe tumeshatengeneza ajira 3,200,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili nisiishie tu kukosoa, niwashauri pia kwamba hatuwezi kuzalisha hizi ajira ikiwa hatukufanya uwekezaji. Siongelei ule uwekezaji ambao ninyi mna mtazamo nao Serikalini; siongelei ule uwekezaji wa mtu anatoka nje na fedha anakuja kufanya jambo hapa. Naongelea uwekezaji wa kuwawezesha Watanzania kuzalisha. Tunaongelea habari ya kilimo, tunataka Serikali yetu iwawezeshe Watanzania kwenye kilimo, tuwe na *millionaires* na *billionaires* kwenye kilimo ambao ni Watanzania. Ukiongelea mifugo, tunataka tumwone tajiri mmoja Mtanzania ambaye Serikali hii imemtengeneza. Tunataka tumwone mvuvi mmoja, vivyo hivyo na kwenye madini. Kwa hiyo, lazima tuwe na uwekezaji ambao ni *very strategic*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikilizeni niwaambie; ukanda wote huu wa Bahari kuanzia Dar es Salaam, shuka Tanga nyumbani pale, mpaka Mtwara na Lindi, ni aibu kwamba hatuna hata kiwanda kimoja kikubwa cha ku-process Samaki. Ni aibu! Sasa tunaongelea uchumi gani kama hilo hatuwezi kufanya? Uwekezaji ninaousema ni ule unaojikita kwenye *big production chains*. Mfano mzuri, tazama Kiwanda cha Cement kilivyo pale, uone *chain* ambayo iko *involved* kwenye kiwanda. Vivyo hivyo ndiyo itakuwa kwenye Kiwanda cha Samaki na maeneo mengine. Kwa hiyo, tujikite kwenye maeneo hayo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

8 NOVEMBA, 2022

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, jiandae Mheshimiwa Kapufi na Mheshimiwa *Engineer* Samweli.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii nami nitoe mchango wangu kidogo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa letu kwa mwaka mmoja unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia ya sasa tunayoishi, viongozi wa zama zetu sisi, tutapambana na changamoto nyingi. Ukisoma taarifa ya Benki ya Dunia wanaweka changamoto 20, *of course* ndani yake humo yapo na yale mambo ambayo sisi hatuyakubali hapa kwetu, lakini katika yale mambo ambayo sisi tunayakubali, angalau nizungumzie matatu makubwa katika hizo changamoto. Ya kwanza ikiwa ni mabadiliko ya tabia nchi, pili ni umasikini uliokithiri, na ya tatu ni ile inayohusiana na njaa. Amezungumza vizuri sana Mheshimiwa Reuben Kwagilwa changamoto inayohusiana na kukosekana na uhakika wa chakula mezani miongoni mwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi tatu zinahusiana kwa ukaribu sana, moja, baada ya nyingine; zina *connectivity* ya ukaribu sana. Kwa mfano, changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi inapelekea kukosa uhakika wa chakula kwa watu wetu ambao wanategemea kilimo cha jembe la mkono. Hii moja kwa moja inaenda kusababisha mfumuko mkubwa sana wa bei (*inflation*). Amezungumza

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Kwagilwa, sina haja ya kurudia. Kwa sababu umasikini uliokithiri ambao unapimwa na Benki ya Dunia kwa kigezo kipya cha Shilingi 5,052/= kwa siku ambacho kimetangazwa juzi tu; maana yake ni umasikini wa kukosa *kukosa mahitaji ya kawaida*, ya lazima ya kila siku (*basic needs*). Watu wengi wanakuwa wamekosa mahitaji yao ya msingi kama vile malazi ya uhakika, chakula cha uhakika na mavazi yenye heshima na staha inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda katika hizo changamoto tatu zilizopo hapo, nijikite zaidi kwenye changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi. Katika zama tunazoishi kumekuwa na ongezeko kubwa sana la idadi kubwa sana ya watu katika Taifa letu, na juzi zimetangazwa *figures* mbalimbali za Sensa ya Watu na Makazi na ukizitazama kwa jicho la kisayansi utaona kwamba idadi ya watu, miaka thelathini ijayo itakuwa ime-double. Kama sensa safari hii inatangaza watu milioni 61, maana yake tutakuwa tumefika watu zaidi ya milioni 120 ifikapo mwaka takribani 2050 na kitu au 2060 huko. Hili lina-*pose a very huge challenge* kwa uongozi wa sasa na uongozi unaokuja kuhusiana na uhakika wa maisha yetu hapa nchini na duniani kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za hivi karibuni nimeona kuna *clip* moja inazunguka kwenye mitandao ya kijamii ya watu ambao wanaendesha bodaboda wakiwa wamepakia mkaa. Ukiona zile bodaboda na kulikuwa kuna mtu alikuwa anaongea kwenye hiyo *clip* akizungumzia suala la mkaa akisema Ruvu hiyo, Ruvu hiyo. Pale unajifunza mambo kadhaa yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ni kwamba tuna changamoto kubwa ya nishati ukanda wa

8 NOVEMBA, 2022

Pwani. Nami nikaamua kwenda kutazama *figures* kwa sababu nakumbuka niliwahi kufanya kazi katika Wizara ya Maliasili na Utalii, na niliwahi ku- *commission* utafiti wa mahitaji ya mkaa hapa nchini. Nilipoenda kutazama *figure* zangu, kwenye ripoti ambayo niliwahi kuletewa huko nyuma katika mapito yangu, nilishtuka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam peke yake, kwanza katika nchi kwa ujumla wake kwa mwaka mzima tunatumia tani 1,895,248 za mkaa na asilimia 50 ya tani hizi za mkaa zinatumiwa katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa sababu wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kwa zaidi ya asilimia 95 wanatumia mkaa. Hii ni biashara kubwa sana ambayo sidhani kama tunaitilia maanani sana kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya mkaa kwa utafiti wa mwaka 2014 uliofanywa na Benki ya Dunia kwa hapa Tanzania ilionesha ni biashara ya Shilingi bilioni moja ya Kimarekani. Kwa utafiti niliou-*commission* mimi nikiwa Waziri kipindi hicho, kwa mwaka volume ya biashara ya mkaa ilikuwa ni ya shilingi trilioni 2.5 za Kitanzania. Kama asilimia 50 ya biashara hii iko kwenye Jiji la Dar es Salaam maana yake unazungumzia pesa inayozunguka zaidi ya shilingi trilioni 1.2. Kwa wakati ule tulikadiria kwamba kutokana na kiwango cha kukusanya mapato cha shilingi 250 kwa kila kilo ya mkaa inayokusanywa na Serikali kwa maana ya Wakala wa Huduma na Misititu, tungeweza kukusanya shilingi bilioni 575 kama biashara ya mkaa ikiwa *properly regulated*, ikasimamiwa vizuri, badala ya *check points* zilizopo sasa hivi ambazo ni kama tu zinahalalisha tu watu ambao tayari wameshafanya uharibifu kwenye misitu, kama ikiwa *regulated*, namna nzuri ya kuvuna na kukusanya mapato tunaweza

8 NOVEMBA, 2022

tukatumia fedha hizi kwenda kuwekeza kwenye uzalishaji wa mkaa huu wa *clean energy* kama vile *briquettes*, hizi tofali zinazotengenezwa kwa pumba za mpunga na vitu vingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaweza kutumia pesa hizi kwenda kuwekeza kwenye utumiaji endelevu wa misitu (*sustainable use of our forest resources*), lakini bahati mbaya sana tunakusanya chini ya Shilingi bilioni 30 kwa mwaka kutokana na mkaa. Hilo lilikuwa ni jambo langu la kwanza ambalo nilipenda kulizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilipenda kuzungumzia suala la kuanzishwa kwa mfuko wa kuhifadhi bei za mazao; sijui kama nimetafsiri Kiswahili kwa usahihi, lakini nazungumzia *Price Stabilization Fund*; kwamba kama Taifa tunahitaji kuwa na mfuko maalum wa kudhibiti bei za mazao hapa nchini. Pia mfuko huu utatuwezesha kununua chakula pindi chakula kipo chini kwa uhakika zaidi na kukigawa kwa wananchi kipindi ambapo chakula kimepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema pale awali kwamba changamoto kubwa hapa nchini kwetu kwa watu wetu wa kawaida ni chakula na mahitaji ya msingi tu, wala watu wetu hawataki mambo makubwa sana. Sasa kama tutaweka utaratibu mzuri wa chakula, na pia ili tuwe na utaratibu mzuri wa kuhifadhi chakula, maana yake tunahitaji utaratibu mzuri wa kuhifadhi mazingira, kwa sababu watu wetu wanalima kwa jembe la mkono na wanategemea zaidi kilimo cha mvua za Mwenyezi Mungu. Sasa kama hakuna mvua kutokana na uharibifu wa mazingira, maana yake hatutaweza kupata chakula cha kutosha katika Taifa letu.

8 NOVEMBA, 2022

Kwa hiyo, nilikuwa napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango katika mapendekezo yake aliyoyaleta atazame sana eneo la mabadiliko ya tabia nchi, na eneo la kuanzisha *Price Stabilization Fund* ili bei za mazao zikishuka, mfuko unaweka pale, wakulima wanapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kwenye korosho tuliwapa matumaini wakulima wa korosho, bei zikapanda mpaka zikafika zaidi ya shilingi 2,600. Kawaulize, leo wanauza korosho yao kwa shilingi ngapi? Ni chini ya shilingi 2,000. Kwenye pamba tuliwapa matumaini wakulima wa pamba na wafanyabiashara wa pamba kwamba pamba inakwenda mpaka shilingi 2,000; kawaulize mwaka huu wameuza pamba yao kwa Shilingi ngapi; na kama wanunuzi walikuwepo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ambacho kitaweza kututoa kwenye hii changamoto ya kutatua matatizo ya wakulima kila mwaka ni kuwa na mfuko...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, ahsante kengele ya pili.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kapufi, Mheshimiwa Engin Samweli na Mheshimiwa Cherehani wajiandae.

8 NOVEMBA, 2022

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami nitajikita katika maeneo yafuatayo: Awali ya yote pamoja na kutoa pole kwa Watanzania wenzetu, lakini inanirudisha kwenye Mpango wa suala zima la usimamizi wa maafa. Kuna kifungu cha 35 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439, kuanzishwa kwa Mfuko wa Dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuamini kwamba wenzetu katika suala zima la mipango ni kweli mengine yanakuja kwa mapenzi ya Mungu na vitu vingine vya namna hiyo. Hata hivyo ni vizuri tukajua kwamba maafa yapo na kwa misingi hiyo kama nchi tusipotengeneza mazingira maana yake inapofika sehemu Mtanzania anapoteza maisha kwa sababu tu hakuna gari ya kunyanyua kitu kizito anapata tabu. Kwa hiyo naendelea kuomba eneo hilo la usimamizi wa maafa tufike sehemu kama nchi mipango yetu tujielekeze huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa uchambuzi wa Kamati. Kamati imesema kwamba sekta zote zilizokua kwa kiasi kikubwa zimetokana na Serikali kuwekeza zaidi katika sekta hizo. Kwa mfano; Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Viwanda, Utalii na Uvuvi wa Bahari Kuu, lakini natamani kuongeza na madini. Hata hivyo, tumeambiwa Mfumuko wa bei, kupanda kwa bidhaa, mafuta ya kula, mbolea na *petrol*, UVIKO-19, Vita vya Urusi na Ukraine vimesababisha hilo. Hata hivyo, bado Kamati imetukumbusha kwamba haya tuyatumie kama fursa.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia mtaalam mmoja wa Singapore, alikuwa anaeleza mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtaalam huyu alikuwa anasema nchi yao ya Singapore ni ndogo lakini wamewekeza katika size ya ngumi wakiutaja ubongo. Sehemu kubwa ya bajetii yao wameipeleka kwenye elimu kuhakikisha watu wanasoma. Baada ya kusoma kwa watu wao, wanaamini kwamba kwanza nchi ni ndogo, hawana eneo la kilimo, *natural resources* ni haba na kwa sura hiyo wameamua kuwekeza kwenye elimu ili sayansi na teknolojia yawe ni matunda na wamefika mahali ambapo umaskini wa nchi yao umegeuka kuwa ni utajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najjuliza nini? Kwa nchi kubwa kama Tanzania, hivi siku zote tunazungumza hapa na hata mimi nilishawahi kusema hapa, nchi kubwa kama hii mipango yetu hata tu uwepo wetu hapa tulipo, kijiografia, hivi mipango hiyo haituelekezi tuitumie kama ni fursa? Nchi zote zinazotuzunguka watu wanatutamani hapa tulipo, lakini niseme tu hata katika ardhi, yote yanayozungumzwa *whether* ni njaa ama ni nini bila matumizi bora ya ardhi hatutoacha kushuhudia ugomvi wa wakulima, wafugaji na watu wengine. Mipango yetu inasemaje katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kurudia kama siku nyingine unavyoniambia *Mr. Kapufi declare* wewe ni nani? Mimi ni mchimbaji mdogo wa madini. Naomba nijikite katika eneo hilo la uchimbaji mdogo wa madini. Amezungumza Mheshimiwa mmoja hapa akitaja nchi kwa upana wake na idadi ya madini.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sijui tunapata tabu, mtu mmoja aliniambia ukienda sehemu halafu ukamwagiwa vitu vingi, kwa wakati mmoja unashindwa kujua uchukue hiki au hiki au hiki. Sasa nchi nzuri Tanzania madini yapo ya kutosha na tumeambiwa idadi hiyo nyingine, nataka nijikite tu kwenye madini ya dhahabu. Leo mipango yetu niseme angalau kwenye kilimo Serikali inatoa ruzuku, vipi kwa wachimbaji hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie hivi, amini usiamini dhahabu pekee inaweza ikafanya vitu vingine vikasubiri kwenye nchi hii. Pia achilia madini hayo mengine, nina mfano hai, kama kweli tumewawezesha vizuri watu wa GST, kwa maana ya tafiti zao, mtu unajua kabisa kwamba mashapo yaliyopo hapa, kwa maana kwamba, katika ekari moja pale chini ya ardhi labda huyu mtu ana kilo tatu, nne, tano au sita za dhahabu. Sasa utafiti utuelekeze tunaitoaje dhahabu hapo chini ili igeuke kuwa fedha? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sura hiyo hatutawafanya wachimbaji waonekana wanashiriki ushirikina, kwa sababu tafiti zinaonyesha kwamba hapa chini kuna madini kiasi hicho na labda ni *three grams per ton or five grams per ton*, tengeneza mazingira tani kadhaa ziweze kuzalisha kiasi kadhaa cha kilo za dhahabu. Kwa sura hiyo, kwa kufanya kisayansi kama hivyo, tunaitoa nchi hii na itafika mbali. Pia niendeleo kusema, bado naamini hatujafanya vya kutosha na wenzetu wa fedha mipango yetu iende huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine zao lao ni moja uvuvi tu na wako mbali. Sasa Tanzania ukija kwenye

8 NOVEMBA, 2022

uvuvi tuko vizuri, kwenye madini tuko vizuri na leo sioni sababu ya nchi kulalamika kuhusu kilimo. Niliwahi kusema hapa na Mheshimiwa Kingu akaniunga mkono, nilisema je, tuna mpango wa mtandao wa maji wa nchi hii? Leo ukitengeneza mtandao wa maji hauzungumzii njaa, hauzungumzii sijui shida ya maji. Je, hatujikiti huko jamani? Nilizungumza ndani ya Bunge hili, nchi kubwa kama China unaunganishwa kwa mtandao wa maji kwa vyanzo vyao tu, labda kutoka kaskazini kwenda kusini, kutoka mashariki kwenda magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la maji tu, mipango ikijielekeza na kwa kutumia vyanzo vyetu tulivyonavyo, tuiweke kwenye mipango, hapa naomba pia twende mbali zaidi. Nimeona tumeambiwa kuhusu ununuzi wa vifaa vya kuchimba mabwawa na kuchimba visima. Bado Serikali wasiache kwenda kwenye tafiti. Sehemu nyingine duniani baadhi ya miji imeanza kuzama kutokana na uchimbaji wa maji haya ya visima. Kwa hiyo ningeweza kuishauri nchi yangu, sikatai, visima tuchimbe lakini tuisahau tafiti ili kuepuka hilo. Hata hivyo sehemu kubwa ya kuweza kupata maji ni kuinga maji ya mvua yanayopotea kwenda baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie kwa maana ya kufungamanisha fursa, leo unaweza ukakinga maji hayo na ukafanya shughuli zifuatazo: Utalima, kwa maana ya kumwagilia; Utafuga kwa maana ya samaki hapo; na Utafanya utalii kwa sababu ndani ya maji hayo hayo, watu wanaweza kufanya utalii ikiwemo *man-made lakes and whatever*, watu wanafanya mpaka utalii. Kwa hiyo tuyaangalie hayo...

8 NOVEMBA, 2022

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hata nchi zinazoendelea wanatumia maji ya bahari, wanaya-*purify* na wanayarudisha kuyatumia. Kwa hiyo hata nchi yetu ianze kufikiri namna ambavyo tunaweza kwenda kwenye utaratibu wa kutumia maji ya bahari kwa sababu hata kina cha bahari kinaongezeka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nusrat wana-*purify* au wanafanya *desalination*?

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi ni Mswahili, naomba nitumie Kiswahili, wanayaondoa chumvi, wanayasafisha, wanayaondoa chumvi, yanatumika.

MWENYEKITI: Kwa hiyo ni *desalination*. Haya Mheshimiwa Kapufi.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea taarifa, lakini nimsaidie tu dada yangu hatujafika mahali pa kutumia maji ya bahari kwa vyanzo tulivyonavyo nchi hii. Maziwa yote tuliyonayo nenda Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, ziwa Nyasa, mito mikubwa mpaka tukaikute Bahari ya Hindi ni baadaye sana. Kwa hiyo sasa hivi nchi ijielekeze kwenye vyanzo vyote vikubwa tulivyonavyo.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, nafahamu kila mmoja anasema kilimo ni uti wa mgongo. Siamini sana kwa watu wengi kushiriki kilimo halafu ni kilimo kisicho na tija. Bora wachache wakafanye kilimo walishe wengine, wengine wakavue, wengine wakachimbe na kadhalika. Nchi za wenzetu *percent* kidogo ya watu wanaoshiriki kilimo wanalisha *the rest of the world*. Sasa sisi asilimia kubwa lakini hatujilishi hata wenyewe, kuna kitu cha kufanya hapo, lazima turudi tupaangalie hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sio muumini wa nchi nzima kulima korosho au kulima sijui kama nini, mimi huko sipo. Tugawe kanda za kilimo, haiwezekani wote tukawe wakulima wa parachichi au korosho. Kwa hiyo mipango yetu nayo ijielekeze huko isije ikawa Mtwara walipata bei nzuri ya korosho, basi nchi nzima tunataka tulime korosho. Ikawa sijui Rungwe walipata bei nzuri ya parachichi, wote tunataka, hapana. Tugawane Kanda za kilimo, lakini kila watu wafanye kwa tafiti na mambo mengine ya namna hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado narudia kusema, kwa kupitia madini peke yake, mipango ijielekeze huko na kama leo kwa mfano tunatoa ruzuku za kilimo, wachimbaji hawa wadogo wapewe ruzuku. Naamini kwa kufanya hivyo, Marehemu Rais John Magufuli alituita wachimbaji wote, akasema nataka mniambie mnafanayaje kuitoa nchi hapa ilipo kwa kupitia madini? Hata hivyo, watu waliuza mawazo yake, kwa hiyo hata kwa mipango yetu hebu tuwashirikishe hawa, kwa sababu kuna wakati ukisikia kuna *gold rush*, mfumuko wa dhahabu *somewhere*, ni kazi ya wachimbaji wadogo. Sasa kama mchimbaji mdogo ndiye anaweza kugundua

8 NOVEMBA, 2022

dhahabu shambani, anagundua akiwa anachimba kisima, watafiti wetu wako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende mbali zaidi, kwa kupitia taarifa zile, kwa mfano kama ni GST wangepanya vizuri, taarifa ya kitafiti isimame, ni fedha. Leo kuna watu wengine kwa kuuza tu taarifa za kitafiti wanasababisha watu wengine wawe matajiri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, kengele ya pili.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango mzuri. Kama ulivyosema Mheshimiwa Kapufi kwenye kilimo kuna sera moja tu ya kilimo. Tu-*diversify* sera, kila zone iwe na sera yake, tutaona na Mheshimiwa Bashe hiki kitu unakiweza vizuri, tunakutegemea wewe Mheshimiwa Bashe. Peleka Sera ya kilimo kanda ya juu, kusini, tukiwa na sera moja ya kilimo *it won't work*.

Mheshimiwa *Engineer* Samwel, wajiandae Mheshimiwa Cherehani na Mheshimiwa Mageni.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mpango wetu wa Taifa wa Mwaka 2023/2024. Kwenye wasilisho ambalo Mheshimiwa Waziri amelifanya ameanisha sekta ambazo zinafanya vizuri. Kati ya sekta tano ambazo zinafanya kazi vizuri ameongelea suala la

8 NOVEMBA, 2022

Sekta za Maji, Fedha na Bima, Uchimbaji wa Madini na Mawe na Sekta ya Huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye sekta zetu za msingi za uzalishaji hapa hazipo. Ukigusa kwenye upande ambao unatusumbua kwenye suala la mfumuko wa bei inayoongoza ni sehemu ya vyakula na viinywaji, ni asilimia 7.8. inamaanisha nini? Vyakula hivi vingi tunaweza kulima wenyewe. Kwa mwaka uliopita haukuwa mzuri kwa sababu tunategemea mvua za Mwenyezi Mungu. Mheshimiwa Kwagirwa aliongelea kidogo suala la kujaribu kwenda kupunguza *tension* ya gharama za maisha ya wananchi wetu huko vijijini kwa vyakula ambavyo viko kwenye maghala yetu ili vipelekwe kwa wananchi ili kupunguza mfumuko wa bei kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza ni muhimu sana kwa sababu kama mfumuko ni mkubwa kiasi hiki inaathiri uchumi wetu, Serikali ichukue hatua sasa bila kuchelewa. Kilimo kinachangia asilimia 26 kwenye pato la Taifa, lakini imeajiri zaidi ya Watanzania asilimia 65, ni watu wengi. Ili tuweze kulikwamua Taifa hili lazima eneo hilo tuliangalie kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza bajeti ya kilimo kutoka Shilingi bilioni 294 mpaka Shilingi bilioni 954. Naamini kwamba changamoto hii ya ukuaji wa uchumi na *intervention* hii itakayofanyika katika kilimo itaenda kutusaidia. Tunamwamini Mheshimiwa Bashe kwa umahiri wake na hatua anazozichukua. Kwa sasa tunaenda kwenye msimu wa kilimo, wakulima wengi wanalia kwenye suala la pembejeo, masuala ya mbegu

8 NOVEMBA, 2022

bora, naomba eneo hili tulisimamie vizuri. Wale wataalam wetu wa kilimo watoke maofisini sasa waende wakakae na wakulima kuona namna ya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa tuliyonayo ni mbegu, natoa mfano kwetu Hanang tunaotegemea sana kilimo cha shayiri na ngano, mpaka sasa haujawekwa utaratibu mzuri wa kupata mbegu bora ya ngano. Hata hivyo, mara nyingi kila msimu unapoanza tunahangaika sana na mbegu ya shayiri ambayo mara nyingi wakulima wetu wamekuwa wakiingia mikataba na makampuni yanayozalisha vinywaji aina ya bia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba eneo hili lisimamiwe vizuri. Fedha zilizowekwa huku ni nyingi hizi fedha zilete tija kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo ili wakulima waweze kuzalisha ni muhimu sana kuwawezesha wakulima kwa mitaji. Benki yetu ya kilimo iweze kuwakopesha wakulima. Kwa sasa wanatoa mikopo lakini masharti bado ni magumu sana. Tumeanzisha Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS), nyingi ambazo zimeanzishwa lakini wakitaka kuanzisha mikataba ili waweze kukopa kwenye hizi benki bado kuna kitu wanaita mkataba wa utatu. Lazima kuwe na mkataba baina ya benki, wakulima wenyewe kupitia AMCOS zao na wale ambao watakuja kununua bidhaa hizo baada ya kuzalishwa. Serikali itengeneze mfumo wa hizi AMCOS zetu kuaminika bila kuhitaji nani atanunua bidhaa baada ya hapo, vinginevyo isaidie wakulima hawa kupata masoko ya mazao watakayozalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie eneo la mifugo. Wafugaji kwenye nchi yetu wengi wamekuwa kama wakimbizi, kila sehemu wanawindwa, kila sehemu kuna

8 NOVEMBA, 2022

mwingiliano baina ya wakulima na wafugaji na kila sehemu wanawindwa. Katika kila sehemu wameonekana kama ni watu wakorofi, mtu yeyote bila kumpa elimu iliyostahiki ama kumtengea nafasi stahiki kwenye jamii lazima ataonekana mkorofi kwa sababu ataitafuta nafasi yake kwa namna anavyoona yeye. Ni muhimu sana kwa nchi hii, kuwatengenezea wafugaji utaratibu mahususi ili wafuge na hatimaye tuwape elimu waweze ku-*transform* mifugo yao kuwa ya kisasa na hatimaye wafuge ufugaji wenye tija kwao...

MHE. ZUBEIRI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. ZUBEIRI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nathamini sana mchango wa mchangiaji anayechangia, amegusa sehemu anasema kwamba wafugaji kwenye nchi hii wanaonekana ni wakorofi, lakini sio tu kwamba wanaonekana ni wakorofi, *nature* ya wafugaji ni wakorofi na wao kuu kwao ni jambo la kawaida.

MWENYEKITI: Hiyo sio taarifa. Endelea na mchango wako. (*Makofi*)

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba niendeleo. Nilichokuwa namaanisha wafugaji lazima tuwatengee eneo lao na tutengeneze mazingira, tuna mifugo mingi nchi hii, tuone namna gani inaweza kutuletea tija. Haileti maana yoyote, tuna ng'ombe wengi, mbuzi wengi, kondoo na kuku wengi, lakini bado tuagize nyama kutoka

8 NOVEMBA, 2022

nje. Tuwajengee uwezo tutengeneze namna ya kuchakata mazao yanayotokana na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la ardhi; kilimo na mifugo yote inahitaji ardhi. Nimesema kabla kwenye Bunge hili kwamba ni muhimu ardhi yetu tuipange vizuri ili kila mtu aweze kupata sehemu ambako ataendeshea shughuli zake. Tupate ardhi kwa ajili ya kilimo, mifugo na shughuli nyingine ikiwemo viwanda. Ni muhimu sana kuipanga ardhi yetu vizuri na tutaondoa mwingiliano na migogoro mingine ambayo inajitokeza kati ya wakulima na wafugaji na jamii nyingine. Tukiipanga ardhi yetu vizuri, tunaweza tukawa kwenye baadhi ya vijiji tukatengeneza *ranches* ndogondogo sio lazima tuwe na *ranches* kubwa ili tuweze kuwaweka wakulima wetu vizuri na hatimaye tuwaweke wafugaji vizuri ili shughuli zao ziweze kuleta tija. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ardhi tukiitumia vizuri kwenye jamii yetu, mwenye ardhi anamkodisha asiye na ardhi ili alime, mwenye ardhi anamkodisha mfugaji ili aweze kulisha mifugo yake lakini pia kuna ile biashara ya kuuziana viwanja na kuuziana mashamba. Tukiirasimisha ardhi yetu yote, kwenye eneo hilo Serikali inaweza kutengeneza mapato. Tukihusisha hata Serikali yetu mpaka hata ngazi ya kijiji, zile shughuli zinazofanyika kule tukaona namna ambavyo tunaweza kupata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana ardhi tukiipanga na kuitumia vizuri italeti tija kubwa kwenye shughuli zetu za ukuaji wa uchumi. Hata hivyo, niombe kwenye eneo hili kuna ardhi ambayo tayari imeshapangwa, ardhi ambayo imelekezwa kwa ajili ya *ranches* kwa ajili ya mifugo, vile vile mashamba

8 NOVEMBA, 2022

makubwa ambayo yapo kwa ajili ya kilimo. Maeneo hayo yatumike kimkakati ili yaweze kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano wa ardhi ambayo iko ndani ya Jimbo langu la Hanang. Ardhi hii tuliwapa wawekezaji zaidi ya ekari 43,000, zaidi ya miaka 18 hatuoni tija sisi kama Wanahanang na Watanzania hawaoni tija yoyote.

Mheshimiwa Spika, maeneo kama haya nchi hii ni mengi, ninachoomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo nimekuwa nikiongea na wewe mara kwa mara nakushukuru kwa ushirikiano unaonipa. Ninachoomba zile kazi ambazo umeshaanza ya kutwaa ardhi ile ambayo haitumiki, kamilisha Ndugu yangu ili Wananchi wa Hanang' waweze kufaidi ardhi ambayo iko kwenye maeneo yao, lakini ifanywe kwa nchi nzima ili ardhi zetu zilizolala ziweze kutumika kwa ajili ya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kwenye upande wa utekelezaji wa miradi, ukuaji wetu wa uchumi inanyoongoza ni sekta ya maji lakini tunayo miradi mingi ya maji. Nashukuru sana Mheshimiwa Rais ametenga fedha kwenye eneo hilo, lakini kuna ucheleweshaji mkubwa wa utekelezaji wa miradi. Ukichelewesha mradi maana yake huduma zile zilozotarajiwa zinachelewa, maendeleo yaliyotarajiwa kwa wananchi yanachelewa na inawezekana hiyo kazi tumewapa Wakandarasi tukiamini kwamba hiyo kazi wataifanya vizuri, tunaomba eneo hilo lisimamiwe kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante, sasa namwita Mheshimiwa Cherehani ajiandae Mheshimiwa Mageni.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na Mheshimiwa Naibu Spika wetu. Kwanza nikumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Dunia kwa uhai na niendeleo kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa fedha nyingi ambazo anatupa hasa kwenye Majimbo yetu. Pia, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Kassim kwa kazi nzuri aliyoifanya juzi kukimbia na kuwahi kwa wahanga wenzetu waliopata tatizo pale Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninampongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kutoa mapendekezo kwa kijana wetu Majaliwa aliyeokoa wananchi wenzetu ya kwenda kwenye mafunzo ya Kijeshi ya Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kidogo kwamba tumekuwa tukiwapa *support* vijana hasa wanapo - *support* kwenye matukio mazito kama hayo, ninaiomba Wizara ya Mambo ya Ndani iendeleo kutoa mafunzo kwa wavuvi wote nchini hasa walioko kwenye bahari zetu ili wajue namna nzuri ya kuokoa hasa katika kipindi kigumu cha majanga kwenye bahari, mito na maziwa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye hoja yangu, naendeleo ku-declare interest yangu kwenye suala la kilimo. Kilimo chetu bado kinategemea mvua. Mvua leo hii tunakaribia miaka miwili na huu ni mwaka wa tatu tunapata mvua chini ya wastani, kitu ambacho ni hatari

8 NOVEMBA, 2022

sana kwenye uchumi wa Taifa letu. Kwenye taarifa ya Waziri wa fedha Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kwanza nimpongeze kwa Bajeti nzuri aliyotupa kwenye kilimo kutoka Bilioni 254 sasa wakulima tumepata kwa mara ya kwanza toka uhuru Bilioni 90, na pointi, hongera sana, sisi kazi yetu tuendeleo kukuombea sana kwa Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa ambayo mimi najikita ni kwenye Kilimo cha Umwagiliaji. Kuna mradi mkubwa sana wa maji kwenye nchi hii wa Ziwa Victoria. Mradi huu unatoka katika Mkoa wa Mwanza eneo la Iherere lakini bomba hili limepita zaidi ya kilometa 245 kwenda Tabora Mjini. Bomba hili linapita Solwa, Misugwi, Kahama, limeenda Shinyanga Mjini, limeenda Kishapu. Sasa hivi limeenda Nzega, Tabora na Igunga lakini tuulizane, bomba hili kote linakopita linapita kwenye mashamba ya wananchi ya wakulima wetu ambao wanategemea mvua, Serikali na Wizara yetu ya Kilimo pamoja na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na Wizara yetu ya Kilimo pamoja na Wizara ya Maji wanashindwaje kukaa pamoja kwenye maeneo ambako linapita bomba wakachimba Mabwawa makubwa ya maji wakachepusha maji kupitia kwenye bomba hili. Wakulima wetu walioko Jirani na bomba hili waendeshe kilimo cha umwagiliaji. Leo hii niseme tu hata kwa Ndugu yangu Waziri wa Kilimo pale bomba linapita kwenye barabara nzuri kwenye mbuga ya wakulima wanaolima mpunga lakini ukipita pale unashuhudia kabisa wakulima wa mpunga unakauka hakuna maji, lakini pale limepita bomba kubwa la maji. Kwa nini wananchi hawa wasichimbiwe Mabwawa makubwa ili maji ya umwagiliaji

8 NOVEMBA, 2022

waweze kulima kiangazi, waweze kulima kipindi chochote, leo hii wanategemea mvua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye mpango wako huu hatujaona kujikita kwenye mradi mkubwa wa Mabwawa ya umwagiliaji, maji haya ni mengi sana, lakini wananchi hawa wanaopelekewa maji haya ya kunywa wakati mwingine wanashindwa kulipia *bill* kwa sababu....

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependa mchango wa Mheshimiwa Cherehani jirani yangu. Wiki iliyopita nafikiri siku tatu zilizopita, nilichangia kuhusu *design* ya miradi ya kimkakati katika nchi yetu. Hapa nauona msisitizo mwingine kwamba tunapo-*design* miradi yetu tuiangalie miradi *strategically and comprehensively* ili kutibu matatizo mengi zaidi kuliko kutibu tatizo moja. Kwa hivyo tatizo letu la kukosa mvua na kupungua kwa chakula lingeweza kutatuliwa na mradi wa kupeleka maji kutoka Ziwa Victoria, kwa kuweka hata mabomba mawili moja ya maji ambayo yako *treated* na moja la maji ambayo hayako *treated*. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Doktari. Mheshimiwa Cherehani

8 NOVEMBA, 2022

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante taarifa hii naipokea kwa sababu kweli maeneo haya hata kama ni Kamati ya Wizara ya Maji itakapotembelea maeneo haya nenda pale Solwa kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Ahmed, wananchi wale unakuta hata bwawa la kunyweshea mifugo yao hakuna, lakini bomba la maji limepita, nenda pale Kishapu, hakuna hata eneo la kunyweshea, zao la pamba linapokosa mvua linazidi kupukutika na kushuka uzalishaji lakini hakuna bwawa lililochimbwa kwa ajili ya kuchepusha maji haya wananchi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda pale Msalala kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Kassim Idd hakuna Bwawa lolote lililochimbwa kwa ajili ya kunyweshea maji, leo ninaenda Igunga kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Ngassa eneo hili lote lilitakiwa liwe na maji, mabwawa yachimbwe yajazwe maji, lakini leo hii hata kwenye tumbaku ambako mwaka huu tuna uzalishaji wa zaidi ya tani 140,000, Serikali na wakulima wetu wanaelekea kupata zaidi ya Bilioni 600 lakini hakuna mabwawa, sasa mbegu zinakauka lakini angalia fedha zinazolingia. Mimi ningeendelea kuiomba Serikali mahali ambako tunakoeleza uzalishaji mkubwa waweke nguvu kuhakikisha Taifa linapata mapato makubwa tuweze kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutamsaidiaje Mheshimiwa Rais? Mheshimiwa Rais anatutafutia fedha, anatupa fedha nyingi lakini fedha nyingi tunashindwaje kuzipeleka mahali ambako tunaweza tukapata fedha? *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mwananchi tu wa kawaida leo anashindwa kulipia *bill* ya maji kwa sababu hana vyanzo vya kuweza kupata mapato. Madhara yake pamoja na kumpelekea maji ya Ziwa Victoria anaamua kwenda kutafuta maji ya kisima lakini tungempelekea bwawa akalima bustani yake, akalima mahindi yake vizuri, akalima mpunga wake vizuri, tayari pale atauza kwa muda wowote halafu ataenda kulipia *bill* zake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye tumbaku tunatarajia kuzalisha tumbaku nyingi sana mwaka huu, lakini tunayo changamoto moja na bahati nzuri nimemwona Waziri wangu wa Kilimo na Naibu wako hapa. Tuna mfumo wa makundi ya watu kumi kwenye sekta ya tumbaku. Makundi haya yanafaidisha sana wakulima wazembe lakini pia wakulima waliopo *serious* na kilimo wanaenda kudumbukia, kwa sababu makundi ya watu kumi mpaka walipe deni lao ndipo waweze kulipwa fedha na wengine. Sasa unakuta kwenye kikundi cha watu kumi kuna wakulima watano wamelaza deni lao. Sasa wanaposhindwa kulipa hawa watano inabidi wawalipie madeni yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwaenyekiti, kwenye Chama cha Ushirika chenye watu 20 watu 15 wamelaza madeni chama kimekufa na hawawezi kukopesheka. Mimi niendeleo kushauri kwenye eneo hili, kwa sababu Serikali yetu iko makini na nampongeza Mheshimiwa Waziri yuko vizuri. Tungeomba sasa wakulima wenyewe mmoja mmoja uje utaratibu mzuri waweze kukopeshwa wenyewe kulingana na dhamana zao ili tuweze kuongeza uchumi kwenye maeneo yetu mbalimbali na wakulima waweze kupata mapato. (Makofi)

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuende kwenye Bodi ya Tumbaku. Bodi ya Tumbaku ndiyo inayosimamia uzalishaji wote huu. Uzalishaji ambao ni Mabilioni ya fedha yanaenda kwenye Serikali yetu lakini niombe waendeleo kuitolea fedha. Bodi ya Tumbaku bado ni changamoto, niseme tu hata Mkurugenzi wa Bodi hii ya Tumbaku hana gari. Anasubiria gari inayoenda *field* ndiyo aje afanye shughuki zake. Niombe bodi hizi za mazao ambazo ziko kwenye mazao ya kimkakati ziweze kupewa fedha za kutosha kuweza kuwa hudumia wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Mageni.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hii nafasi uliyonipatia. Awali ninaipongeza Wizara ya Fedha kwa huu mpango ambao wameuleta hapa, ni mpango ambao unaonesha matumaini kwenye uchumi wetu lakini kwa kuutazama na mimi nimeona walau niongeze mchango wangu ili kuboresha katika maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu na wachangiaji wa mwanzo wamechangia na kuzungumza kuhusu umuhimu wa Sekta ya Kilimo. Sekta ya kilimo, Watanzania tumekuwa tukisema ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu. Sekta ya Kilimo kwa taarifa ambazo zipo na zimeandikwa kwenye taarifa ya Waziri wakati anatoa mpango ni kwamba bajeti imepanda kutoka

8 NOVEMBA, 2022

bilioni 254, mpaka zaidi ya bilioni 900. Sekta hii inatoa ajira asilimia 65 na zaidi ya Watanzania. Kwa hiyo sekta ya kilimo ni sekta ya muhimu sana na kama tunataka kutoka hapa tulipo twende pazuri zaidi ni lazima tuongeze nguvu kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo inayo maeneo mengi ya msingi lakini nitazungumzia eneo moja la usafirishaji wa mazao ya kilimo. Mazao yetu ya kilimo mengi yanatoka maeneo ya vijijini, wakulima wetu wanapolima mazao yao wanatumia gharama kubwa sana kuyasafirisha. Jambo ambalo limekuwa likisababisha bei ya mkulima kuwa chini lakini bei ya mazao kwa mlaji inakuwa juu. Naishauri Serikali kwamba iwekeze zaidi kwenye kuhakisha barabara zilizoko vijijini ambako ndiko kwa wakulima wenyewe zinaboreshwa ili ziweze ku-*accommodate* usafirishaji wa mazao haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikatoa mfano kwa sababu mimi pia ni Mbunge ambaye ninatoka kwenye Jimbo ambalo asilimia kubwa ni wakulima na wafugaji, Jimbo la Sumve. Katika Jimbo zima la Sumve hakuna barabara ambayo inaruhusu gari la zaidi ya tani kumi kupita. Ina maana ili ubebe mazao ya pamba kwa mujibu wa sheria za barabara zetu zilivyo unatakiwa utumie *canter* au magari mengine madogo madogo ukishatoka Sumve ndiyo utafute magari makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa utaratibu huu wa kuwa na barabara mbovu kwenye maeneo ya uzalishaji hatumsaidii mkulima, lazima Wizara ndugu yangu Mwigulu Nchemba Waziri tufikirie hili jambo kwa undani wake. Ndiyo maana kila muda tunaposimama tuataka

8 NOVEMBA, 2022

kushauri kuhusu maendeleo ya nchi hii, tunaotoka huko vijijini tunalia na miundombinu ya usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani umefika wakati sasa Serikali ichukue hatua kwa ajili ya kukuza uchumi wetu. Tunapata taabu sana kwa mazao yetu kufika Mjini yakiwa na bei kubwa na wakulima wetu kupata bei ndogo kwa sababu ya matatizo ya usafiri, halafu tunasema tunaboresha barabara za mijini wakati sisi wa vijijini kila siku tunazungumzia barabara zetu. Hili jambo nilitaka Serikali ilianganalie kwa jicho la pili kwa ajili ya kukuza uchumi wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa sana hapa na michango iliyopita ni kuhusu tunapanga Bajeti hapa, tunapeleka pesa kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya pesa zile kutumika kuleta maendeleo kule lakini pesa zile zimekuwa hazifanyi kazi iliyopangwa. Pesa hizo zinafika kule zinapotea mwisho wa siku unakuta Waziri wa Idara kama TAMISEMI, unakuta kazi yake yeye ni kutumbua kushughulika na wezi kutengeneza Tume za kuchunguza na mwisho wa siku badala ya ile pesa kufanya kazi tunahangaika kufunga watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nafikiri tunatakiwa mpango wetu wa maendeleo huu uangalie hilo kwa jicho la pili. Lazima tujiulize kwa nini pesa nyingi zinazopelekwa kwenye Halmashauri zinakwenda zinaibiwa? Kwa nini iko shida kule? Halmashauri mfumo wake ukiuangalia umewekwa vizuri sana kisheria, Halmashauri zinasimamiwa na Mabaraza ya Madiwani, hawa Madiwani kwa mujibu wa sheria ndiyo walinzi wa Halmashauri zetu.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Halmashauri tunapeleka Mabilioni ya pesa halafu kwenye mpango huu tumepanga wale walinzi wetu tunawalipa kiduchu ndiyo walinde hizo pesa. Kila siku tutatengeneza tume tusipofahamu siri ya wizi. Kwenye Halmashauri imefika wakati sasa hivi Madiwani hawafanyi hata ziara, yaani wale Watumishi wanatumia *loophole* ya Madiwani kutokuenda, mipango yetu na nyaraka zetu na maelekezo ya Mawaziri imefika wakati Madiwani wale wanaolinda mali zetu tunazopeleka kule, wanakutana kwenye Kamati kujadili makabrasha makubwa ambayo hawajajua hata hiyo miradi ikoje. Ziara za Madiwani za Kamati, zimefutwa, wanasema ni maelekezo ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafika wakati utendaji kule umekuwa chini, kwa hiyo hawa walinzi wetu hawafanyi kabisa kazi vizuri, kwa hiyo mwisho wa siku ukiwa na walinzi dhaifu wanashirikiana na mwizi kukuibia. Kwa hiyo, kila siku tutakuwa tunapeleka pesa kule, tutakuwa tunakaa hapa tunapanga mabilioni kama hatujaangalia namna gani tunalinda pesa tulizozipeleka kule. Tutaendelea kuwapa kazi Mawaziri ya kutumbua, kazi ya kusimamisha, TAKUKURU kagua, anafika Mheshimiwa Waziri Mkuu kule anakuta yaani miradi mpaka afike Waziri Mkuu ndiyo ionwe wakati huo kuna wasimamizi kule ambao ni Madiwani, nadhani hili jambo tunatakiwa tuliangalie kwa jicho la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yetu itaendelea kuibiwa ni lazima Serikali ije na mpango wa kulinda mali tunazopeleka kwenye Halmashauri. Halmashauri ndiyo chanzo cha maendeleo ya watu wetu. Nadhani hata Wabunge ni mashahidi. Hapa Wizara zinazotembelewa

8 NOVEMBA, 2022

mara nyingi na Wabunge ni TAMISEMI. Sasa TAMISEMI huko ndiko kapu la pesa zinazowahusu wananchi wetu zinaenda kule, huu mpango tunapanga pesa nyingi tunapeleka kule. Sasa kule hakuna walinzi tumeweka watu tu wa kushirikiana na wengine kuiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu unapompa pesa humwekei mlinzi unamshawishi kuziiba ni lazima tuwe na mpango wa kulinda hizi pesa zetu vinginevyo...

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji, ndani ya huu mwaka tu mmoja zipo Halmashauri ambazo zimepokea Nyaraka Mbili tofauti zinazotoka TAMISEMI, juu ya Madiwani. Mwanzo waliongezewa posho zao lakini ikatokea tena waraka ndani ya huu mwaka mmoja wamepunguziwa posho zao. Kwa hiyo naungana kabisa nahoja ya Mheshimiwa, hawa walinzi wetu wanakaa hawaelewi kesho wataamka wako katika hali gani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mageni taarifa.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii naipokea na ninasisitiza ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge Serikali hili jambo tulipeni umuhimu wake ili pesa tunazozipanga na kuzipeleka huko zitumike vizuri. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, mengine andika. Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO- KATIBU MEZANI:

(Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha semina sasa hivi na baada ya kuwakumbusha semina naahirisha Bunge mpaka saa kumi na moja jioni. *(Makofi/Kicheko)*

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirejea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Tukae.

Waheshimiwa kabla hatujaanza kwa upande wa Serikali, mtaona Mawaziri wengi hawapo, kuna kikao maalum ambacho kimeitishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, wanamalizia watakuja, lakini Serikali ipo. Yupo Waziri wa Fedha na *Chief Whip*, kwa hiyo Serikali imeshawakilishwa humu ndani. Katibu.

8 NOVEMBA, 2022

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa asubuhi hatukutaja majina ya jioni lakini, Mheshimiwa Neema upo? Tutaanza na Mheshimiwa Neema, utajiandaa Mheshimiwa Kalogeris, Mheshimiwa Mgalu upo, Mheshimiwa Manyinyi upo. Haya tunaanza na Mheshimiwa Neema.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia jioni hii katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2023/2024. Niseme tu, kabla sijaendelea nilitamani nitumie nafasi hii kuweza kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuweka ruzuku katika mbolea. Ambako tunaona wakulima wengi sasa hivi wana amani. Pia, niweze kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mheshimiwa Waziri Kindamba kwa namna ambavyo amekuwa akiendelea kupambana na wahujumu mbolea ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kuona kwenye mitandao kwamba kule Mkoani Songwe kulikuwa na wahujumu uchumi kupitia mbolea, waliokuwa wanatoa mbolea Tanzania kwenda Malawi. Kwa hiyo sasa hivi imebadilika, kwamba mbolea badala ya kutoka Malawi

8 NOVEMBA, 2022

kuja Tanzania sasa hivi inatoka Tanzania Kwenda Malawi.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nilitaka nijielekeza kwenye kuchangia katika mapendekezo haya ya huu mpango. Kimsingi nitajikita katika maeneo matatu ambayo ni vipaumbele vya mpango huu. Eneo la kwanza, nitaanzia kwenye kuchochea uchumi shindani na shirikishi, ambapo hapa kuna masuala ya usafirishaji, umeme na TEHAMA. Tunafahamu kwamba barabara ya TANZAM imekuwa ni barabara muhimu sana, na barabara hii ndiyo inayosafirisha mizigo mingi kuelekea Nchi za Ukanda wa SADC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiongea hapa mara nyingi, lakini kwa awamu hii ninatamani kuomba Wizara ya Fedha iweze kuweka kipaumbele ujenzi wa barabara hususan kwenye eneo la Mlowo-Tunduma. Kama vile walivyotia kipaumbele kwa eneo la Mbeya waweke kwa Tunduma kwa sababu barabara ile inapata *jam* kubwa sana. Mawaziri ni mashahidi, wamepita kule na wameona, kwamba hali ya pale si nzuri, mizigo mingi inashindwa kufika kwa wakati katika *destiny* pale mpakani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nilishaongelea kwamba barabara ile kutoka Mlo kwenda Tunduma hakuna barabara ya mchepuko ambayo kama barabara hii ikapata tatizo lolote kutakuwa na njia mbadala ya kuweza kufika mpakani. Kwa hiyo, niombe kupitia bajeti hii, waweze kuitazama barabara hii kama ilivyo muhimu. Kama wanavyowekeza kwa upande wa

8 NOVEMBA, 2022

Dar es Salaam wangewezeza Tunduma nadhani tungepunguza changamoto nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuongelea na kuipongeza Kamati ambao wameweza kuona umuhimu wa kuendelea na mchakato wa hii Sheria ya TAZARA. Nilikuwa natamani kusesitiza pia wafanye haraka iwezekanavyo ili kuboresha hii sheria ili uwekezaji katika TAZARA uendeleo na hivyo uweze kuleta tija katika usafirishaji wa mizigo inayoenda huu Ukanda wa SADC. Kwa hiyo, kwa hili niombe pia kwenye bajeti ijayo waipе kipaumbele TAZARA ili iweze kufanya kazi yake kama ambavyo ilikuwa imetarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu ambacho kimekuwepo, na sijajua ni kwa namna gani huu Mpaka wa Tunduma haujapewa kipaumbele. Kama uwekezaji unavyofanyika Dar es Salaam wangeweza kufanya uwekezaji huu Tunduma mimi nina uhakika nchi hii ingeongeza mapato kwa kiwango kikubwa sana. Tunafahamu mizigo mingi inayotoka Dar es Salaam kwa asilimia 70 inapita kuelekea Ukanda wa SADC. Kama tungepajenga Tunduma tukaweka masoko ya Kimataifa pale, tukajenga *dry port* pale tunaamini kabisa mapato ya nchi hii yangeongezeka; na hata kwenye nchi hizo za Ukanda wa SADC wale wenye mitaji midogo wangeweza kulifikia Soko la Tanzania na kwa namna hiyo tungeweza kupata mapato kutoka kwenye hizo nchi za upande wa SADC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Wizara kupitia bajeti hii tunayoielekea, huu mpango wa kuelekea bajeti hii inayokuja, wafanye, ikiwezekana, utafiti kwa Mji wa Tunduma, waangalie ni fursa gani zipo ambazo

8 NOVEMBA, 2022

wanaweza wakazifanya kuhakikisha tunatengeneza fursa za kimapato kwa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunafahamu pia huu Mpaka wa Tunduma ndio Mpaka wenye changamoto za magendo mengi sana. Magendo mengi yanaenda, bidhaa zinakuwa kama zinaenda Zambia, kama zinaenda Kongo lakini zinapiga *u-turn*, zikifika Tunduma zikaenda Zambia zinarudi tena Tanzania. Na huu udhibiti wa magendo katika ule mpaka ni kitu ambacho Wizara inatakiwa ikichukulie kwa namna ya kipekee sana. Pale pia kuna *deficit* ya watumishi, lakini pia mikakati madhubiti ya kuhakikisha kwamba mazingira ya udhibiti wa magendo yanawekwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi si mtaalam wa mambo ya kodi na wala si mtaalamu wa mambo ya udhibiti wa magendo; lakini magendo nayaona yakitoka Zambia yakirudi Tanzania. Kwa hiyo tunafahamu kabisa nchi zile tunazopakana nazo wao wana mazingira ambayo yanawashawishi wafanyabiashara wa Tanzania wakawekeze na kusajiri kampuni kule ili wanapokuwa wanapeleka mizigo kule, inapiga *u-turn* ionekana kama ilikuwa imeenda Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, niombe sana watumishi pale mpakani waongezwe. Nadhani hii kwenye upande wa mapato ya nchi tutakuwa tunaisaidia nchi kuweza kupata fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nilitamani kuongelea kwa upande wa Tunduma; ni kwamba tumekuwa tunaona kabisa kuna masoko mbali mbali ambayo yanaendelea kujengwa. Kuna Soko la

8 NOVEMBA, 2022

Kakozi ambalo unaona kabisa ni soko la Kimatifa na ni soko zuri. Hata hivyo bado halijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niseme tu, Wizara ije na mkakati kabambe au maalum kwa ajili ya ile zone ya Tunduma na Momba kwa ujumla. Nadhani kuna kitu ambacho tutafanya *additional* katika mapato ya nchi hii. Nitakuwa sijajitendea haki kama sintoongelea hiki kipengele cha kuchochea maendeleo ya watu, kumarisha afya, maji, elimu, upimaji wa ardhi na kuimarisha huduma za maendeleo ya jamii na makundi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongelea hiki kipengele kwa sababu ni kipengele ambacho huwa kinanigusa sana, hususan ukiangalia na changamoto ambazo zimekuwa zikiendelea. Kama vile ongezeko la magonjwa ya afya ya akili, vifo vya watu kujiua au kuua. Nilitamani kwamba kwenye hiki kipaumbele ambacho kimeandikwa kuchochea maendeleo ya watu kuimarisha afya, maji nakadhalika, hapa kwenye maendeleo ya jamii na makundi maalum, hii makundi maalum ingetamka ustawi wa jamii. Kwa sababu tunafahamu hii Wizara ina kada mbili tu, ina maendeleo ya jamii ina ustawi wa jamii. Ustawi wa jamii ndicho kitu kinachobeba makundi yote haya maalum mengine. Kama kweli nchi inataka kupiga hatua kwenye maendeleo ya watu tuanatakiwa ku-*invest* kwenye eneo la ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ni nyingi, kada hii ina wataalamu wengi wazuri. Nitumie *forum* hii pia kumshukuru Rais amejiri Maafisa Ustawi wa Jamii 139. Tunafahamu mahitaji halisi kwa mwaka uliopita kwenye bajeti iliyopita tulikuwa tunaona ni asilimia 97 ya upungufu wa Maafisa Ustawi wa Jamii kwenye maeneo yetu. Hawa

8 NOVEMBA, 2022

ndio watu ambao wanaweza waka-*stabilize* hali halisi ya kisaikolojia ya wananchi wetu ili waweze kufanya vizuri kwenye uchumi, katika mambo mengine ya kielimu na masuala mengine ya kijamii. Hata kupambana na hivyo vikundi vya mikopo na nini, huwezi ukapambana na kuchukua fedha huku akili yako kisaikolojia haiku vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba Wizara hapa, wanaposema maendeleo ya jamii na makundi maalum, ile makundi maalum iondoke na badala yake waweke ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kitu kingine pia nilitamani kuomba kwenye mpango wa bajeti unaokuja suala la maji, kama walivyotuahidi kwa mji wa Tunduma, tunajua changamoto ya mji wa Tunduma. Ninaitaja sana Tunduma kwa sababu ni mji ambao ni mpakani na ndiyo wageni wengi wa nchi zingine wanapokuja wanafikia Tunduma kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna maji pale na kuna mradi ambao tumeahidiwa wa *almost* bilioni 17 basi watusaidie uweze kuisha haraka ili hata watu wanapokuja kuwekeza Tunduma wawe na uhakika wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Waheshimiwa Wabunge kanuni yetu ya kuchangia mjadala huu inasema; “Mjadala wa Mapendekezo wa Mpango wa Taifa utahusu mpango wa mambo ya jumla.

8 NOVEMBA, 2022

Wabunge watachangia na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji kwa sera za kiuchumi, za kifedha, za kodi na kipaumbele katika mpango wa bajeti ya Serikali".

Pamoja na michango mizuri nitawaomba Wabunge mkijikite katika eneo hili mtoe na ushauri kwenye masuala ya kifedha, kiuchumi na masuala ya kikodi.

Nilishamtaja Mheshimiwa Inno naona ameshaingia, ajandae Mheshimiwa Mgalu, ajiandae Mheshimiwa Manyinyi.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ys kuchangia Mpango wa Taifa wa maendeleo. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mama yetu, Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuiendeleza nchi yetu. Nitumie nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu kwa Taifa kwenye sekta ya utalii. Sisi wote ni mashuhuda, Mama amefanya kazi kubwa kupitia *Royal Tour*, watalii wamekuwa wengi na kuna kila sababu ya sasa kuelekeza maeneo mengine yenye utalii ili kusudi tuweze kuongeza pato kwenye Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi utalii upo katika Nyanda ya Kaskazini, lakini nchi yetu imepata bahati ya kuwa na vivutio vingi vya kitalii hata katika sehemu zote za Tanzania. Kuna mradi mkubwa ambao unafanyika wa kuendeleza utalii na kuendeleza rasilimali kusini ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbuga ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere lakini kuna Mbuga ya Mikumi,

8 NOVEMBA, 2022

kuna Mbuga ya Uduzungwa zipo katika Mkoa wa Morogoro. Vile vile kuna Mbuga ya Ruaha Mkoa wa Iringa na kuna Mbuga ya Katavi Mkoani Katavi. Katika mpango huu wa *REGROW* tuna kila sababu ya kudhani kwamba, kama Serikali itasimamia kikamilifu mpango huu tuna uhakika wa kupata mapato mengi kwenye mbuga katika Ukanda wa Kusini na kuongeza mapato makubwa katika Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe tu kupitia mpango huu Serikali isimame na ihakikishe kwamba kuna fedha nyingi, najua zimepelekwa, zikasimamiwe inavyopaswa ili ziweze kuleta matokeo chanya. Yakajengwe madaraja kwenye hifadhi zetu, zikajengwe barabara kwenye hifadhi zetu, lakini vile vile zikatumike kufanya *promotion* ya utalii ili kusudi tuongeze pesa katika sekta ya utalii na kuweza kupata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, sambamba na hilo katika mbuga ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo iko Wilayani Morogoro, niombe Serikali, ili kuweza kuwafanya watalii waweze kufika kwa haraka lakini vile vile kwa wepesi na kwa wingi barabara ya Digwa-Kisaki iko katika mpango wa ujenzi. Bajeti iliyopita imetangazwa, tuliahidiwa mpaka kufikia Mwezi wa Tisa itakuwa tayari imeshatangazwa kwenye *TANePS* kwa ajili ya kumpata mkandarasi. Hata hivyo, mpaka muda huu tunaozungumza jambo hili halija-*tick*. Nikuombe tu Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya ujenzi lakini Waziri wa Fedha najua fedha ipo basi kazi hii ifanyike ili kusudi suala hili likamilike tuweze kuongeza utalii. Tukiweza kuongeza watalii kwa upande wa kusini ni imani yangu kwamba tutakuwa tumepata fedha nyingi za utalii na tutaweza kusaidia kusukuma maendeleo. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, nitumie nafasi hii kuipongeza Kamati ya Bajeti, tumeona ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Bwawa la Mwalimu Nyerere lipo katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini, Jimbo la Morogoro Kusini ambalo mimi nipo kule, lakini vile vile lipo katika Halmashauri ya Rufiji. Bwawa hili likikamilika litaweza kuleta matokeo makubwa sana katika uchumi wa nchi yetu. Niombe Serikali ikasimame katika mazingira yanayotakiwa kuhakikisha kwamba linakwisha kwa muda na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imesema, mradi ulikuwa unatakiwa kukamilika tarehe 15 mwezi Juni mwaka huu, lakini wameongezewa mpaka tarehe 15 mwezi Juni mwaka unaokuja. Ombi langu kwa Serikali, wakandarasi, na mimi mwenyewe ni mkandarasi, kuna ujanja na ubabaishaji; wanaweza wakafika mahali wakataka kutucheleweshea mradi wetu ambao kwetu sisi tunauhitaji kwa kiasi kikubwa. Tuhakikishe kwamba muda huu waliopewa kwa mujibu wa utaratibu kazi iwe imekamilika; kwa sababu; moja, inaonekana, vile vile Kamati yetu imesema, wameongezewa mwaka mmoja lakini mpango kazi wa mkandarasi huyu unaonekana kwamba atamaliza kazi hiyo mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe, wenzetu ambao wanasimama TANESCO wakahakikishe kwamba wanasimama kikamilifu kuhakikisha mradi huu unakamilika ndani ya muda ili yale matumaini ya Watanzania kupata umeme wa uhakika lakini uliokuwa salama uwe umekamilika. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, katika suala hili la mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kuna suala la CSR. Halmashauri ya Morogoro Vijijini na Halmashauri ya Rufiji mpaka tunafikia asilimia 75 ya ujenzi wa Bwawa hili bado hatujapata fedha yetu ya CSR kwa mujibu wa mkataba unavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi napata mashaka, kupitia Kamati ya Bajeti, TANESCO kwa mara ya kwanza walipeleka kwa mkandarasi ujenzi wa uwanja wa michezo Dodoma. Mkandarasi akakataa kwa sababu haikidhi vigezo vinavyotakiwa. Lakini tayari katika Kamati ya Bajeti nimeona, safari hii TANESCO tena wamepeleka miradi ambayo haihusiani na wananchi wa Morogoro Vijiji na Halmashauri ya Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia kuna ujenzi ambao unaambiwa unataka kujenga chuo cha umeme na gesi asilia Lindi, sitaki wala sina mashaka na Serikali kufanya hivyo. Kuna ujenzi wa kituo cha TEHAMA – Kigoma, sina mashaka na Serikali kufanya hivyo, lakini kuna ujenzi wa kituo cha Afya au Zahanati Dodoma sina mashaka na hilo lakini vilevile Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Morogoro hata sisi Halmashauri ya Morogoro Vijijini wanahitaji huduma hizo. Kama ni suala la Chuo cha Umeme, gesi asilia, kwa nini kisijengwe Morogoro au kikajengwa Pwani? Ninaishukuru Kamati ya Bajeti imeliona hilo na imesema, tunaomba fedha ya CSR ambayo iko ndani ya Halmashauri mbili; ya Morogoro Vijijini na Halmashauri ya Rufiji ije kwetu wananchi wenye halmashauri hizo kama vile utaratibu wa mkataba unavyosema. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kilimo. Kilimo ndiyo uti wa mgongo na katika hili umeshuhudia hapa mchana leo kutwa nzima Waheshimiwa Wabunge wakizungumza suala la upungufu wa chakula na tatizo la mvua. Tumefanya kazi kubwa kwenye mbolea, mbegu, viuatilifu na kila kitu. Nadhani ni wakati muafaka sasa hivi tukajipanga katika bajeti yetu ijayo katika kilimo cha umwagiliaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina maeneo makubwa ya kulima kilimo cha umwagiliaji. Mfano katika Mkoa wetu wa Morogoro, tuna zaidi ya hekta 2,000,000 zinazofaa katika kilimo cha umwagiliaji, lakini kila mwaka Serikali inapokuja inaendelea kuleta bajeti kwenye maeneo ya miradi midogo midogo tu ya umwagiliaji. Nadhani ni wakati muafaka kwa Serikali katika bajeti ijayo, kuangalia miradi mikubwa ambayo italeti tija na wingi wa chakula katika nchi, kitoshe nchini na ikiwezekana tusambaze kwa kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, naiomba Serikali, katika mwaka unaokuja iangalie uwezekano wa kuvuna maji ya mvua. Nilishalizingumza katika bajeti karibu mbili. Kipindi cha mvua, pale Mbande, kuna eneo linaitwa Matoroli, maji yanavuka mpaka juu ya barabara. Pia kipindi cha mvua, pale Mtanana karibu na Kibaigwa, maji yanavuka hadi juu ya barabara. Dumila vile vile mpaka yanafanya uharibifu mkubwa kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuna mabwawa katika *station* ya reli Msaganza-Kidete. Nadhani ni wakati muafaka kwa Serikali katika bajeti inayokuja ikaelekeza kufukua mabwawa yale, lakini tukachimba mabwawa

8 NOVEMBA, 2022

katika maeneo haya niliyoyasema ili tuvune maji ya mvua, tufanye kilimo cha umwagiliaji ambacho ndicho chenye uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la maji. Niendeleo kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo inaifanya katika suala la maji. Karibu tumepata taarifa, maji yamefika vijijini kuna mahali asilimia 80, asilimia 75, lakini uhalisia ni kwamba bado changamoto ya maji ni kubwa katika nchi yetu. Naishauri Serikali yangu, katika bajeti inayokuja, hebu ijielekeze kwenye kufanya miradi mikubwa ya maji yenye uhakika ili iweze kusambaza maji katika maeneo mengi na tukaondokana na adha hii ya maji, kuliko hii miradi midogo midogo ya kuchimba visima, halafu ndani ya kipindi kifupi visima vimekauka; kuchukua maji kwenye mito midogo midogo wakati tuna maziwa makubwa katika nchi hii ambayo tukiyatumia yanaweza kupunguza kero ya maji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba kwa Serikali yangu, ijitahidi kwa kiasi inachoweza kufanya kufanikisha haya yote ili kuleta tija na mafanikio kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Huo ndiyo ulikuwa mchango wangu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mgalu, halafu ajiandae Mheshimiwa Manyinyi. Mheshimiwa Mgalu hayupo, Mheshimiwa Manyinyi endelea, halafu ajiandae Mheshimiwa Mchungahela.

MHE. VEDASTUS M. MATHAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami

8 NOVEMBA, 2022

niweze kuchangia katika mpango ulioko mbele yetu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha na Mipango kwa namna ambavyo amejitahidi sana kuwasilisha mpango wake kama maandalizi ya bajeti ya mwaka kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia hali halisi katika mazingira ya kawaida ya wananchi. Maana mimi nafika mahali najiuliza, yawezekana ni mimi tu kule Musoma au ni nchi nzima ndivyo ilivyo? Hali halisi ya maisha sasa hivi ni ngumu, kwa sababu vitu vimepanda sana bei. Nimeona hapa katika mpango Mheshimiwa Waziri anasema mfumuko wa bei siyo mkubwa, nikashindwa kuelewa kwamba yawezekana vigezo tunavyoviangalia siyo vigezo vinavyogusa hali halisi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano hai; leo ukiangalia bei ya chakula, nakumbuka mwaka 2021 mwezi Julai, mchele kwa pale Musoma ulikuwa unauzwa shilingi 1,100; lakini leo hivi tunavyozungumza, bei ya mchele ni shilingi 2,500. Hali hii ikiendelea kuja kufika mwezi Desemba, ni ukweli usiopingika kwamba utakuwa unauzwa siyo chini ya shilingi 3,000. Sasa kama bei ya chakula kama mchele ambao ni wa lazima, unaweza ukapanda mara tatu, halafu unawezaje kusema kwamba mfumuko wa bei siyo mkubwa! Unapozungumza habari ya mahindi Musoma mwaka 2021, tulikuwa tunanunua shilingi 50,000, leo hivi tunavyozungumza gunia moja la mahindi ni shilingi 120,000. Bei imepanda zaidi ya mara mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa namna yoyote ile, ni vizuri tuangalie kwamba hali halisi ya uchumi

8 NOVEMBA, 2022

wa watu wetu wanapolia, wana haki ya kulia, kwa sababu kwanza fedha zenyewe hazipatikani, lakini bei yake ndiyo hiyo tu kwamba maisha yameendelea kuwa magumu kulingana na mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kwanza naishukuru Serikali kwa maana ya Waziri wa Kilimo, wiki hii nimwomba chakula na ametupatia kiasi cha kutosha ambacho kiko njiani kinaenda Musoma kwa ajili ya kwenda kupunguza yale makali ya bei ya vyakula. Ombi langu ni kwamba basi wajitahidi hicho chakula kiendeleo kwenda mara kwa mara, kwa sababu tofauti na hapo, naamini yawezekana chakula kitauzwa mpaka shilingi 150,000 kwa gunia na ukilinganisha na kipato cha watu wetu, hali ya maisha itaendelea kuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sasa hivi tunachangia mpango kwamba nini kifanyike katika kuhakikisha kwamba angalau kwenye bajeti ya mwaka kesho tunaendelea kuboresha; kati ya maeneo ambayo tunadhani tunahitaji kuwekeza fedha sana, moja ni eneo la kilimo. Tunashukuru kwamba Serikali imeongeza kwenye bajeti iliyopita, lakini iendeleo kuongeza zaidi. Kwa sababu tukiongeza fedha kwenye kilimo, kwanza tafasiri yake ni kwamba itawafanya wale watu wetu kule kwa maana ya Serikali iendeleo kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji. Maana hata kama tungeweka fedha kwenye kilimo halafu tukajikuta kwamba hatutengenezi miundombinu ya umwagiliaji na hali ya ukame ambayo inalisumbua Taifa letu, wakati mwingine tutajikuta kwamba fedha zimeongezeka, watu wamelima na matokeo yake bado shida inabaki pale pale kwa sababu ya ukosefu wa mvua.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe tu kusema, katika nchi yetu kwa namna ilivyokaa, imezungukwa na nchi nyingi ambazo vile vile zinaitegemea Tanzania ili iweze kuilisha. Sasa tunadhani nini kifanyike katika mpango ujao? Hebu tujaribu kuwa na aina mbili za mazao; mazao ya chakula na mazao ya biashara. Kwa sababu leo ninavyojua, kama sisi watu wa Mara kwa mfano, mchele wetu mwingi unaliwa na watu wa Kenya na Uganda ambapo kwa kusema kweli wanatusaidia katika kutupatia fedha, lakini sasa, hata kama tunauza kule chakula, lazima tuwe na akiba yetu ya kutufanya tuendelee ku-survive.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ungeniuliza ushauri wangu ningesema, kila mkoa uandae mazao yao ya chakula na mazao ya biashara. Kwenye yale mazao ya chakula hebu tujaribu kuwa *strict* tusiyauze nje. Mfano, kwa pale Mara, leo tukianzisha mfano, kilimo cha mihogo ambacho mpaka leo tunalima mihogo na tukawa *strict* kwamba mihogo tusii-export nje na Serikali ikaweka nguvu pale katika kusaidia wale wakulima wa mihogo kama ambavyo inasaidia kwenye maeneo mengine...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Fedha, umesikia mihogo! (*Kicheko/Makofi*)

MHE. VEDASTUS M. MATHAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafasiri yake ni kwamba sisi Mara tutajua kabisa kwamba zao letu la chakula, tunalima mihogo na mtama; ambapo ukichanganya mihogo na mtama ni chakula safi kabisa kuliko hata mahindi. Kwa hiyo, kwa sababu wenzetu wa Kenya

8 NOVEMBA, 2022

wanahitaji mahindi, sisi Mara tutalima mahindi, tutawasafirishia, tutalima mpunga kwa maana ya mchele tutawasafirishia. Kwa hiyo, tutamaliza sasa katika kuondoa tatizo. Kumbesasa tukishakuwa na huo utaratibu wa zao la chakula na zao la biashara, basi itatusaidia sana kuhakikisha kwamba tunaendelea ku-*survive* na mfumuko wa bei unaendelea kushuka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine lililopo ambalo ni kubwa sana ni tatizo la ajira. Yaani ukiangalia kadri vijana wanaozalishwa kuingia kwenye soko la ajira, lakini wakati huo hakuna ajira, siyo mjini, wala vijijini. Hata zile ajira za mjini kwa sisi watu wa mjini nizile biashara ndogo ndogo. Ukizungumza biashara ndogo ndogo tunafika mahali tunasema Wamachinga watengewe maeneo. Kumbuka kwamba wale ni watu wenye mitaji midogo, lakini tunawatenga mbali na soko, mbali na watu. Matokeo yake ni kwamba tunapofanya hivyo, ndiyo maana kila leo wanalazimisha kurudi mjini. Kwa hiyo, wanakukwa ni kama wakimbizi katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani katika mpango huu ni vizuri vile vile tukaangalia katika yale maeneo ambayo yana mikusanyiko ya watu, hata kama kuna taasisi ya Kiserikali pale tuone namna ya wao kupata eneo ili waweze kufanya biashara. Tofauti na hapo, maana yake ni kwamba maisha yanaendelea kuwa magumu na Wamachinga hawawezi kufanya biashara, lakini hata kule kijijini ambako wangeweza kwenda, bado nako hawataweza kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lingine ambalo naishukuru kwamba Serikali imeanza kuliona, lakini hebu

8 NOVEMBA, 2022

iongeze bidii ni kwenye eneo la uvuvi. Tunakubali kwamba angalau kwa sasa hivi, Serikali imeweka mpango wa kukopesha wale wavuvi wadogo wadogo. Tunadhani watu wengi suala la elimu bado linawasumbua sana na vile vile namna ya kuweza kuipata mikopo. Kwa hiyo, ombi langu, tuweke katika mpango namna ya kuendelea kuelimisha wananchi wetu ili waone namna bora zaidi ya kuweza kupata mikopo. Pia baadhi ya maeneo Serikali inapaswa iwekeze. Mfano, leo unapozungumza pale kwangu mjini, eneo kama la Makoko, ni eneo ambalo ni zuri sana kwa biashara ya dagaa, utawakuta akina mama wamebeba mabeseni wanaenda kuanika halafu wanauza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe Serikali ikiwekeza pale, wale akina mama wakaweza kuwa wanakaushiwa dagaa zao vizuri, tafsiri yake ni kwamba wale wavuvi watawekeza kwenye vifaa vizuri vya kuvulia. Hata akina mama ambao wanahangaika na mabeseni kichwani, wataweza kukausha dagaa zao pale pale na hatimaye watauza katika maeneo yote ambayo tunadhani yanahitaji hao dagaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mchungahela, halafu ajiandae Mheshimiwa Felix.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunipa nafasi hii ya kupumua. Nakushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchango wa mapendekezo na bajeti.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kuwa, pato la Tanzania kwa maana ya pato la nchi limekuwa likiongezeka kwa wastani wa asilimia 4.9, wastani ambao ni pungufu kwa 1% ya wastani ule tuliokuwa tumeukusudia. Ongezeko hili limechangiwa na sekta mbalimbali. Sekta zilizosaidia kuchangia ongezeko hili ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Sanaa na Burudani imechangia kwa asilimia 19.4; Sekta ya Umeme imechangia asilimia 10; Sekta ya Madini imechangia asilimia 9.6; halikadhalika Sekta ya Habari na Mawasiliano imechangia kwa asilimia 9.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango huo mzuri kwenye hizo sekta, bado kuna sekta muhimu sana za kiuchumi ambazo zenyewe zinategemewa kuwa ndiyo nyenzo za kufanya pato la Mtanzania au pato la nchi likue kwa haraka, lakini sekta hizi hazikukua katika kiwango kinachoridhisa. Sekta hizi zimechangia mchango kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Elimu ni asilimia 5.1; Sekta ya Viwanda imechangia kwa asilimia 4.8; halikadhalika Sekta ya Kilimo imechangia kwa asilimia 3.9; Sekta ya Biashara kwa asilimia 3.5; na Sekta ya Fedha na Bima imechangia kwa asilimia 4.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hizi ni muhimu sana kama nilivyosema kwa ajili ya ukuaji wa pato la Taifa. Kama kungekuwa na jitihada za kuhakikisha kwamba sekta hizi nilizozitaja hapo ambazo ni muhimu katika ukuaji wa pato la Taifa zingeangaliwa au kupewa *attention* ya

8 NOVEMBA, 2022

kutosha, bila shaka hali ya uchumi ingekuwa imekua zaidi ya hali iliyoko sasa.

Mheshimiwa Spika, ili tuendeleo tunahitaji sekta hizi zikue zaidi kiasi cha kuwezesha wastani mzima wa pato la Taifa kukua kwa angalau 8% na kuendelea. Hivyo ndiyo hali halisi ilivyojitokeza katika nchi nyingi sana zilizoendelea au zinazoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanikiwa au kutokufanikiwa kunatokana na sababu, na sababu hii ni jinsi tafsiri iliyopatikana kwenye sekta hizi nilizozitaja kwenye mpango ule: Je, mpango ule umetafsiri nini katika sekta hizi? Kwamba inajua kitu gani kuhusiana na hizi sekta? Kwa mfano, ukuaji wa elimu, tafsiri sahihi ya ukuaji wa elimu, lazima iwe kama ifuatavyo: Kwamba nchi yenye ukuaji wa elimu basi itakuwa na rasilimali watu bora ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji; pia itakuwa na watu wenye fikra pevu; na halikadhalika ina watu wastaarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya ukuaji wa viwanda ni nini hasa? Soko la uzalishaji linaonekana hapo katika tafsiri ya ukuaji wa viwanda. Ukuaji wa viwanda pia unatafsiriwa na ukuaji wa vitu vilivyozalishwa kama vile madini, mazao ya kilimo, mazao ya misitu, mazao ya uchumi, mazao ya uchumi wa bluu na mazao ya mifugo. Pia sekta hii ukuaji wake unatafsiri kodi iliyokuwa rafiki kwa maana kama kodi ni rafiki, inaweza ikaonekana waziwazi katika ukuaji wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa biashara pia unachangia sana katika kuenenda, yaani kuonesha jinsi gani uchumi unatakiwa uwe. Tafsiri sahihi ni nini?

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa biashara pia unachangia sana katika kuenenda, yaani kuonesha jinsi gani uchumi unatakiwa uwe. Hapa tafsiri sahihi ni nini? Tafsiri inaonyesha kwamba, kama biashara imekuwa hapa kuna suala la ukuaji wa uwekezaji. Hali kadhalika, kuna ukuaji wa pato la Serikali kupitia vyanzo vya kodi ikiwa ni pamoja na leseni pamoja na tozo. Vilevile pato la mtu mmoja mmoja linakuwa linajionyesha hapa, hii ndio tafsiri inayopatikana katika ukuaji wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna uwezo wa mtu mmoja mmoja katika kufanya manunuzi yaani *purchasing power*, inaonekana hapa. Halikadhalika, ongezeko la bidhaa bora, ambazo zenye kuweza kuleta ushindani, mnunuzi ana uwezo wa kuchagua bidhaa anayojisikia. Haya yote yanatokana na ukuaji uliokuwa bora wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa fedha na bima tafsiri yake ni nini pia? Tafsiri yake ni kwamba, kuna ongezeko kubwa la mtaji, lakini kuna kuimarika kwa biashara pia na uwekezaji. Vilevile inaonesha hapa kuna mikopo shindani ambapo benki zinashindana kuweka riba ya chini kabisa ya mkopo, kiasi kwamba mlaji au mtumiaji wa mkopo ule anachagua wapi aende akachukue. Hali hii inaleta athari kubwa katika pale ambapo yeye atawekeza, halikadhalika ni kuwezesha uchumi wote wa nchi hii kwa ujumla au nchi husika kukua kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa kilimo na wenyewe una athari zake ambazo una tafsiri sahihi, ambazo tafsiri hizi zinatakiwa pia zionekane wakati

8 NOVEMBA, 2022

tunatengeneza *plan* au tuna-*plan* bajeti. Ongezeko la uzalishaji linaonekana pale, pia bei nzuri ya bidhaa zile zilizozalishwa. Pia kuna kinga ya bidhaa na bei, hapa kinga ni nini? Maana yake kwamba kile kilichozalishwa, kama kunatokea changamoto ya uzalishaji, kwa mfano, mvua, maana yake changamoto hii inaweza ikafidiwa kwa ile kinga iliyowekwa pale kwa maana ya bima. Vile vile hata kama bei itashuka, pia bei ile itafidiwa na bima ile, kwa maana hiyo kinga hii itakuwa imesaidia. Hizi ndio tafsiri za msingi kabisa ambazo zinatakiwa zi-*reflect* katika mipango yetu. Kama mpango wowote ule hauwezi ku-*reflect* tafsiri ya mambo haya basi ni kiasi kidogo sana tutaona kuna ukuaji wa pato la mtu mmoja mmoja, lakini na pato la Taifa ukuaji wake utakuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojaribu kuanza kusema kule mwanzo, tafsiri hizi lazima zionekane katika mpango na mpango ambao utazalisha bajeti. Kwa sababu hiyo Mpango lazima uzungumze waziwazi *products* zote zile zinazotengenezwa soko lake liko wapi. Kama mpango hauonyeshi soko basi ni kama vile mpango huu umefeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta mbalimbali za habari na mawasiliano ambazo zimeonyeshwa pale katika zile sekta zilizochangia maendeleo au ukuaji wa pato la Taifa, zilionyesha kama kwamba zimekua kwa kiasi kikubwa. Pamoja na ukuaji ule kwa sababu Sekta hii ya Habari na Mawasiliano ni sekta unganishi tu, ni sekta ambayo haiwezi kutoa athari yake moja kwa moja katika pato, kwa maana vile vyanzo ambavyo ni muhimu nilivyovitaja vinaunganishwa na sekta hii.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumeonekana pia ongezeko la madini, lakini athari ya madini haiwezi kujionyesha moja kwa moja kutokana na hali ya sasa ya uchumi ulivyo, kwa sababu madini haya tunauza ghafi. Kama tungekuwa tumeyauza yakishakuwa *processed* bila shaka hali ya uchumi wa sasa hivi au ongezeko la pato la Taifa ingekuwa ni kubwa kuliko hali ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojaribu kuzungumza pale, mpango huu wa sasa hivi kwa mfano, umeonesha changamoto nyingi. Changamoto mojawapo ni kutokuonesha masoko ya *product* ambazo zinatokana na uzalishaji. Mfano ni uzalishaji wa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, kengele ya pili.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kavejuru Felix, wajiandae Mheshimiwa Shabiby na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

MHE. KAVEJURU E. FELIX: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niweze kutoa ushauri kwenye Mpango huu wa Maendeleo. Ushauri wangu utajikita katika maeneo matatu: Kwanza, ni kwenye zao la chikichi; pili, ni zao la kahawa; na kama muda utatosheleza basi nitakuwa na ushauri kwenye shughuli ya uvuvi.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu idadi kubwa ya watu wamejiajiri kwenye kilimo. Asilimia 65 ambayo ukipiga hesabu kwa sasa hivi ambayo tumepata idadi ya milioni 61 ya Watanzania, kama asilimia 65 ndio inayoshughulika na kilimo, basi ukipiga hesabu kwa harakaharaka utakuta kwamba kilimo kimeajiri zaidi ya milioni 39.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu za mwaka jana 2021, Sekta hii ya Kilimo ilichangia kwenye pato la Taifa asilimia 26.1, ukilinganisha idadi ya wanaoshughulika na kilimo na kiwango kinachochangiwa kwenye pato la Taifa haviwiani kabisa. Hapa kuna *gap*, tunatakiwa tuangalie ni kitu gani kinachokosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ya jumla ambayo bado tunatakiwa tuyafanyie kazi. Kwa kuwa idadi kubwa ya Watanzania wamejiajiri kwenye shughuli ya kilimo, basi Serikali inahitaji kuwa na jicho pevu la kuwekeza hasa hasa kwenye shughuli za kilimo na hasa kwa kuboresha miundombinu ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na zao la chikichi; nchi yetu kwa mwaka imetumia zaidi ya bilioni 500 kuagiza mafuta. Mafuta mengine ambayo yanatokana na zao la chikichi ambalo tayari Mwenyezi Mungu amekwishatupa lipo Kigoma. Kigoma ina ardhi inayofaa kwa chikichi pamoja na Katavi. Nchi ya Malaysia ambapo tunaagiza mafuta walipata mbegu ya mchikichi kutoka Kigoma. Tunatumia zaidi ya bilioni 500 kuagiza mafuta ambayo tayari tungeweza kuzalisha Kigoma na hizo hela zingine zikatumika kwenye maeneo mengine.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri, kwanza kabla ya kutoa ushauri nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa Mkoa wetu wa Kigoma. Amehamasisha wakulima wapaneue mashamba, walime na kweli wamehamasika na wamelima zao la chikichi mashamba sasa ni makubwa. Kituo cha *TARI* kimezalisha mbegu na miche mizuri wamehamasika. Changamoto ambayo Serikali inatakiwa ikafanyie kazi ili tuokoe hayo mabilioni ni kuleta viwanda vya kati vitakavyoweza kuchakata zao hili la michikichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda tulivyonavyo Kigoma ni vidogovidogo, kutokana na zao la chikichi, unapata mafuta haya ambayo ni ya kula tunayatumia kila siku, unapata chakula cha mifugo bado unapata malighafi ya kutengeneza samani za nyumbani na bidhaa nyinginyingi. Naomba kwenye Mpango huu wa Serikali, Wizara ya Kilimo ishirikiane na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kutafuta wawekezaji wa ndani na nje ili wajenge viwanda vya kuchakata mafuta katika Mkoa wetu wa Kigoma. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeokoa fedha nyingi na nchi itakuwa na uwezo wa kupata mafuta yenyewe ya kuzalisha mafuta na kutosheleza mahitaji ya ndani na ziada tutapeleka kwenye nchi zingine, tutauza kama biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, ni kwenye zao la kahawa. Kahawa ni zao la biashara ambalo linatuingizia fedha za kigeni. Katika nchi yetu ya Tanzania zaidi ya mikoa 16 inalima zao la kahawa. Tunashukuru kwa juhudi kubwa na tunamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ruzuku ambayo

8 NOVEMBA, 2022

ameiweka kwenye mbolea. Watu tunaolima kahawa ametugusa, tunasema mama ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao hili bado halijapewa kipaumbele na ndiyo mwarobaini ambalo linaweza likatuingizia fedha za kigeni. Ukilinganisha na nchi zingine ambazo wanazalisha lakini kwa maeneo madogo, bado miche inayozalishwa na *TARI* na *TaCRI* bado ni midogo ukilinganisha na nchi jirani. Uganda kwa mwaka wanazalisha miche ya kisasa bora zadi ya milioni 61. Ethiopia ambayo ndio wazalishaji wa kwanza wanazalisha miche kwa mwaka zaidi ya milioni 121, lakini sisi Tanzania kwa mwaka huu ndio tumeongeza tumezalisha miche milioni 21. Hiki ni kiwango kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunayo maeneo makubwa na wananchi wamehamasika na tuna vijana wengi ambao wako mitaani, kama zao hili likiboresha, likawekewa pembejeo zote asilimia mia, sawa na korosho nina uhakika kwamba mapato yatakayotokana na kahawa yataongezeka na hela za kigeni zitaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mambo yafuatayo yafanyike, bado kwenye kilimo hicho hicho cha kahawa, tunahitaji kuwekeza kwenye tafiti. Naomba Mpango huu uoneshe ni namna gani ambavyo itawekeza kwenye tafiti za kupata miche bora na usambazaji wa matokeo yake ya utafiti na kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo, basi Mpango unaokuja ni lazima, bora, vyema uoneshe namna gani ambavyo wakulima wataweza kupewa mafunzo pamoja na Maafisa Ugani ili uzalishaji uweze kuongezeka.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la kahawa, watu wamehamasika wanalima kahawa lakini soko lake limekuwa likipanda na kushuka. Mkulima amekuwa akilima lakini bila kuwa na uhakika wa masoko. Tunaomba Mpango wa Serikali katika bajeti ijayo ituwekee masoko, ituonyeshe masoko ili wakulima wawe wanalima wakijua kwamba masoko ya zao hilo la kahawa ni wapi na wapi. Tukifanya hivyo, basi Taifa litaweza kuingiza fedha nyingi za kigeni na uchumi wetu utaongezeka, utakua ili tuweze kufikia asilimia nane kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ni kwenye uvuvi. Tanzania katika Bara la Afrika ndio nchi iliyopendelewa na Mwenyezi Mungu tukapewa maziwa yote makuu, matano yako Tanzania, tuna Ziwa Tanganyika, Victoria, Rukwa, Manyara, Eyasi na maziwa mengine madogo madogo. Hata hivyo, mchango unaotokana na shughuli za uvuvi bado ni mdogo. Mwaka 1954 na mwaka 1957, Serikali ya Kikoloni ya Uingereza ilikuwa na Kituo chake cha Utafiti, walifanya majaribio wakachukua samaki aina ya sangara kutoka katika Ziwa Tanganyika ambalo halikuwepo katika Ziwa Victoria, wakaenda kufanya majaribio wakapata katika Ziwa Victoria kwa mwaka 1954 na 1957. Leo tunashuhudia sasa sangara inatuingizia fedha nyingi sana kutoka kwenye Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye upande wa uvuvi tuna vituo vile vya *TAFIRI*, viwezeshe wafanye tafiti kutokana na haya maziwa madogo madogo ambayo tunayo. Wafanye tafiti ikiwezekana kama sangara anaweza bado akaenda kupandwa kwenye maziwa mengine madogomadogo au migebuga, au

8 NOVEMBA, 2022

samaki wengine ziende kupandikizwa kwenye maziwa mengine madogo madogo ambayo sasa hivi mchango wake wa kiuchumi kwenye upande wa uvuvi ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ya nne ni kwenye biashara. Mkoa wetu wa Kigoma uko mpakani ile ni *gateway* ya biashara ambapo pale tunapakana na Wakongo ambao zaidi ya nusu ya watu wa Kongo wako kwenye ukanda wa mashariki. Tungeomba kwenye mkakati ujao Wizara ya Uchukuzi iwezeshe kutengeneza zile bandari za nchi kavu ile ya Katosho na kuhakikisha ukamilishaji wa meli katika Ziwa Tanganyika, zikamilike mapema ili mzunguko wa kibiashara ukamilike na uende vizuri ili ile SGR itakapokamilika tayari ile Kongo ya Kati kuanzia Kalemii, Bukavu, Bujimai, kuja mpaka huku Kindu wawe wamekwishazoea wote kuja kufanya biashara na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shabiby, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndugulile na ajiandae Mheshimiwa Venant Ptotas.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji. Kabla sijaingia kwenye mpango zaidi, niseme tu kwamba, lengo la nchi yote au mipango ya nchi yote ni kukuza uchumi wa nchi yake. Kwa hiyo masuala yote ya Mpango wa Maendeleo lazima yaendane na mipango ya muda mrefu. Wabunge wengi wameongea lakini bila mpango wa muda mrefu nchi

8 NOVEMBA, 2022

yetu tutakuwa tunapiga *marktime* muda wote. Maana yake tutakuwa tunajenga na kubomoa. Nitoe mfano mmoja, ukiangalia wataalam wetu, ikiwezekana saa nyingine hawa wataalam wa mipango mirefu kama Watanzania wenzetu wanashindwa, basi tungetafuta hata *consultant* kutoka nchi za nje waje kutusaidia ili tusipate hasara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna mipango ile ya muda mrefu ya kuona mbali, tunaangalia hapa, kesho tunabomoa, tunajenga hapa, keshokutwa tukipata kipya tunabomoa kile tulichogharamia tunajenga kipya. Kwa mfano, wewe angalia barabara hata zile za pale Morogoro Road yaani mipango hata haijafika miaka 15 au 16 tayari imekuja mwendokasi, barabara nyembamba inang'ang'anizwa hiyo hiyo ili mradi tu daladala hizi za mwendokasi zipite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija Sam Nujoma barabara haina hata miaka 10 limekuja lile daraja lile *flyover*, kuna madaraja pale yale mawili makubwa yalikuwa pale upande wa *external* nayo yamevunjwa tayari yaani tunapata gharama, tunavunja na kujenga. Sasa ukiangalia ni kwa kuwa hatuna mipango ya muda mrefu, yaani kwamba ujue kwamba mji huu utakuwa hivi, barabara hii itakuwa hivi, eneo hili litakuwa hivi. Kila siku tunajenga, tunapata hasara. Kwa hiyo tunatumia kodi za wananchi kwa kuvunja na kujenga upya kwa muda mfupi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija hapa Dodoma peke yake tunajua kabisa ndani ya miaka mitano nyuma kwamba kuna *airport* ya Msalato inakuja, lakini leo hapa tumeongeza *runway* tumelipa yale majumba, wakati

8 NOVEMBA, 2022

tunajua kabisa tunajenga kule. Kwa hiyo tumeifanya Dodoma leo tumeigawanya katikati. Kwa nini hizo pesa tulizolipa wale *runway* ile tuliyojenga na zile fidia zile ingetoshwa kujenga kiwanja kidogo kama kile ili watu watue. Leo kule kwenye Uwanja wa Msalato kuna Marais watashuka pale, viongozi watashuka pale, uwanja mkubwa. Sasa palikuwa na haja gani ya kupoteza pesa wakati kuna mpango mwingine unakuja? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawa watu wa mipango kwenye nchi hii ni shida, hawana mipango ya kuangalia mbele. Sasa hivi ukiangalia Bandari Kavu, tumepiga kelele bandari kavu imepelekwa pale Kwala pale Vigwaza, Bandari kila siku ya Mungu inafunguliwa kesho, inafunguliwa kesho, sasa hivi tayari imeishakuwa nayo ya kizamani, maana yake reli ya *standard gauge* itafika hapa Dodoma, kwa hiyo itakuwa nayo haina thamani *standard gauge* itafika pale Morogoro, sasa una haja gani tena kwenda kufuata mzigo Kwala badala ya kuweka Bandari Kavu Morogoro kwa ajili ya watu wa Kongo, watu wa Malawi na Dodoma ni kwa ajili ya watu wa Uganda na sehemu nyingine kwa kuanzia, kwani hatuna mipango ile endelevu? Hiyo Kwala imeishakula mabilioni ya pesa na aina kazi yeyote tena ya msingi kama itafunguliwa hii *standard gauge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia barabara sasa hivi katika bajeti hii inayokuja lazima tukubali kwamba sasa hivi kwenye barabara lazima tutumie PPP. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ufanye kila aina uwezavyo leo hii *accident* nyingi zinauwa mpaka Viongozi wengi hapa Maprofesa, Madaktari, kwa mfano yule wa SUA. Kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro ile barabara ni foleni si ya kawaida, kutoka Morogoro mpaka hapa

8 NOVEMBA, 2022

panaitwa Makunganya foleni si ya kawaida, kutoka hapa Dodoma Mjini kwenda mpaka pale Ihumwa foleni si ya kawaida. Hivyo leo, au ninyi kwa sababu wengine mnapitapita humu kwenye vinanii nanii humo hatuonani huku vizuri, tuangalieni sisi tunaokaaa foleni! Ndiyo maana hata saa nyingine kila mtu anajiwekea king'ora na vile vitaa, mnasema ahaaa! anayeruhusiwa hapa ni kuanzia Waziri Mkuu, watu kila mtu anaweka ili apige mkwara apite, kwa sababu barabara hazipitiki, kwa hiyo tutumie mpango wa PPP. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kila Mbunge hapa akipiga kelele mnampa kilometa tano, yule mwingine karuka sarakasi, pamoja na sarakasi kapewa kilometa ishirini mpaka barabara ije ifike kwake ni miaka kumi. Sasa hatuwezi kumaliza barabara zote. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale panaitwa nini; Mlima Nyoka pale Mbeya kila siku *accident* lakini ukiziangalia zote zinasababishwa na barabara, pale panatakiwa *four-way*, *six-way* akija huyu Waziri wa Ujenzi, anasema tunao mpango, lakini ukiangalia ule mpango wa muda mrefu hatuwezi kujenga wenyewe, Dunia nzima inajenga kwa PPP na kama PPP hatupati? Basi kopeni, kukopa siyo dhambi. Mimi mtu anaponiambia kama mnasema wenyewe deni himilivu kopeni! Kama Inyala pale kila siku watu wanakufa kopeni, hapa Dar-es-Salaam-Morogoro na siyo hapo sehemu nyingi hata huko Mwanza barabara nyingi hazipitiki. Kopeni halafu wekeni mpango wa *road tall* nyinyi Serikali wenyewe badala ya kutumia PPP mtakuwa mnachukua *road tall*, mtu anataka kupita pale atapita kwa *road tall* mtarudisha ile mikopo siyo shida.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unapokopa kitu unapokopa kitu, maana yake mimi sitaki kuwa mnafikimnafiki wananchi huko nje.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shabiby, taarifa.

T A A R I F A

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Kaka yangu Mheshimiwa Shabiby, kwamba hata hizo kilometa 25 nilizopigia sarakasi bado hazijatangazwa mpaka sasa. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shabiby, endelea.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa naipokea na nilijua kwa sababu nafanya *research* na nipo Kamati ya Miundombinu. Ni kweli. Bila PPP huwezi kupata Mheshimiwa Mbunge.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shabiby, subiri. Waziri wa Fedha na Mipango

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuongea ni mtani wangu, lakini Mheshimiwa anaechangia, anachangia vizuri lakini nilitaka niweke kumbukumbu sawa kwamba moja naunga mkono mchango wake, anachangia vizuri Mheshimiwa Shabiby.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nitoe taarifa kwamba Serikali tayari imeishatoa tangazo la kazi la kupata watu wa kufanyakazi na wameandika barua kuonyesha nia, kwa utaratibu huu anaousema wa PPP tutajenga barabara inayotokea Kibaha mpaka Morogoro njia za kutosha kama za majuu kule. Pia kwa utaratibu ule ule kutokea Igawa mpaka Tunduma na Mbunge wa kutoka Songwe naye alisema hilo. Hii ni tayari ipo kwenye hatua ya taratibu za kimanunuzi, watu wameishaonesha nia kwa hiyo taratibu zinaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hii barabara ndefu anayosema pamoja na kupiga sarakasi siyo kwamba hajapewa, nayo pia zabuni zilishatangazwa na *shortlisting* imeishafanyika. Barabara ndefu kwenye historia inayoanzia Mbulu inakwenda mpaka Maswa kupitia Sibiti imeishatangazwa, barabara inayotoka Ifakara mpaka Lumecha kule na yenyewe imeshatangazwa kwa utaratibu uleule. Barabara inayotoka Handeni mpaka Singida na yenyewe imeshatangazwa, barabara inayotoka Arusha mpaka Kongwa imeishatangazwa, ile barabara ya kule Mtwango pamoja na Nachingwea inaunga mpaka inatokea *somewhere* Masasi inapita Wilaya tatu hizo zimeishatangazwa na *shortlisting* zimeishafanyika, zenye urefu wa zaidi ya kilometa 2,500 kwa utaratibu wa *EPC+F*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile na kwa hapa Dodoma tayari tulishaweka Jiwe la Msingi na ujenzi unaendelea wa ile *by-pass* ambayo ni zaidi ya kilometa 100 na ninaamini pia na yenyewe itatoa suluhisho hilo. Tukiishamaliza hii PPP ya kwanza na tunaleta Sheria Bunge linalokuja kurekebisha ile Sheria ili iweze kuweka urahisi wa

8 NOVEMBA, 2022

kutekelezeka kwa sababu hilo ni dirisha ambalo tunaamini litapunguza Deni la Taifa pia litatoa space kwenye Bajeti ya Serikali ili Serikali iweze kutoa zaidi huduma za jamii ikiwepo Mikopo ya Elimu ya Juu. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, hujazungumzia barabara za Dar-es-Salaam, tunaendelea Mheshimiwa Shabiby.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza dakika tatu naomba msimamishe muda. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijakataa, lakini nipo Kamati ya Bunge ya Miundombinu, hizo barabara alizozitaja zote tuna kilometa 25, kilometa 30, kilometa ngapi... za kuanzia, hata mkiangalia ile ya Kiteto kwani imepitishwa leo? Si ina miaka kama mitatu, minne? Ndiyo maana nimesema Serikali yeyote duniani haiwezi ikamaliza barabara kwa kupitia pesa zake. Ukienda nchi yeyote iliyoendelea unakuta kuna barabara zinalipiwa *road tall* kwahiyo tumieni *PPP* na mkishindwa kopeni pesa halafu zile barabara mzifanye za *road tall* ili hela ikusanywe kwa *road tall* ili Wabunge wote watapata hiyo pesa. Kwa sababu hao wanaonesha nia wanaonesha nia siku nyingi lakini hawapati majibu, maana yake mimi nipo kwenye Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme huko nje mitaani watu wengi wanaamini kwamba Serikali ya Awamu ya Tano iliacha pesa kwenye Serikali hii. Kwamba ilikusanya pesa mpaka zingine zimebaki, zipo na watu wanaamini kwamba miradi yote ilikuwa inafanya kama reli, kama Bwala la Mwalimu Nyerere bila mkopo pamoja

8 NOVEMBA, 2022

na madaraja. Hata hivyo nataka niseme hakuna ukweli, kwamba hizo reli tunazojenga ni mkopo, hilo bwawa tunalojenga ni mkopo na watu lazima wafahamu kwamba hiyo Serikali ya Awamu Tano ilikopa kiasi kikubwa cha pesa. Hata tunapokuja hapa Serikali ya Awamu ya Sita, inapoanza kuingia kigugumizi wakitishwa kidogo mkopa sana hawakopi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wakiambiwa tu ninyi mna kazi ya kukopa toka muingie mnakopa na wao kweli wanaingiwa woga hawakopi kweli. Nataka niseme hii reli waliyoipeleka mpaka Mwanza bila kukopa kufika Kigoma ni sawasawa na mtu umechukua mkopo, umejenga jumba linatakiwa likurudishie pesa hujalifanyia *finishing*, sasa utarudishaje hiyo pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni lazima wakope, wafikishe hii reli Kigoma, lazima wakope, wafikishe hii reli Kalimwa hadi Kalema, bila hivyo hii Reli ya Mwanza bila kushirikisha nchi ya Uganda na nchi ya *South Sudan* reli ya Mwanza itakuwa haina faida yeyote katika Serikali hata tone, kwa sababu utakwenda Mwanza treni utarudi na nini? Hakuna chochote. Lazima ukienda Mwanza unaporudi upate mzigo wa kwenda South Sudan, upate mzigo wa kwenda Uganda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii reli ya Kigoma ndiyo ambayo italipa zaidi kwa sababu leo hii pale wanayo machimbo ya *nickel* ambayo kila siku itakuwa inasafiri kutoka Burundi kuja Dar e Salaam. Leo hii Kalemi kuna Shaba nyingi sana inatoka kule inakuja Tanzania lakini inashindwa kwa ajili usafiri wa reli haupo na Serikali imetoa bilioni 48 kwa ajili ya kujenga ile bandari lakini

8 NOVEMBA, 2022

bandari imekaa haina faida yeyote ile kwa sababu ya ukosefu wa reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nataka nizungumzie ni kuhusu mazingira. Mazingira nchi hii tunakazi ya kuzungumza tu. Maji, tuchukue maji ya bahari tuchuje, mara tuchimbe mabwawa, hivyo mlishawahi kujiuliza Wabunge huko yanakotoka maji kuna mtu alienda kupanda mti hata mmoja? Tuna kazi ya kusema tu tabianchi.

Mimi kwangu pale Gairo kule Tarafa ya Nongwe kuna Mito Minne, Mto Msowelo, Mto Ludewa, Mto Mvumi, Mto Mkondoa ambayo inaenda Dakawa, inaenda Mto Wami. Ukienda kule mpaka Mbunge ufanye kuhemea uweke watu wawafukuze watu wasikate miti. Vyanzo vya maji vinakufa lakini hakuna Mamlaka yeyote inayoweza kupanda hiyo miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunalalmika tabianchi, ukiangalia ukienda kwenye Wizara ya Maji wanamabonde, kuna Bonde Wami, Ruvu, kuna Bonde sijui la Kanda gani, ukija huku Mazingira wanatoa hela mpaka zawadi Million 50, lakini mtu anaepewa hizo zawadi za Million 50 na Mazingira wamepanda miti kwenye nyumba za gorofa mbele mijini, kule kwenye vyanzo vya mito hakuna! Ukienda TFS wapo, wanasimamia misitu. Basi waungane hawa kati ya maliasili, mazingira na hawa watu wa maji na hizi pesa wanazopewapewa za kupanda miti itafutwe Taasisi moja isimamie vyanzo vyote vya maji hapa Tanzania, zaidi ya hivyo tunapiga kelele! *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapiga kelele Mto Ruvu, lakini Mto Ruvu chanzo chake ni kule Morogoro Kusini, nenda kaangalie kila kona kuna ng'ombe! Ng'ombe peke yake wamemaliza ile miti yote, wamekula kila kitu, wamekata kila kitu, ukienda si ng'ombe tu wakulima wamefanya mashamba mpaka ile mbuga ilikuwa inaitwa Gode yote, sasa maji yatatoka wapi? Mnatafuta vyanzo vingine wakati mlivyonavyo tunashindwa kuvitunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana hawa Maliasili, Wizara ya Maji na Wizara ya Mazingira wakae pamoja waangalie kama nikumkabidhi TFS wamkabidhi TFS kwa sababu sasa hivi yeye ana Jeshi atunze ile misitu na apange ile miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni barabara ile ya kutoka Gairo kwenda Kilindi ya lami ambayo inaenda kukutanika na ile barabara ya kutoka Handeni mpaka Tanga kwenda mpaka Minjingu, ile Barabara ina ahadi ya Marais watatu, Rais Kikwete, Rais Magufuli lakini mpaka leo haijawekwa kwenye mpango naomba ikae kwenye huo mpango, kwa sababu ni barabara nyepesi kabisa. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ahsante sana. Mheshimiwa Ndugulile, jiandae Mheshimiwa Venant Protasa na Mheshimiwa Kandege ajiandae.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuweza kuchangia katika mpango, lengo langu si kuyarudia yale ambayo yametoka kusemwa na wenzangu lakini mengi yameshagusiwa kuhusiana na maeneo ya kimkakati

8 NOVEMBA, 2022

ambayo Bunge linashauri Serikali iende kuyaangalia ambayo yatasaidia kukuza uchumi wetu sambamba na hilo litakwenda kuzalisha ajira mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mfumuko wa bei nalo limegusiwa ni jambo ambalo linawaathiri wananchi wengi, ukizingatia kwamba sasa hivi tuna tatizo la ukame bei ya vyakula itaenda kupanda mara dufu, mimi siyo mchumi lakini naiona hii hali ambayo tunakwenda nayo tusipoweka mikakati thabiti ni jambo ambalo litatuletea shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijielekeza nirudi tena katika mpango. Nimesikiliza sana michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi, kuna mambo ambayo na mimi nayaona kuna changamoto. Jambo la kwanza katika mipango hii ambayo tunaita Bungeni kila mwaka, kunakosekana muunganiko mpango wa mwaka jana hakuna muunganiko na mpango wa mwaka huu na mpango ambao tunaumaliza sasa hivi hauna muunganiko na ule ambao tumepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunaona kwamba hakuna mwendelezo. Vilevile jambo la tatu ambalo naliona ni kwamba tunatengeza mpango ambao siyo shirikishi na ukiangalia mikakati ya sekta mbalimbali ukija ukiangalia hapa katika mpango huu huwezi kuuona huo muunganiko. Kwa hiyo, inaonekana kwamba Wizara ya Fedha ipo kivyake, Wizara nyingine ambazo za kisekta nazo ziko kivyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nitoe ushauri na mchango wangu utakuwa mfupi sana. Jambo la kwanza ambalo naliona nataka kuishauri Serikali ni kuirudisha

8 NOVEMBA, 2022

Tume ya Mipango. Wizara ya Fedha ibaki kuwa Wizara ya Fedha isimamie Sera ya Fedha, isimamie ukusanyaji wa fedha, isimamie matumizi ya fedha. Sasa hivi ukiingalia ile iliyokuwa Tume ya Mipango imemezwa ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango na majukumu yake yamefinywafinywa sana huioni kujitokeza. Kwa hiyo, nashauri ile Tume ya Mipango irudi iwe chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Rais na kazi iwe sasa kufanya yale ambayo nimeyaainisha kwamba itusaidie kukaa na kuangalia mpango mzima wa maendeleo wa muda mfupi, wa muda wa kati na muda mrefu, kutengeneza mwelekeo, kutengeneza mwendelezo vilevile na kuainisha vipaumbele ambavyo sasa tutakuwa tunakaa tunaviongelea ambavyo vitakuwa na tija katika maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ushauri wangu wa pili. Tulianza lakini hapo katikati tukaivunja kitu kinaitwa *Presidential Delivery Bureau* ama *Presidential Delivery Unity* tunahitaji hiki chombo. Sababu ambazo nazisema kwa nini tunakihitaji hiki chombo ni kwa sababu hiki kitatusaidia katika masuala ya uratibu ambayo ni changamoto tunaiona. Kwa sababu ukiangalia sasa hivi kila sekta inaonekana kama ina-*operate* kivyake vyake, sasa tukiwa na chombo kama hiki, kitatusaidia katika hii miradi ya kimkakati kuwa na uratibu mzuri, itafanya tathmini na ufuatiliaji wa hii miradi mikubwa ambayo tunaitekeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho. Hii inatuhusu sisi kama Wabunge, Kamati yetu ya Bajeti inafanya kazi nzuri sana, lakini inaitwa Kamati ya Bajeti. Mimi nilitaka tu na Mheshimiwa Spika yupo hapa ninaomba na kushauri tupanue wigo wa Kamati hii tuuite

8 NOVEMBA, 2022

Kamati ya Fedha Mipango na Ufuatiliaji, ili hii sasa ikae kuangalia ule mtiriko mzima tangia tunaweka mipango, fedha gani tunazibajeti? zinakuwa *disbursed* kwa kiasi gani? Na hii ndiyo changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatengeneza bajeti hapa lakini fedha ambayo inaenda kutolewa mwisho wa siku hailingani na kile ambacho tulikuwa tumekibajeti. Sasa tukiwa na Kamati ya Bunge ambayo itakuwa inafanya ufuatiliaji pamoja na zile Kamati zetu za kisekta itatusaidia sana. Kwa hiyo mimi ushauri wangu ni kuwa, hii Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti iwe ni Kamati ya Fedha, Mipango na Ufuatiliaji, tukienda kwa staili hii itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nimalizie kuhusu Dar-es-Salaam. Ukiangalia ina asilimia Nane ya wakazi wa Tanzania nzima, lakini uchimi wa Tanzania hii asilimia zaidi ya themanini unatoka Dar-es-Salaam. Sambamba na hilo ukiangalia wingi wa magari yako Dar-es-Salaam, ukiangalia miundombinu ya Dar-es-Salaam hailingani na uwekezaji uliopo pale. Vilevile ukiangalia Dar es Salaam tunafanya uwekezaji mkubwa wa reli ya SGR, tunafanya upanuzi wa Bandari hivyo unaendelea, tunaanza kufikiria vilevile kuwa na Bandari ya Bagamoyo, lakini ili uweze kufika Bagamoyo lazima upite Dar-es-Salaam ili uweze kufikia reli ya SGR lazima ufike Dar-es-salaam. Kwa hiyo, pamoja na hili Waziri Mwigulu Nchemba analijua, sisi kwetu wana Dar-es-Salaam wa DMDP ni mradi wa kimkakati na ni mradi muhimu sana kwa hiyo pamoja na zile barabara walizokuwa wanazisema lakini sisi kama Dar-es-Salaam tunazihitaji hizo barabara. Tunazihitaji hizo barabara jana, tulikuwa

8 NOVEMBA, 2022

tunazihitaji leo na tunahitaji tufike kesho katika msingi wa kupata hizo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji, amesema kwamba uchumi Dar es Salaam unachangia kwa asilimia themanini lakini amesahau kwamba Mikoa yetu Songwe, Mbeya, Njombe na maeneo mengine tunachangia uchumi kwa kupitia kilimo asilimia 26 katika Pato la Taifa. Kwa hiyo, tuombe hebu ajaribu kurekebisha kauli ili tuende sawa.

MWENYEKITI: Hiyo siyo taarifa kaa chini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikifikiri ulikuwa unatoa taarifa kuhusu Dar es Salaam au umeghairi, nimekuona umenyanyua mkono kidogo hebu simama kidogo. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam mradi huo wa *DMDP* tunakamilisha mazungumzo nadhani tutakapoanza mwaka huu wa fedha unaanza *DMDP in full* itakuwepo, lakini kwa Mwaka wa Fedha huu tunaanza na Daraja la pale Jangwani linaloshughulika na masuala ya mafuriko ili

8 NOVEMBA, 2022

kuweza kuhakikisha kwamba tunakabiliana na tatizo la mafuriko. Mradi mzima wa miundombinu ya Dar-es-Salaam tumeweka hicho kipaumbele na katika mwaka wa fedha huu ambao bajeti yake hii tunaisoma tutakuwa na *full package*.

MWENYEKITI: Haya, basi pumzika, inatosha, pumzika.
(Makofi)

Mheshimiwa Venant Protas, ajiandae Mheshimiwa Kandege.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia mpango uliowasilishwa na Waziri wa Fedha. Nami niungane na Wabunge wenzangu waliotangulia kuchangia, kwanza kwa kuipongeza Serikali yetu, Serikali ya Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuhangaika huku na kule kuhakikisha Watanzania na sisi kama wawakilishi wa wananchi tunatekeleza yale aliyokuwa amedhamiria kwa kipindi chake cha miaka mitano.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunazungumzia mpango wa Serikali ambao utatusababisha kutengeneza Bajeti Kuu ya mwaka 2023/2024; lakini pia tumekuwa na mpango wa miaka mitano. Waziri wa Fedha alishawasilisha mpango wa miaka mitano, nini Serikali itafanya kwa kipindi cha miaka mitano, kwa hiyo ndiyo maana tunaivunja hii mipango tunaiweka kwa mwaka mmoja mmoja ili iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamezungumza hapa kuhusu Serikali kuwa na mipango

8 NOVEMBA, 2022

mingi bila utekelezaji, lakini tumekuwa na mipango ya muda mfupi. Tunatengeneza mpango wa miaka mitano, lakini baada ya miaka mitano ule mradi unakuwa hauna tija tena kwa jamii. Ndicho alichokuwa anakisema Mheshimiwa Shabiby. Tulitengeneza mpango wa kutengeneza ICD nje ya Dar es Salaam kilometa 40 ya Kwala pale, lakini sasa hivi ile ICD inaonesha haiwezi kuwa msaada kwa Watanzania ilhali wataalamu wetu walisema itakuwa msaada, na tayari shilingi bilioni 30 imeshakwenda pale. Kwa hiyo tunapokuja kujadili mipango basi iwe yenye tija na inakuwa msaada kwa muda mrefu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge walishasema, tunapo-*design* miradi basi tuwe tunaangalia na muda wa mradi utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mingapi. Hauwezi kwenda ku-*design* mradi wa trilion za fedha halafu *life span* yake inaishia miaka 10; hiyo tunakuwa tunakuwa tunamaliza fedha za wananchi na walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishashauri hapa tukasema na kama Mbunge mmoja alisema hapa kama tungechora vizuri mradi wa Ziwa Victoria, tukatengeneza *design* ya kuleta maji safi na maji ambayo yatakuja kutumika kwenye kilimo nchi hii leo ingefungua fursa ya kilimo; lakini wataalamu wetu hawakulifikiria hilo wakafikiria kwenda kuwatibu wananchi halafu wakasahau wananchi wanahitaji kula. Na ndiyo maana wanasema kula ni lazima kuoga hiyari, hawakuliangalia hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa tumeshakosea, tunashauri tena. Tuna mradi wa bomba la mafuta kutoka Uganda kuelekea Tanga, lakini linapotoka

8 NOVEMBA, 2022

Uganda linapita nchini ketu kwa asilimia zaidi ya 70. Nchi yetu itakuwa inanufaika kwa kiasi kikubwa. Tulishauri hapa kwa kuwa, wenzetu wa Uganda wanapitisha bomba hilo la kupeleka mafuta ghafi kwenye Bandari ya Tanga, tukasema kupitia mradi huohuo na fidia hizohizo tutumie tena mradi huo tutengeneze bomba kwa upande mwingine ambalo litarudisha mafuta safi, ili tutakapokuwa tunalilinda kwa gharama zilezile za kulilinda kwa kupeleka mafuta ghafi na ndizo hizohizo gharama tutatumia kurudisha mafuta safi. Ambapo tungejenga matenki makubwa kwa ukanda wa Tabora pale Bukene, tungeweka matenki pale watu wa Mwanza, watu wa Shinyanga, Tabora, Kigoma na Katavi wangeweza kunywa mafuta pale na; malori yote yanayokwenda Dar-es-Salaam leo tusingeyaona. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tungeenda kuweka huko kwa wajomba zangu huko Bukoba matenki mengine, yangeweza kulisha ukanda ule wote, yangeweza kutusaidia. Hata hao waganda wangeweza kupitisha mafuta safi kurudisha katika nchi yao, tungeweza kuokoa fedha nyingi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda mji wa Dar es Salaam mpaka wanaweka *limit* ya malori kuingia mjini kwa sababu bidhaa, kila kitu tumeweka Dar-es-Salaam. Leo ile barabara ya Morogoro – Dar-es-Salaam siku ikija kupata majanga ya kufungwa barabara kwa siku tano na barabara ya Arusha, huku Kanda ya Ziwa kote mawasiliano yanakatika, hususan nishati ya mafuta. Kwa hiyo tulikuwa tunashauri jambo hilo. (Makofi)

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo tunashauri hapa; wataalamu wa uchumi wamesema sekta ya kilimo inachangia Pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 30, na Serikali yetu ya Awamu ya Sita imejikita kwenye kuwasaidia wakulima wetu; kwa sababu wanafahamu unaweza kuzunguka popote lakini jioni lazima ukumbuke chakula. Hata kama ukisema uende siku mbili, siku tatu, lakini ya nne lazima ule na chakula chetu lazima tukizalishe nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumepitisha hapa bajeti ya Serikali zaidi ya bilioni 900 ambayo inakwenda kwenye sekta ya kilimo. Ni katika historia hatujawahi kupitisha bajeti ya namna hii, lakini sasa wataalamu wetu bado wako nyuma. Tunaona kila mwaka maji yanapotea, kila mwaka tunasema mito imejaa wakati wa masika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba Wizara ya Kilimo, hakuna njia bora ambayo tunaweza kuwaokoa Watanzania kama tukiwekeza kwenye kilimo. Leo ukija pale katika Mkoa wa Tabora; huu ni Mkoa ambao uko kimkakati wa kulisha chakula mikoa ya Kanda ya ziwa, Kanda ya kati na Mkoa wa Dar es Salaam, pale chakula kingi kinatoka. Kule tuna mbuga nyingi nzuri ambazo zinatoa mchele mzuri, lakini leo mimi nashangaa hata kwenye Wizara yetu hatuna *block farm* hata moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo ielekeze Mkoa wa Tabora kutenga maeneo ambayo yatakwenda kusaidia kutengeneza *block farm* ambayo tuzalisha chakula ambacho kitalisha mikoa hiyo niliyoitaja.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale katika Jimbo langu la Igalula kuna maji mengi ikifika wakati wa masika yanaleta maafa katika Kata ya Loya na Miswati. Yale maji tukiyawekea mtiririko mzuri, tukaweka kilimo cha umwagiliaji, basi hata yale maafa ambayo huwa yanatokea kila mwaka katika Kata za Loya na Miswati hatutayaona. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ilete mipango ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la tatu. Tumetengeneza SGR, SGR hii ni kwaajili ya kwenda kufungua fursa ya kiuchumi katika nchi yetu, lakini tumeweka *lot* zaidi ya tano ambazo zinaendelea sasahivi katika ujenzi wa reli. Sasa, kuchelewa kwa miradi hii ambayo tunaweka fedha nyingi basi ndiyo tujue tunasababisha wananchi wetu kuchelewa kupata maendeleo kwa sababu wananchi wamefunga mikanda kusubiria miradi yao iweze kukamilika. Leo tunasema mradi wa SGR kutoka Dar-es-Salaam kuja Morogoro na kutoka Morogoro mpaka Dodoma umechelewa kwa zaidi ya miezi 12 na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukija kuangalia mradi ambao tumesaini wa kutoka Makutupora kwenda Tabora na Makutupora kwenda Kigoma ambao tunategemea utakamilika 2024 kwa *delay* hii ambayo tumeiona tunapata mashaka, kwamba kama tusipojipanga vizuri kama Serikali hata hiyo miradi haitakamilika kwa wakati. Mimi niombe Serikali kwenye hii miradi, ambapo tumeamua kufungua nchi, lazima tuwe *serious* ili tuweze kufikia malengo. Watanzania wana imani kubwa na Serikali yao, lakini watakuwa na imani kubwa kama hii miradi tukiifikisha na ikianza kuleta tija kwa wananchi wetu. Kwa hiyo lazima tuangalie jambo hilo.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo tunatakiwa tuliangalie, lazima tutengeneze viwanda vyetu vya ndani viweze kufanya kazi. Sasa, hatuwezi kutengeneza viwanda kama hatuna umeme wa kutosha. Leo tunapeleka umeme kila Kijiji, bado hatujaunganisha umeme kila Kijiji, lakini kuna tatizo kubwa la umeme katika nchi yetu kiasi kwamba sijawahi kuona. Vijiji vyenyewe mnasema tupeleke kule, bado hatujapeleka *resources* nzuri za kutosha ambazo zitakwenda kudhibiti upatikanaji wa umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi jiiombe Serikali kuna umuhimu wa kuhakikisha tunaharakisha bwawa letu la Mwalimu Nyerere ili likamilike haraka ili liweze kwenda kufungua nchi. Leo viwanda vinaendeshwa kwa gharama kubwa kwa sababu ya ukosefu wa umeme, lakini kama tukitengeneza umeme wetu wa uhakika na ukatufikisha katika vijiji vyetu, leo tunapeleka umeme kule angalao bora tungewaacha na *solar* zao zina uhakika zaidi kuliko umeme huu wa *TANESCO* ambao tunaupoleka. Dakika 10 umekatika, dakika mbili umerudi, taabu tupu inaendelea huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe Serikali, pamoja na nia njema ya kupeleka umeme kwa kila Kijiji lazima na sisi tujipange. Kule tunapeleka umeme watu wa Mwamabondo kule ambako hawajawahi kufikiwa na umeme wakiona shoti watafute *solution* kwa kutumia njia gani? Maana tunaweza kupeleka umeme kule, hakuna wafanyakazi, hakuna vifaa vya kuwawezesha *TANESCO* kufika kutatua na matatizo kule; tunakuwa tumepeleka matatizo kwa wananchi wetu. Kwa hiyo mimi nilitaka nichangie katika mpango huu ambao tunaenda kuujadili.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la mwisho ni kuhusu sekta ya ufugaji ambayo inasemekana inachangia baadhi ya pato katika mfuko mkuu wa Serikali. Hata hivyo wafugaji wetu tumewarundikia mrundikano wa tozo nyingi sana. Mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri, hebu pitieni hizi tozo. Kila siku, mara chanjo ya mapele, inakuja heleni, heleni yenyewe ambayo tunaiweka unaweza kuitengeneza hata kwa kupitia Wizara yako kwa shilingi 200, lakini mmempa mzabuni anaenda kuwatoza wafugaji shilingi 1,700. Bora hata ingekuwa inaingia kwenye Serikali wananchi wajue wanaisaidia Serikali kuingiza mapato yataenda kuwaletea maendeleo, lakini inakuwa fedha hii inaingia mfukoni mwa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kandege.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ili na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji jioni ya leo. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, kwa hiyo mchango uliotolewa na kamati mimi ni miongoni mwa waliochangia. Hata hivyo kwa jioni ya leo nitaomba nichangie maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kujikita zaidi katika eneo linalohusu gharama za usafirishaji na jinsi ambavyo zinaongeza gharama kubwa katika ufanyaji wa biashara katika nchi yetu. Kipindi cha mwaka jana tukiwa hapa Bungeni sisi Waheshimiwa Wabunge tulipata fursa ya kugawiwa kitabu ambacho kimeandikwa na

8 NOVEMBA, 2022

Mtanzania mwenzetu, Ndugu Erastus Mtui chenye jina la “*Poverty Within Not on The Skin*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge tupate fursa ya kukipitia kitabu hiki, kina elimu ya kutosha na hasa kwa watunga sera ni kitabu cha lazima cha kukisoma. Nilikuta katika ambao wame-*recommend* kitabu hiki kisomwe ni pamoja na Prof. Kitila Mkumbo. Hakika kitabu hiki kinatoa elimu ya kutosha na kinatufaa Watanzania. Tanzania tuna watu wazuri ambao ni vizuri tukaunga mkono kazi nzuri wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma katika ibara ya sita ya kitabu hiki unakutana na maongezi kati ya bilionea Aliko Dangote pamoja na Mo Ibrahim wakiwa wanaeleza jinsi ambavyo gharama ilivyokuwa kubwa kuchukua mzigo kutoka mpaka mmoja ndani ya Afrika kwenda upande wa pili wa Afrika. Ni wakati muafaka mpango wetu ujielekeze ni namna gani tunaenda kuboresha ufanyaji biashara. Maana ni ukweli usioplingika, ukishaweka gharama kubwa katika usafirishaji tafsiri yake ni kwamba gharama za mlaji lazima ziongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ambayo napenda niongelee kwa kirefu zaidi ni kuhusiana na mpaka wetu wa Tunduma. Wako Wabunge waliotangulia kuchangia, wanaeleza jinsi ambavyo kuna ugumu wa mpaka ule kufanya kazi vile ambavyo inatakiwa. Ni ukweli usioplingika inafika kipindi ambapo malori yanakaa mpaka siku nne mpaka siku tano bila kuvusha mzigo. Tafsiri yake ni kwamba tunaharibu uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kipekee niipongeze Serikali imefanya kazi kubwa sana katika ujenzi wa barabara. Ni wakati muafaka sasa tufungue *corridor* ya kupitia Tabora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwenye lori anataka kusafiri kutoka Mwanza kwa kwenda mpaka Tunduma anaenda kilometa 1,400, mpaka kwenda kufika mpaka wa Tunduma na Nakonde; lakini huyohuyo aliyekuwa na mzigo kutoka Mwanza akipita Tabora – Sikonge – Mpanda mpaka kufika Sumbawanga na kufika Kalambo, *Kasesha Border*, ni kilometa 1,000 tu; maana yake anaokoa zaidi ya kilometa 400, kiuchumi tunaharibu uchumi kwa kupita umbali mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama kuna mtu ambaye anasafirisha mzigo kutoka mpakani mwa Tanzania na Uganda kwa maana ya Mutukula mpaka kwenda kufika Tunduma ni kilometa 1,700; lakini akapita *short cut*, akapita Tabora – Mpanda – Sumbawanga na mpaka kufika Kalambo ni kilometa 1,080 tofauti ya kilometa 620. Kama hiyo haitoshi, gari limefika hapo likiwa na shehena ya mzigo, aidha inaenda upande wa pili au inakuja upande wa kwetu sisi, lori likikaa siku zaidi ya tatu mpaka siku nne ni gharama kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali, katika mipango ya kuhakikisha kwamba, tunaboresha ufanyaji biashara na kupunguza gharama katika ufanyaji biashara ni kazi ndogo tu, mawasiliano kati ya Serikali yetu ya Tanzania ambayo naamini tuna mahusiano mazuri na Serikali upande wa pili wa Zambia, kufanya mpaka wa Kasesha ufanye kazi saa 24 kama ilivyo Tunduma. Tafsiiri yake ni kwamba, badala ya malori kukaa muda mrefu

8 NOVEMBA, 2022

Tunduma yataka mengine yataenda kupita Kasesha, na hivyo kufanya mzunguko wa kibiashara kuwa mkubwa. Ni kama ambavyo mwanzo kulikuwa na hofu kwamba kukiwa na *Kasimuro Border* ikiwa inafanya kazi itapunguza biashara Tunduma, lakini ukweli ni kwamba, *frequency* za kusafiri zitakuwa nyingi na kibiashara hakika uchumi utachehemka na itasaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa haina maana kujenga barabara za lami kwenda Tabora, Sikonge, kama barabara hizi zitakuwa unasubiri malori, ulione lori moja baada ya wiki. Na kimsingi naomba nipongeze wanaoenda Kigoma na Burundi wameanza kutumia hii *route*. Sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kutoa hamasa; na hii itapunguza hata uharibu wa barabara ya kwenda Tunduma kwa hiyo, hata hiyo itakayokuwa inajengwa itakaa muda mrefu, tutahudumia magari mengi, shehena itakuwa kubwa na gharama ya ufanyaji biashara itakuwa ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonesha kwamba, usafirishaji wa mizigo kwa nchi za Afrika Mashariki ni asilimia 30 gharama zaidi ukilinganisha na nchi za Kusini mwa Asia. Ukilinganisha na Marekani gharama zetu ziko kubwa zaidi kwa asilimia 60 mpaka 70. Sasa kwa vyovyote vile mlaji wa mwisho ndiye anaumia. Ni wakati muafaka mpango huu ukatafsiri kwa vitendo maana hakuna uwekezaji mkubwa ambao unahitajika, ni suala la kuhakikisha tu kwamba tunafungua hiyo *corridor* na inaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

8 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kunipa nafasi. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada za kuleta maendeleo katika nchi yetu. Pia nimpongeze Waziri mwenye dhamana kwa kuwasilisha mpango ambao kama utafuatwa utakuwa na manufaa ya siku za baadaye. Niipongeze Kamati ya Bajeti kwa mawazo yao mazuri sana ambayo wameishauri Serikali. Mimi naamini mawazo yaliyowasilishwa na Kamati ya Bajeti mengi ni yale ambayo Wabunge wengi wamekuwa wakiishauri Serikali lakini kwa bahati mbaya huwa hayatekelezwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu kwenye sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo ni sekta ambayo inawagusa wananchi wengi hapa nchini. Na Serikali kama inadhamira ya dhati kuwasaidia kundi kubwa la wakulima watakuwa na maendeleo makubwa sana na nchi itanufaika. Lakini kilimo ambacho tunakishauri kwa Serikali ni uwekezaji mkubwa ambao lazima Serikali iwe na dhamira ya dhati kuhakikisha wanatoka kwenye kilimo cha kubahatisha tuingie kwenye kilimo ambacho kina uhakika, cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina maeneo mapana ambayo tuna maziwa na mito mikubwa ambayo haitumiki vizuri. Maeneo mengi yanafaa kwenye shughuli za kilimo lakini kwa bahati mbaya nchi yetu ilishakuwa na mabadiliko ya tabia nchi. Sasa kwa kuwa kuna mabadiliko ya tabia nchi, lazima Serikali ije na mkakati wa kutumia rasilimali zilizopo kwa ajili ya kuwasaidia wakulima ili waweze kulima kilimo ambacho kina uhakika.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, matajiri wote duniani wanatengenezwa na Serikali. Kama Serikali haijawatengeneza matajiri, huwezi kuwapata. Matajiri hao ni hao hao Watanzania ambao wapo. Wanachohitaji ni uwezeshwaji. Rasilimali ya kwanza waliyonayo ni ardhi ambayo haijatumika vizuri kwa sababu taasisi nyingi za fedha hazitoi mikopo kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha, tuache mipango ile ambayo haitekelezeki. Tumeanzisha Benki ya Kilimo ambayo kimsingi haijamkaribia sana mkulima. Taasisi zile za fedha tunaomba ziandae mpango mkakati ambao utakuwa chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha wanawawezesha wakulima ambao wanaweza wakatoa tija kwa kiwango kikubwa sana. Naomba hili mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwenye Sekta ya Kilimo ni kuwawezesha wakulima watoke kwenye kilimo cha jembe la mkono. Wakulima wengi wanalima kilimo cha kujikimu, wawezesheni wapewe zana za kisasa, sambamba na kuwawezesha kuwapa eneo la masoko, itawafanya wakulima wawe na manufaa na watu wengi watakimbilia kwenye Sekta ya Kilimo. Naomba hili Serikali ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo maeneo ambayo Serikali ikiwawezesha katika eneo la masoko, kwenye sekta ya kilimo kutakuwa na ukuaji mkubwa sana, Tumezungukwa na nchi ambazo uzalishaji wake ni mdogo...

8 NOVEMBA, 2022

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba pamoja na wakulima kutumia jembe la mkono, lakini wakulima hao hao kwenye korosho mwaka huu wamepata shilingi bilioni 300, kwenye tumbaku shilingi bilioni 600, kwenye pamba shilingi bilioni 275, lakini hawana matrekta. Pia mabenki hayo hayo yametangaza riba kutoka 15% mpaka 9% lakini kwa wakulima bado masharti ni makubwa sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Moshi Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo ambayo ameitoa Mheshimiwa Cherehani, ingawa bado pamoja na hiyo taarifa tunayopata, tija ni ndogo. Kipato wanachokipata wakulima bado hakitoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wetu kwa Serikali, tuwekeze kwa kiwango kikubwa kwenye sekta ya Kilimo. Pamoja na kwamba mwaka huu Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kutoa ruzuku ya pembejeo, lakini kwenye maeneo ya kilimo cha umwagiliaji na uwezeshaji mkubwa kwenye sekta hiyo ya kilimo kutoka kwenye jembe la mkono kwenda kwenye kilimo cha kisasa ni muhimu sana.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nashauri Serikali ni miradi inayowekezwa na Serikali kwenye sekta ya ujenzi. Nakubaliana na wachangiaji wenzangu ambao wamechangia kwamba Serikali iachane na mpango wa kuanzisha miradi midogo midogo hasa ya ujenzi wa barabara. Ujenzi huu utafanya Serikali iwe inatumia gharama kubwa lakini tija yake inakuwa ndogo. Mwaka huu tulipitisha bajeti na mpango uliopita wa mwaka jana 2021, walionesha kila eneo kwamba wanaweza kupeleka Kilometa 25, kitu ambacho hakiwezekani. Ni lazima Serikali iwe na mpangilio wa maeneo ya kipaumbele cha kujenga miradi ya maendeleo. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeisaidia sana Serikali kuliko kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shabiby ameishauri Serikali kujenga miradi ya maendeleo ya ushirikishaji wa PPP na ile ambayo imekuja Wizara ya Fedha ya EPC iliyopendekezwa. Tunaafikiana nayo, lakini hoja yetu hapani kwamba iharakishe mpango mkakati kuliko iliyopo tu kwenye mipango ya kwenye makaratasi. Tunaishauri Serikali iharakishe mpango huu, utasaidia kufanya maboresho makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Serikali ni vyema ikapeleka miradi ya maendeleo ni kwenye maeneo ambayo yatakuwa yana *return* ya urejeshaji wa fedha zilizowekezwa kwa kiwango kikubwa. Tunajenga reli. Reli ambayo ina manufaa makubwa ni reli ya kutoka Tabora kwenda Kigoma; reli ya Kaliuwa - Mpanda - Karema. Hizo ndizo reli ambazo zina uwezo mkubwa kuweza kutoa manufaa makubwa sana. Serikali imewekeza uwekezaji mkubwa wa Bandari ya Karema.

8 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenekiti, sasa hivi wafanyabiashara wa DRC Congo walishaanza kusafirisha shaba kwa njia ya mashua ambayo inatuharakisha sisi tupokee kwamba ni fursa iliyopo, tuweze kuitumia vizuri. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali mchango mkubwa wa uwekezaji wa reli uwekezwe kwenye reli ya kutoka Tabora kwenda Kigoma na kile kipande cha kutoka Uvinza kwenda Msongati hadi Burundi. Hata hivyo, reli ya Kaliuwa - Mpanda hadi Karema ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie miradi ya maji. Tuna miradi ya maji mingi midogo midogo ambayo haiwasaidii Watanzania. Tukichukulie mfano wa Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa, ni mikoa ambayo imezungukwa na maziwa. Kwa bahati mbaya, hakuna mradi mkubwa wowote unaounganisha miradi hii ya maji. Naomba tutumie fursa tulizonazo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nizungumzie suala la uvunaji wa hewa ya ukaa. Tanzania ina misitu mingi na Wizara tumeishauri mara kwa mara na kwa bahati mbaya hawajaitumia hii fursa vizuri. Wenzetu Kenya wanaitumia fursa ya uwekezaji mkubwa kwenye uvunaji wa hewa ya ukaa. Kwa nchi yetu sasa hivi tuna maeneo kama matatu; Mkoa wa Katavi, Kiteto, eneo la Mkoa wa Manyara na Ruvuma, wameanza uvunaji lakini kwa kiwango kidogo sana. Tunaomba sasa Serikali ije na sheria mpya ambayo itafanya mabadilko hata kwenye maeneo ya hifadhi za Taifa, tuweze kuvuna hewa ya ukaa kama wenzetu Kenya wanavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekuwa tukitoa mawazo haya na kwa bahati mbaya sana Serikali haifanyii kazi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, itumie

8 NOVEMBA, 2022

nafasi hiyo ili muweze kupata fedha nyingi ambazo wenzenu jirani Kenya wanazipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye sekta ya utalii. Utalii ulielekezwa ukanda wa Kaskazini, lakini nchi yetu ina maeneo mengi ambayo yana vivutio vya utalii na kwa bahati mbaya havijatumika vizuri. Naomba na maeneo hayo yafanyiwe kazi. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango mzuri. Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:

(Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wamekwisha. Nawapongeza kwa michango mizuri. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, na Serikali mko hapa, hili suala la kilimo kama hatuku-engage *private sector* wa ndani na wa Kimataifa, hatuwezi kufika malengo. Kama Serikali sasa mmeamua kufanya PPP kwenye miundombinu ya barabara, mwende kwenye kilimo. Fikra za kizamani za kasumba ya ubepali na unyonyaji kwenye kilimo cha watu binafsi tuachane na hizi fikra sasa hivi. Tunahitaji chakula, tumezungukwa na Mataifa sasa hivi nchi zote, hakuna ardhi, ardhi imebaki Tanzania tu. *(Makofi)*

Serikali i-*regulate*, iweke utaratibu mzuri wa kuingia ubia na *private sectors*. Leo tunaagiza ngano kutoka Ukraine, tunaagiza vyakula kutoka nchi za nje, *it is very*

8 NOVEMBA, 2022

wrong. Kwa hiyo, nafikiri mwekeze sana kwenye kilimo na mtumie utalaam wa nje. Tunafanya sasa hivi *irrigation*, lakini *irrigation* yetu ni *canal irrigation* ambayo inatumia maji mengi sana, yanapita yanaondoka. Lazima twende kwenye *drip irrigation* ya kuhifadhi maji ili yasije yakapotea kwa wingi.

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.52 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 9 Novemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)